

IMAM MAHDI (A.S.)

**IMAM WA ZAMA HIZI NA
KIONGOZI WA DUNIA**

Kimeandikwa na:
Mulabbah Saleh Lulat

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 – 9987 – 17 – 089 – 0

Kimeandikwa na:
Mulabbah Saleh Lulat

Kimehaririwa na:
Alhaji Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitiwa na:
Mbaraka A. Tila

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Decemba, 2014
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

**“Yeyote anayekufa bila ya kumjua Imam wa zama zake basi amekufa kifo cha kijahiliyyah (zama za kijahiliyyah: zama kabla ya Uislamu).”
Mtukufu Mtume (saww)**

**Kwa jina Lako tukufu
Kimeanza kila kitu
Peke Yako twakusifu
Wote watu Mola Wetu
Uwezo na utukufu
Ni Wako Mola wa watu
Ewe Rasuli, Mkweli na Mwaminifu,
Rehema kwa wote alamina,**

Rehema na amani za Mola zipo daima juu yako toka alipoumba nuru yako, Malaika wote wanakutakia rehema na amani, Na wote kaumu ni wajibu kukusalia, Nani kama wewe ewe mbora wa viumbe wa Mola? Huyu ni Al Mahdi nuru na fakhari ya kizazi chako, Kwa upanga wako, joho lako na kilemba chako atatokomezwa wote ukafiri, Kila aina ya ukoma na udajali: ufalme, demokrasia, ukomunisti, ubepari, ulahidi, ushirikina, utaghuti, dini mseto,... vyote vitatoweka na kubaki Nuru ya Mwenyezi Mungu. Wanaokukejeli Abtaru¹ na wakapambana na wewe, wote hawa batili wametoweka zahakani² kama povu la baharini, Mola alikupa Kauthari, Aali Muhammadi, kizazi kilicho bora minal Awwalina wal Akhirina, Yawatosha utukufu kwamba asiyewasalia, yake sala ni batili, Sana umemtaja na kumbashiri huyu mtukufu wa kizazi chako, Katika kitabu hiki nimeyakusanya ya hamu ili Waislamu wayafahamu, Na pia wote kaumu, wenye akili huru na nyoyo zenye harara, Nataraji wako uombezi na radhi zako.

Ya Qaima Aali Muhammad, Ya Saahibaz Zamaan

¹ Abtaru: katika kiarabu asiye na kizazi. Makafiri walimkejeli Mtume kwamba hana watoto wa kiume. Kwa hiyo hana kizazi cha kumrithi na kuendeleza kazi yake. Pia wako Waislamu wanaoshikilia fikra hiyo.

² Zahakani: latokana na ‘ZAHAAQA’ yenye maana ya kuangamia, kutoweka

Ewe Khalifa wa Mwenyezi Mungu na Khalifa wa baba zake walioongoka!

Ewe Wasii wa Mawasii waliotangulia!

Ewe mwenye kuhifadhi siri za Mola wa walimwengu!

Ewe Bakisho la Mwenyezi Mungu kutokana na wabora walioteuliwa!

Ewe mtoto wa Nuru zing'arazo!

Ewe mtoto wa Mabwana watukufu wenye nuru!

Ewe mtoto wa kizazi kilichotoharika!

Ewe machimbo ya elimu ya Mtume (saww)!

Ewe mlango wa Mwenyezi Mungu, (mlango) wa pekee wa kuingilia Kwake!

Ewe njia ya Mwenyezi Mungu ambayo asiyeipita lazima ataangamia!

Ewe mwenye kutazama Mti wa Neema (Tuba) na Mkunazi wa (upeo wa) mwisho kabisa!

Ewe nuru ya Mwenyezi Mungu isiyo-zimwa!

Ewe Hujjah (Hoja) ya Mwenyezi Mungu isiyofichwa!

Ewe Hujjah wa Mwenyezi Mungu kwa wote walio ardhini na mbinguni!

Ewe Hujjah juu ya waliotangulia na kwa watakaokuja!

Ewe Mtukufu ambaye nyuma yako atasali Neno na Roho wa Mwenyezi Mungu!

Ewe Kiongozi wa Hizbullahi, ambalo ndilo kundi la wenye ushindi!

Hakika watetezi wako ndiyo wenye kufuzu!

Na maadui zako ndiyo wenye hasara!

Na hakika wewe ni hazina ya kila elimu!

Na mfunguaji (mpasuaji) wa kila kili-chofungwa!

Na msimamishaji wa kila haki!

Na muondoshaji wa kila upotofu!

Ewe Bwana wangu mwelekezaji! Nimekuridhia wewe kuwa ndio Imamu wangu, kiongozi, na bwana!

Kamwe, simtaki yeyote badili yako na wala sitamchukua bwana mwigine zaidi yako!

Nashuhudia ya kwamba wewe ndiyo haki iliyo thabiti na isiyo na kasoro yeyote!

Na kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu kuhusu wewe ni haki. Kamwe sina chembe ya shaka kwa urefu wa ghaiba hii na umbali wa zama!

Nasubiri na kutegemea siku zako (za kudhihiri)!

Na wewe ni mwombezi usiye na upinzani!

Na mpenzi (wa Mwenyezi Mungu) usiyerudishwa nyuma!

Tafadhali pokea kazi hii dhalili kutoka kwa mja dhaifu!

Ushike mkono wangu, ili nibusu mikono yako mitakatifu!

Inua yako mikono yenye tohara, kubuli na kila utukufu

Niombee dua...

SHUKRANI

Al Mahdi Centre,

Nyinyi ndio chemchemi

Ya haya maji matamu

Hisani haina tarjumi

Haya shikeni hatamu

Mola awape uchumi

Mfanye kazi karimu

Umm Zahra,

Juhudi zako si haba,

Nyingi ndani ya kibaba

Mola akupe mahaba,

Ya wakweli masahaba

Akujaze mara saba,

Kwa kila punje ya haba

Alhajj Kurban Khaki

Mwenyezi Mola wadudi

kwa zako nyingi juhudi

Akupe mengi ya sudi

mazuri yasiyo rudi

msaada wako umewezesha kazi hii.

Kwa Kila mwanafunzi wa dini,

Kila mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, utume na Kiyama,

Kila mwenye kutaraji amani na haki duniani,

Kila mwenye akili huru na moyo wenye harara,

Kila Mwislamu anayekerwa na umadhehebu, na anatamani umoja wa

Umma wa Kiislamu,

Kitabu hiki ni nuru na mwongozo, kisomeni.

YALIYOMO

Neno la Uchapishaji.....	1
Utangulizi.....	3
MAIMAMU KUMI NA WAWILI:.....	6
Makhalifa wa Mtume (as) na Viongozi baada yake.....	6
Uislamu ni Mfumo kamili:.....	6
Uongozi ni uti wa mgongo:.....	6
Ukhalifa baada ya Mtume (saww):.....	8
Hadithi ya Ghadir Khum:.....	11
Hadithi ya <i>Thaqalayn</i> (vizito viwili):.....	11
Hadithi ya Safina:.....	11
Hadithi ya Makhalifa Kumi na wawili:.....	12
Muhimu kuzingatia:.....	13
IMAM MAHDI (A.T.F.) NI IMAMU WA KUMI NA MBILI:	15
Dalili kutoka katika Qur’ani:.....	18
A - Imam Mahdi Katika Sahih Sita (Vitabu Sita Sahihi vya Hadithi):	20
B - Maimamu wa Ahlulbait (a.s.) na Imam Mahdi.....	21
C –Uchambuzi wa Kitaalamu wa Hadithi kuhusu Imam Mahdi (as).....	27
Dalili za Kihistoria.....	43
A – Baadhi ya watu waliodai UMahdi na Waliosingiziwa UMahdi	43
1 – Waliodai UMahdi	43
2 – Watu waliodhaniwa UMahdi.....	49

B – Kauli za Ulamaa wa Kisunni kwamba Imam Mahdi ndiye bin Imam Hasan Askariy (as)	54
--	----

**VITABU KUHUSU GHAYBAH VILIVYOANDIKWA
KABLA YA KUZALIWA IMAM MAHDI (AS) 65**

Bishara katika vitabu vingine.....	66
------------------------------------	----

MLANGO WA 2: HISTORIA YA IMAM MAHDI (AS)..... 71

1 – Imam Mahdi ni Nani?	71
2 – Kuzaliwa na Kuonekana	73
3 – Ghayba ndogo (Sughra)	79
4 – Ghayba kubwa (Kubra).....	82
Visa vya kweli kuhusu kukutana naye	90
Baadhi ya Miujiza.....	98

**MLANGO WA 3: ALAMA ZA KUDHIHIRI NA
SERIKALI YA HAKI 133**

1 – Alama za kudhihiri Imam	133
Alama Thabiti, lazima zitatokea	133
1 – Kuenea dhulma na ukandamizaji	137
2 – Kuja kwa Dajjal	138
3 – Sufyaniy	138
4 – Bendera Nyeusi kutokea Khorasan	145
5 – Sauti kutoka Mbinguni.....	145
6 – Kuteremka Nabii Isa (as) na kuswali nyuma ya Imam Mahdi (a.t.f.)	146
7 – Al-Yamaniy	146

8 – Kupasuka ardhi hapo Baidaa.....	146
9 – Kuuliwa Nafsi Zakiyya.....	146
10 – Sayyid Hasaniy	147

**SERIKALI YA KIISLAMU ZAMA ZA GHAYBA,
KABLA YA KUDHIHIRI IMAM MAHDI (A.T.F.) 147**

2 – Mapambano dhidi ya Dhulma	148
Vita vya Dunia.....	148
Hali ya Hijaz karibu na kudhihiri Imam.....	149
Kuteremka Nabii Isa (as) kutoka Mbinguni	155
3 – Serikali moja ya Mungu Duniani yenye haki na uadilifu	158
A – Allahkrasia	159
Nidhamu ya Utawala wa Imam:.....	159
Allahkrasia:.....	159
Imam na msaada wa Malaika:	160
Sifa za masahaba wa Imam Mahdi (as):.....	160
Masharti ya Imam wa Zama (as) wakati wa kiapo cha utii:....	161
Mshika bendera wa Imam (as):	162
B – Zama za amani na haki.....	163
Kipindi cha utawala wa Imam Mahdi (a.t.f.):.....	163
Kushamiri Haki na Uadilifu:	163
Kutokomeza mizizi ya dhulma na kusimika Uadilifu	163
Uwingi wa Neema na Utajiri zama za Serikali ya Imam Mahdi (a.t.f.)	164
Muhimili wa Neema:	164
Neema na Baraka kwa wingi:	165
Amri ya Imam Mahdi (as) kwa wawakilishi wake kote duniani:	166

Maendeleo ya sayansi na teknolojia:	166
Safari katika anga na sayari za mbali:	168

MLANGO WA 4: HAZINA / URITHI ALIYOTUPA

IMAM MAHDI (AS) 170

1 - Mwongozo na mafunzo kupitia wawakilishi wake zama za Ghayba Ndogo:.....	170
2 - Ghayba Kubwa	170
3 - Baadhi ya dua, Ziyarah na mafunzo:	170
Dua ‘Ahd	171
Dua Faraj	173
Ziyarah ya Imam Mahdi (as).....	174

HITIMISHO NA MAFUNZO 191

1 - Maimamu, Makhalfu baada ya Mtume (saww) ni kumi na mbili:	191
Kwa nini Maimamu hawa siyo maarufu?.....	192
2 - Kwa nini imani ya Mahdi imetelekezwa?	193
3 - Itikadi ya Imam Mahdi (as) ni Sahihi:.....	194
4 - Ushia wa Ahlul Bayt (as) ndiyo Uislamu halisi:	194
5 - Uimamu, Ukhalifa wa Allah ndiyo msingi wa kusimamisha Umoja wa Ummah:.....	195
6 - Matunda ya Mti wa Utume uliobarikiwa:	197
7 - Tuache kutetea mifumo batili:	198
8 - Kila anayemsubiri Mahdi, lazima kujiepusha na udhalimu na kupambana:.....	200
9 - Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ni mfano wa kuigwa na kujivunia kwa Waislamu wote:	200

10 - Nidhamu ya Mahdi (a.t.f.) siyo nidhamu ya kubweteka na kumsubiria aje kufyeka uovu na kuung'oa:	201
11 - Imam Mahdi (a.t.f.) na Umadhehebu:	201
12 - Mahdi wa Kisunni na Mahdi wa Kishia:	202
AMBATANISHO	204
Ambatanisho 1: Mkabala na Allamah Harun Yahya kuhusu Imam Mahdi (as)	204
An Interview with Harun Yahya:	204
1. To what extent is belief in the Mahdi prevalent in the Sunni faith today? Can you give a percentage?	204
2. Does belief in the Mahdi have a widespread influence on all classes, on all sections of society, in Sunni Islam, or have some certain sections adopted it more than others?	205
3. What are your personal and religious views on those people who have previously declared themselves to be the Mahdi (Ibn Tumart, Muhammed Ahmed, and Manisali Mehmet in 1930s Turkey)?	206
4. How can a false Mahdi be distinguished from the true Mahdi?	207
5. What kind of relationship will there be between the Prophet Jesus and the Mahdi when both are on the earth?	209
6. Could you describe your analysis of the hidden imam in Shiite belief?	209
7. What would your thoughts be regarding someone who declared himself to be the Mahdi today?	211
8. If someone claiming to be the Mahdi emerged today or in the near future, how should you or a devout Sunni Muslim react?	214

9. What do you think about the claim that Muqtada al Sadr is the hidden imam or represents the “army of the Mahdi” since the coming of the Mahdi is close at hand? ... 214

AMBATANISHO LA 2:..... 219

- Wasifu wa Allamah, Muhaddith Abdullah bin Sadik 219

AMBATANISHO LA 3:..... 224

- Shaykh Hisham Kabbani, msufi wa tariqa ya Naqshbandi ni mmoja wapo wa ulamaa wenye kuthibitisha imani ya Imam Mahdi 224

AMBATANISHO LA 4:..... 226

- Fatwa za Mashaykh wa ki-Sunni 226

AMBATANISHO LA 5: 226

- Msimamo sahihi wa ma-Sunni kuhusu maimamu kumi na mbili 226

AMBATANISHO LA 6:..... 230

- Orodha ya Baadhi ya Vitabu mashuhuri vilivyoandikwa kuhusu Mahdi..... 230

- Misamiati 235

REJEA 237

- A – Vitabu 237

- B – Mitandao (Websites): 239



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako kimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa jina la “**Imam Mahdi (a.s) Kiongozi wa Zama**” kilichoandikwa na Sheikh Mulabah Saleh Lulat.

Kitabu hiki kwa ujumla huelezea uwepo wa Imam Mahdi (a.s) ambaye ni Imam wa Zama hizi kama ilivyotabiriwa na mtukufu Mtume (s.a.w.w) mwenyewe.

Imam Mahdi (a.s) yuko hai lakini macho yetu hayamuoni kwa vile Allah (swt) amemuweka katika *Ghaibat kubra* a (ghaibu kubwa), kutokana na urefu wa ghaibu hii watu wengi wamefikia hitimisho kwamba Imam huyu hayupo au alikwisha tokea zamani na kuondoka, kwa hiyo hakuna tena cha Imam Mahdi. Haya ni mawazo ya watu wavivu wa kufikiri na waliokata tamaa.

Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alipokuwa anatoa bishara hii ya kuja kwa Imam Mahdi (a.s) kutoka katika kizazi chake alisema kuhusu urefu wa *ghaibat* yake na akanuliwa akisema kwamba “*Ghaibat* yake itakuwa ndefu sana kiasi kwamba imani ya kuwepo kwake itabaki kwa watu wachache sana - hawajai hata katika kitengele cha mkono.” Kwa hiyo sio ajabu kwa sasa kuona watu walio wengi kutokuwa na imani ya kuwepo kwake - kwani hilo lilikwisha tajwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kabla.

Hadithi sahihi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kuhusiana na suala hili utazikuta ndani ya kitabu hiki, zilizosimuliwa na wanachuoni wote wa Kiislamu - Shia na Sunni.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa makubwa hususan wakati huu wa sayansi na tekinolojia kubwa ambapo ngano, hadithi za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo kwa sasa havina nafasi katika akili za watu.

Tunamshukuru ndugu yetu **Sheikh Mulaba Saleh Lulat** kwa juhudi zake kubwa alizofanya na kufanikiwa kupatikana kwa kitabu hiki muhimu kwa lugha ya Kiswahili, pia shukrani zetu ziwaendee wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine mpaka kuwezesha kitabu hiki kuchapishwa. Allah (swt) awalipe wote malipo mema duniani na Akhera pia.

MCHAPISHAJI
AL-ITRAH FOUNDATION

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Leo ulimwengu unaelekea taratibu kwenye utandawazi tukishuhudia nguvu zinazomkana Mwenyezi Mungu na mfumo wake zikijitahidi kutawala ulimwengu mzima kwa kuwa na serikali moja na kiongozi mmoja anayehukumu kwa sheria za kikafiri. Huu ndiyo *Utandawazi* ambao malengo yake ni kuwa na serikali moja itakayotawala kimabavu dunia nzima kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa sheria za kitaghuti.

Ikiwa mataghuti wanalenga kutawala dunia yote na ulimwengu wote unyenyekee kwenye hukumu zao, je waumini tunalenga nini? Je Mwenyezi Mungu ametuahidi nini? Je ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba Yeye atashinda pamoja na waumini (58:21, 3:12, 8:36) na kwamba Yeye hatawapa makafiri ubwana juu ya waumini (4:141) iko wapi?

Historia inathibitisha, Qur'ani inaweka wazi kwamba Mwenyezi Mungu daima yu pamoja na waja Wake wema, amewasaidia na kuangamiza waovu.

Na pia Uislamu ukiwa ndiyo dini ya mwisho, kwa nini usienee ulimwengu mzima na kushinda dini zote na hivyo kuhakiki ushindi wa Mwenyezi Mungu, Mitume Wake na wote Waumini?

Kuwepo Imamu ambaye anakamilisha sifa za kuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu ni jambo muhimu na la lazima ili umma kupata nguvu na umoja. Hakuna jamii wala mfumo usiokuwa na kiongozi. Ni muhimu kwa kila muumini kumjua kiongozi wake na kumfuata.

Imani ya kwamba dunia haitamalizika na Kiyama kusimama hadi pale Uislamu utakaposhinda na Imam Mahdi (as) kutoka katika kizazi cha Mtume (saww) kusimama kama kiongozi na mtawala wa dunia yote ni thabiti wala haina shaka kwa Waislamu wote. Imani hii ipo pia miongoni mwa dini nyingine.

Habari kuhusu Imam Mahdi (as) chimbuko lake ni Mtukufu Mtume (saww) ambaye alielezea mambo yatakayotokea zama za mwisho. Hakuna aliye bora kujua na kutabiri mambo ya zama za mwisho kuliko Mtume (saww). Ikiwa Mitume waliotangulia waliwaelezea kaumu zao habari hizo, basi Mtume (saww) alielezea kwa mapana na marefu. Pia Maimamu wa Ahlulbayt (as) wote kwa zama zao, walielezea mambo hayo na kuyapa umuhimu wake mkubwa.

Wataalamu na wachambuzi wa mambo ya siasa bila shaka wanaelewa ya kwamba utandawazi (*globalization*) ni mfumo unaoipeleka dunia kuwa chini ya utawala wa ubeberu na mabepari wanaomiliki mitaji ya makampuni makubwa (*Transnational Companies*.) duniani. Wamiliki wa makampuni haya ni Mayahudi, Mazayuni ambao sera zao ni kumkana Mungu na kueneza ufisadi ili kutawala dunia. Dunia imejaa kila aina ya dhulma na ukandamizaji. Hali hii haiwezi kuendelea kwani Mwenyezi Mungu ana taratibu Zake. Dhulma ni jengo ambalo limejengwa juu ya tope. Kadiri linavyozidi kupanda ndivyo linavyotitia na kubomoka. Waovu huangamizwa na mwisho mwema ni wa wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu (7:128, 11:49, 28:83).

Dunia haiwezi kukombolewa ila kwa kupatikana kiongozi ambaye ana nguvu na uwezo, wa kielimu, kimwili na kiroho, kuongoza dunia nzima. Kiongozi huyo bila shaka ni Imam Mahdi (as).

Kitabu hiki kinafafanua kwa uwazi na kwa lugha nyepesi historia ya Imam Mahdi (as). Pia kinatoa dalili kuhusu kuwepo Imam Mahdi (as) na umuhimu wa kuwepo Imam kama huyo.

Kitabu hiki ni hoja dhidi ya wale wote ambao ni wapotoshaji wenye malengo ya kujenga mfarakano katika Umma huu kwa kudai eti kuna ‘Mahdi wa Kisunni’ na ‘Mahdi wa Kishia’. Kitabu hiki ni muhimu kwa kila muumini na wote wapendao amani.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MAIMAMU KUMI NA WAWILI

MAKHALIFA WA MTUME (AS) NA VIONGOZI BAADA YAKE

Uislamu ni mfumo kamili:

Uislamu ni mwongozo kamili kwa walimwengu wote hadi siku ya Kiyama. Maana ya kamili ni kwamba unamuongoza mwanadamu katika kila nyanja ya maisha yake iwe kiroho au kimwili. Uislamu una mfumo wake kisiasa, kiuchumi na kijamii. Huu ni mfumo ameuweka Mwenyezi Mungu ili kumwezesha mwanadamu kufikia ukamilifu, ustawi na fanaka hapa duniani na kesho Akhera na kusimamisha utawala pekee wa Mwenyezi Mungu.

Uongozi ni uti wa mgongo:

Nafasi ya mfumo wa uongozi katika kila jamii ni sawa na nafasi ya kichwa kwa kiwiliwili. Kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu amelipa jambo hili umuhimu mkubwa. Qur'ani imetubainishia uongozi gani Mwenyezi Mungu anaouridhia kuongoza na akatusisitiza tuwafuate hao viongozi wema waliochaguliwa na tujiepushe na mataghuti ikiwa kweli sisi tumeamini. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٢٣﴾ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٢٤﴾ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuh na watoto wa Ibrahim na watoto wa Imran juu ya walimwengu wote. Ni kizazi cha wao kwa wao na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.” (3:33-34)

أُولَئِكَ الَّذِينَ آتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ فَإِنْ يَكْفُرْ بِهَا هَتُّوْلَاءٍ فَقَدْ وَكَلْنَا بِهَا قَوْمًا لَيَسُوْا بِهَا بِكْفِرِينَ ﴿٨٩﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهِدَاهُمْ أَقْتَدَهُ قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٩٠﴾

“Hao ndio tuliowapa Kitabu na hukumu na utume. Kama hawa wakiyakataa, basi tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao. Sema: Siwaombi ujira juu ya haya. Haikuwa hiyo ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.” (6:89-90)

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَى فَيُضِلَّكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّ الَّذِينَ يَضِلُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا يَوْمَ الْحِسَابِ ﴿٣٨﴾

“Ewe Daud! Hakika Sisi tumekufanya uwe Khalifa ardhini. Basi wahu-kumu watu kwa haki, wala usifuate matamano, yakakupoteza Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika wanaopotea Njia ya Mwenyezi Mungu, wata-pata adhabu kali kwa sababu ya kusahau kwao Siku ya Hisabu.” (38:26)

Ukhalifa baada ya Mtume (saww):

Ama baada ya Mtume (saww) nani Khalifa anayehusika kuwaongoza Waislamu katika mfumo wa Qur’ani na Sunnah? Hapa tunanukuu baadhi ya Aya chache. Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ
وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ﴿٥٥﴾

“Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukui.” (5:55)

Wanatafsiri wamekubaliana kwamba sababu ya kuteremka Aya hii ni Sayyidna Ali (as) ambaye alitoa sadaka pete yake na hali akiwa katika hali ya kurukuu. Kwa hiyo **Walii** wa Waumini baada ya Mtume (saww) ni Sayyidna Ali (as).

يَتَّيِبُهَا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِيَ الْأَمْرِ
مِنْكُمْ ﴿٥٩﴾

“Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenyne mamlaka katika nyinyi....” (4:59)

Aya hii inathibitisha kwamba ni dharura na lazima kuwatii wenyne mamlaka (*Ulil amr*) kama ilivyo wajibu kumtii Mtume (saww) na Mwenyezi Mungu.

Ulil Amr ni nani? Bila shaka ni wale tu walioteuliwa na kuri-dhiwa na Mwenyezi Mungu. Kama inavyosema aya ya 3:34, lazima

watokane na Mtume (saww). Wao ndiyo kizazi cha Mtume (saww) yaani Ahlulbayt (as). Utukufu na daraja ya Ahlul Bayt (as) ni dhahiri ndani ya Qur’ani. Hizi ni baadhi ya Aya:

Wametakaswa wao ni maasumu hawawezi kudhulumu wala kufanya madhambi:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ
تَطْهِيرًا

“Hakika si mengineyo Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea ucha-fu, enyi watu wa nyumba ya Mtume, na kuwatakasa kabisa kabisa.”
(33:33)

Ni wajibu kuwasalia :

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا
صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

“Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu.”
(33:56).

Mtume alipoulizwa namna ya kumsalia alifundisha: “*Allahum-ma swalli alaa Muhammad wa aali Muhammad kamaa swallayta alaa Ibrahiima wa aali Ibrahiima...*” Katika kumsalia Mtume lazima tuwasalie Aali Muhammad ambao ndiyo hawa Maimamu walio-toharishwa wa nyumba yake (s).

Ni wajibu kuwapenda:

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ وَمَن يَقْتَرِفْ
حَسَنَةً نَّزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْنًا إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٢٣﴾

“Sema: kwa haya siwaombi malipo yoyote kwenu isipokuwa mapenzi katika ndugu. Na anayefanya wema tutamzidishia wema. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwingi wa shukrani.” (42:23)

Kupenda ndiyo msingi wa kufuata.

Wamepewa kitabu, hekima na ufalme:

أَمْ تَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ ۗ فَقَدْ
آتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَآتَيْنَاهُم مَّلَكًا
عَظِيمًا ﴿٥٤﴾

“Au wanawahusudu watu kwa alichowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila yake? Basi tumewapa watoto wa Ibrahim Kitabu na hekima na tukawapa ufalme mkubwa.” (4:54)

Wao ndiyo wajuzi wa Qur’ani na sunnah. Kuwatangulia ni kuangamia.

Mtume (saww) katika mambo muhimu ya dini aliyoyatilia mkazo ni suala la uongozi. Ni wazi kwamba ikiwa Mtume (saww) hakuacha kutuongoza katika mambo madogo madogo, basi bila shaka alitungoza katika mambo mazito na muhimu kama haya ya uongozi na

utawala. Hizi ni baadhi ya hadithi zinazotosheleza kwamba Mtume (saww) alimchagua Imam Ali (as) kwa amri ya Mwenyezi Mungu kuwa Khalifa wake. Na baada yake Maimamu kumi na moja wa mwisho akiwa ni Imam Mahdi (a.t.f.).

Hadithi ya Ghadir Khum:

Baada ya Hijjatul Wada' (Hija ya mwisho), Mtume (saww) alipowasili mahala panapoitwa Khum baina ya Makka na Madina, aliwakusanya Masahaba wote na kuwahutubia. Baadaye alimshika Imam Ali (as) na kuinua mkono wake na kusema: “Kwa yeyote yule ambaye mimi ni maula wake basi Ali ni maula wake, ewe Mola mpende ampendaye Ali (as) na uwe adui ya yule amfanyiaye uadui Ali, mbughudhi anayembughudhi, mnusuru anayemnusuru, mdhalilishe anayemdhalilisha, ipitishie haki pale anapopita. Basi yeyote aliyehudhuria na amfikishie (ujumbe huu muhimu) asiyekuwepo...”

Neno **Mawla** lina maana nyingi, lakini hapa kwa kuzingatia hali na mtiririko katika hotuba, Mtume (saww) alikuwa anausia kwamba Ali (as) ndiye Khalifa na wasii wake na kwamba yeye ni bora kwa Waumini kuliko nafsi zao kama alivyokuwa Mtume (saww). Kumuasi Ali ni kumuasi Mtume (saww).

Hadithi ya *Thaqalayn* (vizito viwili):

Pia Mtume (saww) akausia kwamba anaacha vitu viwili vizito (*thaqalayn*) ambavyo ni: Qur'ani na Ahlulbayt (as), na kwamba ikiwa Umma utashikamana na vizito viwili hivyo hautapotea.

Hadithi ya Safina:

Katika hadithi hii Mtume (saww) anapiga mfano wa Ahlulbayt na nafasi yao katika uongozi. Anayewafuata huyo ameongoka na asiye-wafuata ameangamia. Mtume (s) anasema:

“Mfano wa Ahlubayt wangu ni kama vile mfano wa Safina ya Nuhu (as). Anayepanda ndani ya Safina anaokoka na yule asiyepanda anaangamia.”

Hadithi ya Makhalifa Kumi na wawili:

Al-Qanduzi, kutoka kitabu ‘*Faraidus Simtwayn*’ (hadithi ya 562) cha mwanazuoni mashuhuri wa kishafi‘iy, Sheikh Muhammad bin Ibrahim Al-Hamuiniy ananukuu hadithi zifuatazo:

1. Kutoka kwa Sa‘id bin Jubayr kutoka kwa Ibn Abbas, Mtume (saww) alisema: “Hakika Makhalifa wangu na Mawasii wangu na mahujjah (hoja) wa Mwenyezi Mungu juu ya walimwengu baada yangu ni **kumi na wawili**; wa kwanza wao ni Ali (as) na wa mwisho ni mwanangu Mahdi (a.t.f.). Atateremka roho wa Mwenyezi Mungu Isa bin Maryam (as) na atasali nyuma yake, na ardhi hapo itaangaza kwa nuru ya Mola Wake, na utawala wake utaenea Mashariki na Magharibi.”³

Katika kitabu ‘*Mawaddatul Qurbaa*’ cha Sayyid Ali Al-Hamdany ananukuu hadithi zifuatazo:

2. ‘Abayah bin Rabi‘iy kutoka kwa Jabir kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: “Mimi ni Bwana wa Mitume, na Ali ni Bwana wa Mawasii, na hakika Mawasii wangu baada yangu ni **kumi na mbili**, wa kwanza miongoni mwao ni Ali na wa mwisho ni Al-Qaim, Al-Mahdi.”
3. Kutoka kwa Ibn Abbas (r): “Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: ‘Mimi na Ali na Hasan na

³ Qanduzi, S.I., *Yanabi‘ul Mawaddah*, Juz.3, Uk. 295.

Husayn na tisa katika kizazi cha Husayn ni watu tuliotoharishwa, maasumu (watakasifu, wasiotenda dhambi).⁴

4. Kutoka kwa Ali (k.w.), Rasulullah (saww) alisema: “Anayependa kupanda safina ya uokovu, na kushikamana na kiunganishi madhubuti na kupata hifadhi ya kamba ya Mwenyezi Mungu isiyokatika, basi amfuate na kumnusuru Ali (as) na kuwa adui wa adui yake, na awafuate Maimamu waongofu wa kizazi chake. Hakika wao ndiyo Makhalfu wangu na Mawasii wangu na mahujjah (hoja) wa Mwenyezi Mungu juu ya walimwengu baada yangu, na Mabwana wa umma wangu, viongozi wa waliosafika kwenda peponi, kundi lao ndio kundi langu, na kundi langu ndio kundi la Mwenyezi Mungu na kundi la maadui wao ndiyo kundi la Shetani.”⁵

Muhimu kuzingatia:

- Ahlul Bayt ni watu maalumu waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu kuwa Makhalfu na Mawasii wa Mtume (saww) baada yake hadi Kiyama. Hawa ndiyo Maimamu kumi na mbili: Ali, Hasan, Husayn, Ali Zaynulabidin, Muhammad Baqir, Ja’far Sadiq, Musa Kadhim, Ali Ridhwa, Muhammad Jawad, Ali Naqi, Hasan Askariy, Mahdi.
- Maimamu hawa ni maasumu, wametoharishwa na kupewa elimu ya Kitabu na Sunnah. Baada ya Mtume (saww) hakuna aliye bora kama wao. Kuwatangulia ni dhulma kubwa na kuangamia.
- Maimamu hawa ndiyo ‘*urwatul wuuthqaa*’ (**shikio, kiunganishi madhubuti**) na ‘*hablullah*’ (**Kamba ya Mwenyezi Mungu**)

⁴ Rejea iliyotangulia, Uk. 291.

⁵ Rejea iliyotangulia, Uk. 291.

isiyokatika, wao ndiyo **Njia iliyonyooka**, wao ndiyo **safina ya amani na uokovu...**wao ndiyo **nuru ya Mwenyezi Mungu** na **rehema kwa walimwengu.**

- Ni wajibu kwa kila Muislamu kuwapenda, kuwafuata na kuwatii
- Sala ya mja haikubaliki ila kwa kuwasalia pamoja na Mtume (saww)
- Maadui zao ndiyo kundi la Shetani.

IMAM MAHDI (A.T.F.) NI IMAMU WA KUMI NA MBILI

Dalili kutoka katika Qur’ani:

Kudhahari Mahdi katika zama za mwisho, ambaye atasimamisha Serikali moja ya Mwenyezi Mungu ulimwenguni kote, na kuleta ushindi wa Uislamu na haki dhidi ya kila aina ya dini kwa uongozi wake, na kuangamiza kila aina ya mfumo usio na msingi wa haki, ni tukio muhimu katika historia ya binadamu. Tukio kama hili lazima Qur’ani ilizungumzie kwa kuwa ni Kitabu kinachobainisha kila kitu na mwongozo kwa walimwengu. Qur’ani katika Surah Nahl, 16:89, inasema:

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِّنْ أَنْفُسِهِمْ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيدًا عَلَىٰ هَؤُلَاءِ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تَبْيِينًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَنُذْرًا لِلْمُسْلِمِينَ

“Na siku tutakapomwinua katika kila umma akiwashudia kutokana na wao na tukakuleta wewe uwe shahidi juu ya hawa na tumekuteremshia Kitabu hiki kubainisha kila kitu na uongofu na bishara kwa Waislamu.” (16:89)

Kwa hivyo zipo ndani ya Qur’ani Aya zinazoashiria kuja kwa Imam Mahdi. Hapa tutataja baadhi ya Aya hizo:

1. Surah Anbiyaa, 21:105:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا
عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ

“Na hakika tulikwishaandika katika Zaburi baada ya ukumbusho kuwa Ardhi watairithi waja wangu walio wema.”

Aya hii inaashiria utabiri wa Mwenyezi Mungu kwa Mitume wake kwamba ardhi itarithiwa na waja wema na kwamba mapambano baina ya haki na batili yatamalizika kwa ushindi wa haki kutawala ulimwengu mzima.

2. Surah Nur, 24:55:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ
خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۗ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ
بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale ambao wameamini na waka-tenda mema kuwa hakika atawafanya makhalifa katika ardhi, kama alivyowafanya waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini atawaimarishia

dini yao aliyowapendelea na hakika atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi. Na mwenye kuku-furu baada ya hayo, basi hao ndio mafasiki.”

Hii ni ahadi kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu ya kwamba wasimame imara katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa sababu hatima ya msimamo wao ni ushindi na kuwa makhalifa wa Mwenyezi Mungu juu ya Ardhi.

3. Surah Tawbah, 9:32-33 , Surah Swaff, 61:9:

يُرِيدُونَ أَنْ يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى اللَّهُ إِلَّا أَنْ
يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٣٢﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ
رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ
كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

“Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu amekataa isipokuwa kuitimiza nuru Yake, ijapokuwa makafiri wamechukia. Yeye ndiye aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na dini ya haki ili ipate kushinda dini zote, ijapokuwa washirikina wamechukia.”

Said bin Jubayr, mmoja katika ya matabiina mashuhuri, alisema kuhusu tafsiri ya ‘*kushinda dini zote*’ inahusu zama za Mahdi katika kizazi cha Fatima (as). Ulama wa Tafsiri wamekubaliana kwamba Aya hii inaashiria ya kwamba Uislamu ambao ndiyo dini ya haki lazima utashinda dini zote. Mifumo yote iliyobuniwa itapukutika na Uislamu pekee ndio utaongoza dunia yote. Bishara hii bila shaka inamhusu Imam Mahdi ambaye atadhihiri zama za mwisho na kuon-

goza ushindi wa Haki dhidi ya Batili na kusimamisha Serikali ya Mwenyezi Mungu kote duniani.

4. Surah Zukhruf, 43:61:

وَإِنَّهُ لَعِلْمٌ لِلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرْنَ بِهَا وَأَتَّبِعُونَ^ج هَذَا صِرَاطَ^س
 مُسْتَقِيمٍ^س

“Na kwa hakika hiyo ni elimu ya Saa. Basi usiitilie shaka, na ni-fuateni. Hii ndiyo njia iliyonyooka.”

Baadhi ya wafasiri wanasema ‘Yeye’ ni dhamiri inayorejea kwa Nabii Isa (as). Allamah Suyuti katika kitabu chake ‘*Durrul Manthur*’ ananukuu hadithi kutoka kwa Ahmad bin Hanbal, Tabraani, Ibn Mardawayh, na wengine kutoka kwa Ibn Abbas.

Ama Muqatil bin Sulayman na wengine kama Ibn Hajar Haythamy, Shablanji, Safariini, Qanduzi, miongoni mwa ulamaa wakubwa wa Kisunni wanathibitisha Aya hii inamhusu Mahdi (as) ambaye atadhiri zama za mwisho. Baada ya zama zake ndipo zitaanza ishara za Kiyama.

Dalili kutoka katika Sunnah:

Maudhui ya Mahdi imezungumziwa kwa nafasi na umuhimu mkubwa. Zimepokelewa zaidi ya hadithi elfu moja (1000) kutoka kwa Mtume (saww) kwa njia mbalimbali, nyingi zikiwa ni kwa njia za Masunni. Ulamaa wengi wa Kisunni wameandika vitabu mahsusi kuhusu Mahdi.⁶

⁶ Rejea orodha ya vitabu hivyo katika ambatanisho namba 2.

Jumla ya hadithi zilizopokelewa kutoka kwa Mtume (saww) na Maimamu wa Ahlulbayt (as) zinazidi elfu tatu (3000).

Hadithi hizo zinabainisha kwamba:

- Imam Mahdi (as) ni wa tisa katika kizazi cha Imam Husayn ibn Ali (as),
- Baba yake ni Imam Hasan Askari (as),
- Mama yake ni Bibi Nargis Khatun,
- Jina lake ni sawa na lile la Mtume (saww), na miongoni mwa sifa zake ni al-Mahdi, Al-Qaim, Al-Muntadhar...,
- Atokana na kizazi cha Maimamu wa Ahlulbayt (as) mmoja baada ya mwingine,
- Atazaliwa Samarra, na kuishi katika Ghaiba ndefu kama atakavyotaka Mwenyezi Mungu,
- Hatadhihiri mpaka baadhi ya alama zikamilike,
- Atadhihiri wakati Dunia itakuwa imejaa dhulma na atasimamisha haki na usawa kote ulimwenguni,
- Atakapokuja, akiwa ameegemea Kaaba atawaita wafuasi wake 313 na wote watahudhuria,
- Nabii Isa (as) atateremka na kuswali nyuma ya Imam Mahdi (as),
- Imam wa Zama atasimamisha Sheria za Kiislamu kote duniani na dunia itageuka kuwa kama Pepo.

A - IMAM MAHDI KATIKA SAHIH SITA (VITABU SITA SAHIHI VYA HADITHI):

Maadui wa Uislamu katika kila zama wamejitahidi kupambana na Uislamu kwa kupandikiza mafunzo bandia ambayo yamedhoofisha Uislamu kwa kuleta mfarakano ndani ya umma. Itikadi ya Mahdi ni itikadi ambayo inaupa umma huu utukufu na nguvu, na kwa sababu hiyo imekuwa ni shabaha ya makombora ya makafiri.

Imani ya Mahdi (as) ni itikadi ya Kiislamu yenye ushahidi wa Qur’ani na Sunnah. Na kamwe si itikadi ya Kishia kama vile baadhi ya wazushi wanavyodai kwa maslahi yao ya kisiasa. Hizi ni baadhi ya hadithi za Mtume (saww) kutoka katika Vitabu Sita Sahihi:⁷

Kutoka kwa Ummu Salama anasimulia kwamba alimsikia Mtume (saww) akisema: “Mahdi (as) anatokana na kizazi changu kwa kupitia kizazi cha Fatima (as).” Abu Dawud, An-Nasai, Ibnu Maajah, Bayhaqiy (As-Sakhawiy, Uk. 518).

Imam Ali (as) anasimulia kwamba Mtume (saww) alisema: “Lau kama ingebaki katika umri wa dunia ila siku moja, [basi Mwenyezi Mungu angeirefusha siku hiyo ili kumuwezesha] mtu katika watu wa Nyumba yangu (Ahlul Bayt) [ambaye ataitwa kwa jina langu] kuitawala Ardhi na kuijaza uadilifu kama itakavyokuwa imejaa

⁷ *Sahihi Bukhari* (cha Muhammad bin Ismail Al-Bukhariy, 194 H./810 M. – 256 H./870 M. ; mwanahadithi, Hafidh, Faqihi, na mwanahistoria)

- *Sahihi Muslim* (cha Muslim bin Al-Hajjaj Al-Qashiiriy Al-Nisaabuuriy, kaf. 261H./875M. ; mwanahadithi, Hafidh)

- *Sunan at-Tirmidhi* (cha Muhammad bin Isa Al-Tirmidhiy, 209 H./824 M. - 279 H./892 M.; mwanahadithi.)

- *Sunan Abi Dawud* (cha Sulayman bin Al-Ashath As-Sajistaaniy, kaf. 275 H./889 M., imam wa wanahadithi zama zake)

- *Sunan Ibn Maajah* (cha Muhammad bin Yazid Al-Qazwiniy, kaf. 273 H./887 M.; mwanahadithi, Hafidh, Mfasiri, Mwanahistoria)

- *Sunan an-Nisai* (Ahmad bin Ali bin Shuayb, kaf. 303H./915M.; mwanahadithi, Hafidh)

jeuri.” Abu Dawud, Ibn Maajah, Tirmidhy, Ahmad bin Hanbal, Tab-rani, Hakim,..., (As-Sakhawiy, Uk. 522).

Kutoka kwa Abu Hurayra, Mtume (saww) alisema: “Mtakuwaje nyinyi pindi Isa bin Maryam (as) (atakapoteremka) atakapokuwa miongoni mwenu na Imam wenu akiwa baina yenu.” (Bukhari, Muslim.)⁸

Miongoni mwa mambo ambayo ni ya yakini zama za kudhihiri Mahdi ni kuteremka Isa bin Maryam (as) na kuswali nyuma ya Imam Mahdi (as) na kuuwa ‘nguruwe’ na kuvunja ‘msalaba.’ (at-Tha’labiy kuhusu tafsiri ya 43:61). Zipo hadithi nyingi ambazo zinaelezea kila zama za maisha ya Imam Mahdi (as). (Rejea vitabu katika ambatanisho na. 2).

Hizi hadithi chache uchambuzi wake unaonyesha kwamba:

1. Imam Mahdi (as) anatokana na Nyumba ya Mtume (saww), Ahlulbait (as),
2. Imam Mahdi (as) atadhihiri zama za mwisho na kusimami-sha Serikali moja ya Mwenyezi Mungu kote ulimwenguni,
3. Nabii Isa (as) ataswali nyuma ya Imam na kumsaidia.

B - MAIMAMU WA AHLULBAIT (A.S.) NA IMAM MAHDI⁹

Salman al-Farsi alisema: “Nilikwenda kwa Mtume (saww), na kum-kuta Husayn ibn ‘Ali amekaa juu ya paja la Mtume (saww) na huku anambusu macho yake na mdomo wake, na akisema:

“Wewe ni mtukufu, mtoto wa mtukufu, ndugu ya mtukufu; wewe ni Imam, mtoto wa Imam, na ndugu wa Imam. Wewe ni Hujja, mtoto wa Hujja, ndugu wa Hujja, na utakuwa baba wa maHujja tisa na wa tisa ndiye al-Qa’im.”

⁸ Khan, Muhsin: *Sahih al-Bukhari*, Arabic-English, v4, Tradition #658

⁹ Hadithi hizo, rejea *Kashful Gummah*, Kamaaluddin, Imam Mahdi (Qarshi)

Ni muhimu kuelewa kwamba Maimamu wa Ahlul Bayt (a.s.) wote kama warithi wa elimu na sunnah ya Mtume (saww), walieleza habari za Imam Mahdi (a.s.) kwa upana na hadithi nyingi zimepokelewa kutoka kwao. Hizi ni baadhi ya hadithi:

IMAM ALI (AS):

Asbagh bin Nubata alisimulia kwamba Imam Ali (a.s.) alisema: “Katika zama za mwisho, Mahdi ni yule atokanaye nasi...”

Imam Husayn (a.s.) alimnukuu baba yake Imam Ali (a.s.) kwamba aliwahi kumwambia: “Ewe Husayn, wa tisa katika dhuria (kizazi) wako ndiye *al-Qaim Bil Haqq* na yeye ndiye atakayeneza dini na kusimika haki mahala pote.” Baada ya kuomba ufafanuzi zaidi Imam Ali (a.s.) alisema: “Naam! Wallahi! Naapa kwa Yule aliyemtuma Mtukufu Muhammad (saww) na kumchagua juu ya wote, hivyo ndivyo, lakini atakuwa na ghayba ambayo itachanganya na kufadhaisha. Wale tu wenye ikhlasi (niya safi) na yakini na ambao Mwenyezi Mungu amechukua ahadi ya *wilayah* (kutupenda na kutufuata) yetu na kuthibitisha imani ndani ya nyoyo zao, kisha akawabariki na kuwasaidia, ndiyo watakasimama imara na kuendelea kuwa na imani ya al-Qaim.”

IMAM HASAN (AS):

Imam Hasan alipofanya ‘sulhu’ na Muawiya baadhi ya mashia walimlaumu. Naye aliwaambia: “Ole wenu, Wallahi nilichokifanya ni bora kwenu kuliko chochote kile. Je hamjui ya kwamba mimi ni Imam wenu ambaye ni faradhi juu yenu kunitii? Na kwamba mimi ni mmoja wa mabwana wawili wa vijana peponi?” Wote wakajibu: ‘Bila shaka.’ Akaendelea kusema: “Je hamjui ya kwamba Khidhr (a.s.) alipotoboa ile safina na kumuua yule kija-

na, na kusimamisha ule ukuta yalikuwa ni maovu kwa Nabi Musa (a.s.) kwa kuwa upande wa hikma ulikuwa umefichwa kwake. Ama kwa Mwenyezi Mungu ilikuwa ni sawa na hekima. Je hamjui ya kwamba hakuna yeyote miongoni mwetu ila atachukua shingoni mwake bay'ah ya kiongozi dhalimu wa zama zake isipokua mmoja tu, naye ni al-Qaim ambaye Ruhullah Isa bin Maryam (as) atasali nyuma yake. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu ataficha kuzaliwa kwake na atamsitiri katika ghayba ili asiwe na bay a'h shingoni mwake. Atakapotokeza huyo wa tisa katika kizazi cha ndugu yangu Husayn (as), Mwenyezi Mungu atarefusha umri wake katika ghayba kisha atamdhihirisha kwa kudra yake katika sura ya kijana ambaye hajafikia miaka arobaini, hivyo mjue ya kwamba Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu.

IMAM HUSAYN (AS):

Imam Sadiq (sa) kama alivyopokea kutoka kwa babu zake kwamba Imam Husayn (as) alisema: “Katika kizazi changu cha tisa kuna sunnah kutoka kwa Yusuf (as) na sunnah kutoka kwa Musa bin Imran, na yeye ndiye Qaimu wetu Ahlul Bayt (as) ...”

IMAM ALI ZAYNULABIDIN (AS):

“Kwa al-Qaim kutoka kwetu kuna sunnah kutoka kwa Mitume: Sunnah kutoka kwa Nuh (as), sunnah kutoka kwa Ibrahim (as), sunnah ya Musa (as), sunnah ya Isa (as), sunnah ya Ayub (as) na sunnah ya Muhammad (saww)...” Sunna hizo moja baada ya nyingine ni: umri mrefu, kuzaliwa bila watu kujua, hofu na ghayba, watu kuhitilafiana juu yake, faraja baada ya balaa, kutokana na upanga.

IMAM MUHAMMAD BAQIR (AS):

Imam alipoulizwa ni lini atatokeza al-Qaim wenu? Alijibu (a.s.): “Wanaume watakapojifananisha na wanawake, na wanawake kujifananisha na wanaume ... atakapouliwa kijana miongoni mwa kizazi cha Mtume (as) baina ya Rukn na Maqam jina lake Muhammad bin Hasan Nafs Zakiyyah, atakapotokeza Sufyani huko Sham, ...”

IMAM JA’FAR SADIQ (AS):

Imam Ja’far Sadiq (a.s.) alisema: “Al-Khalafu-Salih (Mrithi mwe-ma) atokana na uzao wangu na yeye ndiye Mahdi, ambaye jina lake ni Muhammad na kuniya yake Abul Qasim. Atadhihiri Zama za mwisho. Mama yake atakuwa ni Narjis. Juu ya kichwa chake daima kutakuwa na wingu kumkinga na joto la jua...”

Abu Basir anasimulia: Nilimuuliza Imam Ja’far Sadiq kuhusu nani al-Qaim miongoni mwa Ahlul Bayt (a.s.). Alinjibu: “Ewe Abu Basir, yeye ni wa tano katika kizazi cha mwanangu Musa (as), na huyo ni mtoto wa bibi bora (aliyechukuliwa kama mtumwa), atatoweka katika ghaiba na watashuku wenye kuwa na shaka, kisha Mwenyezi Mungu atamdhihirisha na kumpa ushindi wa kuiteka Magharibi na Mashariki ya ardhi, kisha atateremka Ruhullah Isa bin Maryam (as) na ataswali nyuma yake na hapo ardhi itang’ara na nuru ya Mola Wake, na hakutobaki juu ya ardhi eneo ambamo aliabudiwa asiye Mwenyezi Mungu ila ataabudiwa ndani yake Mwenyezi Mungu, na dini yote itakuwa ni ya Mwenyezi Mungu hata kama watachukia mushrikina.”

IMAM MUSA KADHIM (AS):

Yunus bin ‘Abdurahman anasimulia: “Niliingia kwa Musa bin Ja’far na kumuuliza: Ewe mtoto wa Mtume (saww), hivi wewe ndiye al-

Qaim bil Haqq?” Akajibu: “Mimi ni al-Qaim bil Haqq, lakini Yule al-Qaim ambaye atatoharisha ardhi na kuwafyeka maadui wa Mwenyezi Mungu na kuijaza uadilifu kama vile ilivyokuwa imejaa dhulma, ni wa tano katika uzao wangu. Atakuwa na ghayba ndefu kwa sababu ya kuhofia nafsi yake na (katika kipindi hicho) watu wataritadi na wengine kuthibiti”. Kisha akasema: “Wamebarikiwa wale mashia wetu ambao wameshikamana na kamba yetu katika kipindi cha ghayba ya al-Qaim wetu, wakawa wenye kusimama imara kwenye ufuasi wetu na kujiepusha na maadui wetu. Hao ndiyo wotokanao nasi na sisi twatokana nao, wameturidhia sisi kuwa ndiyo maimamu na sisi tumewaridhia wao kuwa ndiyo wafuasi. Wamebarikiwa kisha wamebarikiwa, na Wallahi wao watakuwa nasi katika daraja yetu Siku ya Kiyama.

IMAM ALI RIDHA (AS):

Imam Ali ibn Musa ar-Ridha (Imam wa nane) alisema: «Imam baada yangu ni mwanangu Muhammad, na baada yake ni mwanawe ‘Ali, na baada ya ‘Ali ni mtoto wake, Hasan, na baada ya Hasan ni mtoto wake Hujjatu’l-Qa’im, ambaye ni msubiriwa wakati wa Ghaiba yake na mtiiwa wakati wa kudhihiri kwake...» ikiwa katika umri wa dunia hii itabakia siku moja, basi Mwenyezi Mungu atairefusha hadi pale atakapodhihiri na kujaza haki duniani kote kama vile ilivyokuwa imejaa dhulma. ... ama Mtume alipoulizwa lini al-Qa’im ambaye atokana na kizazi chako atadhihiri? Mtume (saww) alijibu na kusema: ‘Hali (kadhia) yake ni kama ile ya Siku ya Kiyamah’. Yeye pekee ndiye atakayeidhihirisha kwa wakati wake mwafaka. Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haiji ila nanyi mkiwa hamtambui.

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَلُهَا قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّي
 لَا تَجْلِيهَا لَوْ قَتَبْنَا إِلَّا هُوَ ثَقُلَتْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا
 تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً يَسْأَلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا
 عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

“Wanakuuliza hiyo Saa (ya mwisho) itakuwa lini? Sema: Kuijua kwake kuko kwa Mola Mlezi wangu. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye. Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haikujiini ila kwa ghafla tu. Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kuijua. Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini aghlabu ya watu hawajui.” (7:187)

IMAM MUHAMMAD TAQI (AS):

Saqr ibn Abi Dulaf alisema: “Nilimsikia Abu Ja’far Muhammad ibn Ali ar-Ridha (Imam wa tisa) ambaye alisema: “Imam baada yangu ni mwanangu Ali, amri yake ni amri yangu, Imam baada yake ni mwanawe, Hasan. Amri yake ni amri ya baba yake; kauli yake ndiyo kauli ya baba yake; kumtii yeye ndiyo kumtii baba yake.” Baada ya kusema hayo Imam alinyamaza na hapo nikamuuliza: ‘Ewe mtoto wa Mtume, ni nani atakuwa Imam baada ya Hasan?’ Imam alilia sana na kisha alisema: “Hakika baada ya Hasan ni mwanawe Imam msubiriwa ambaye ndiye al-Qa’im Bi’l-Haqq.”

IMAM ALI NAQIY (AS):

Ibn Abi Dalaf alisema: Nilimsikia Imam Ali ibn Muhammad (imam wa kumi) akisema kwamba: “Imam baada yangu ni mwanangu Hasan, na baada yake ni mtoto wake ndiye al-Qaim, ambaye ataijaza ardhi uadilifu wakati itakapokuwa imejaa dhulma.”

IMAM HASAN ASKARIY (AS):

Musa ibn Ja’far Baghdadi alisema: “Nilimsikia Imam Abu Muhammad al-Hasan ibn Ali (Imam wa kumi na moja) akisema: ‘Naona baada yangu zitazuka tofauti miongoni mwenu kuhusu nani Imam baada yangu. Basi jueni ya kwamba yeyote anayewakubali maimamu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu lakini akamkana mwanangu ni sawa na yule anayewakubali Mitume wote kisha akaukana utume wa Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad (saww). Na yeyote anayemkana Muhammad (saww) ni sawa na yule aliyekana Mitume wote wa Mwenyezi Mungu... basi kwa hiyo kuweni makini, kwani mwanangu atakuwa na kipindi cha ghaiba ambacho watu wote wataanguka ndani ya shaka isipokuwa tu wale ambao Mwenyezi Mungu atawahifadhi.’”

C - UCHAMBUZI WA KITAALAMU WA HADITHI KUHUSU IMAM MAHDI (AS)

1. Ulamaa na maimamu waliotoa hadithi kuhusu Imam Mahdi (as): Ni sahihi kabisa kusema kwamba hakuna mwanahadithi katika maimamu wa hadithi ambaye hakutoa hadithi zinazohusu kudhihiri kwa Imam Mahdi (a.s.) hapo Akhirizaman. Wengi wameandika vitabu mahsusi kumuelezea kwa mapana Imam

Mahdi (a.s.). Hii ni orodha ya baadhi ya ulamaa na maimamu wa hadithi:

Idadi	Jina	Kaf. (H.)
1.	Ibn Sa'd	230
2.	Ibn Abi Shayba	235
3.	Ahmad bin Hambal	241
4.	Al Bukhary	256
5.	Muslim	261
7.	Abu Bakr Al Askaafy	
8.	Ibn Maajah	273
9.	Abu Dawud	275
10.	Ibn Qutaybah Al Daynuury	276
11.	Al Tirmidhy	279
12.	Al Bazaar	292
13.	Abu Ya'laa Al Musuly	307
14.	Al Twabary	310
15.	Al 'Aqiily	322
16.	Na'iim bin Hamaad	328
17.	Al-Barbahaary Shaykh wa Mahambaly zama zake	329
18.	Ibn Hibbaan Al Basty	354
19.	Al Muqaddasy	355
20.	Al Tabraany	360
21.	Abul Hasan Al Aabiry	363
22.	Al Daaraqtuny	385
23.	Al Khatwaaby	388
24.	Al Haakim Al Niisaabury	405
25.	Abu Na'iim Al Iswbahaany	430
26.	Abu 'Amruu Al Daany	444
27.	Al Bayhaqy	458
28.	Al Khatib Al Baghdady	463
29.	Ibn 'Abdul Barr Al Maaliky	463

30.	Al Daylamy	509
31.	Al Baghwy	510
32.	Al Qaadhy ‘Ayaadhw	544
33.	Al Khuwaarazmy al Hanafy	568
34.	Ibn ‘Asaakir	571
35.	Ibn Al Jawzy	597
36.	Ibn Al Athir Al Jazary	606
37.	Ibn Al Araby	638
37.	Muhammad bin Talha Al Shafi‘i	652
38.	Sibt bin Al Jawzy	654
39.	Ibn Abil Hadiid Al Mu‘tazily Al Hanafy	655
40.	Al Mundhary	656
41.	Al Kanjy Al Shafi‘i	658
42.	Al Qurtuby Al Maliky	671
43.	Ibn Khalikkaan	681
44.	Muhibuddin Al Tabary	694
45.	Ibn Mandhuur, Muhammad bin Mukarram ¹⁰	711
46.	Ibnu Al Taymiyyah	728
47.	Al Juwayny Al Shafi ‘i	730
48.	‘Alauddin bin Balbaan’	739
49.	Waliyuddin Al Tabriizy	Baada ya mwaka 741
50.	Al Muziy	739
51.	Al Dhababiy	748
52.	Ibnul Wardiy	749
53.	Al Zarandiy Al Hanafiy	750
54.	Ibnul Qayyim Al Jawziyyah	751
55.	Ibnul Kathir	774
56.	Sa‘duddin Al Taftaazaaniy	793
57.	Nuruddin Al Haythamiy	807
58.	Ibnul Khaldun Al Maghribiy	808

¹⁰ Katika kamusi yake maarufu ‘Lisanul ‘Arab’ chini ya neno: Huda

59.	Muhammad Al-Jazariy Al-Dimashqiy Al-Shaafi 'i	833
60.	Abu Bakr Al Buuswiiriy	840
61.	Ibnul Hajar Al Asqalaaniy	852
62.	Al Sakhaawiy	902
63.	Al Suyyuutwiy	911
64.	Al Sha'raaniy	973
65.	Ibnul Hajar Al Haythamy	974
66.	Al Muttaqiy Al Hindiy	975
67.	Mar'iy Al Hambaliy	1033
68.	Muhammad Rasuul Al Barzanjiy	1103
69.	Al Zarqaany	1122
70.	Muhammad bin Qasim Al Malikiy	1182
71.	Abul 'Alaail 'Iraaqiy Al Maghribiy	1183
72.	As Safaariniy Al Hambaliy	1188
73.	Al Zubaydiy Al Hambaliy ¹¹	1205
74.	Al Swabbaan	1206
75.	Muhammad Amiin Al Suwaydiy	1246
76.	Al Shawqaaniy	1250
77.	Muumin Al Shablanjiy	1291
78.	Ahmad Zayniy Dahlaan Al-Shaafi 'i	1304
79.	Sayyid Muhammad Swiddiiq Al-Qanuujiy Al-Bukhariy	1307
80.	Shihabuddin Al Halwaany Al Shaafi 'i	1308
81.	Abul Barakaat Al Aaluusiy Al Hanafiy	1317
82.	Abu Al Twayyib Muhammad Shamsul Haqqil 'Adhiim Aabaadiy	1329
83.	Al Kattaaniy Al Maalikiy	1345
84.	Al Mubaar Kafuuriy	1353
85.	Mansuur Aliy Naaswif	1371
86.	Muhammad Al Khidhr Husayn Al Miswriy	1377
87.	Abul Faydh Al Ghamaariy Al Shafi 'iy	1380

88.	Muhammad bin ‘Abdil ‘Aziz Al Maani ‘i	1385
89.	Muhammad Fuad ‘Abdul Baaqi	1388
90.	Abul A ‘laa Al Mawduudy	
91.	Naaswiruddin Al Albaaniy, Abdulaziz bin Baaz (maWahhabi)	
	Wengine wengi miongoni mwa wanazuoni wa hivi sasa.	

Ama ulamaa wa Kishia ambao wametoa hadithi za Imam Mahdi (as), idadi yao ni kubwa kwa kuwa itikadi hii ni ya msingi katika Ushia.¹¹

2. Masahaba waliosimulia hadithi za Imam Mahdi (as) kutoka kwa Mtume (saww):

Masahaba waliosimulia hadithi za Imam Mahdi (as) kutoka kwa Mtume (saww) au ambao hadithi zao ni ‘*mauquufa*’ kwao na zenye hukumu ya kupandishwa kwa Mtume (saww) ni wengi sana, na lau ingethibiti kunukuliwa kutoka kwa asilimia 10 yao basi ingethibiti ‘*tawaatur*’ bila shaka.

Idadi	Jina la Sahaba	Kaf. (H.)
1	Fatima Zahraa (as)	11
2	Ma ‘adh bin Jabal	18
3	Qataada bin Al Nu’maan	23
4	Umar bin Al Khattwaab	23
5	Abuu Dhaar Al Ghifaariy	32
6	‘AbdurRahmaan bin ‘Awf	32
7	‘Abdullah bin Mas ‘uud	32
8	‘Abbaas bin ‘Abdul Muttwalib	32
9	Uthmaan bin ‘Affaan	35
10	Salmaan Al Faarisiy	35 / 36
11	Twalha bin ‘Abdullah	36

¹¹ Katika kitabu chake “*Tajul ‘Aruus*” mada ya HADIYA

IMAM MAHDI IMAM WA ZAMA HIZI NA KIONGOZI WA DUNIA

12	Hudhayfa bin AlYamaan	36
13	‘Ammaar bin Yaasir	37
14	Imam ‘Ali bin Abi Twaalib (as)	40
15	Imam Hasan bin ‘Ali (as)	50
16	Tamim Al Daariy	50
17	‘AbdurRahmaan bin Samrah	50
18	Majma ‘ bin Jaariyah	50
19	‘Umraan bin Huswayn	52
20	Abuu Ayyub Al Answariy	52
21	Thuubaan maula wa Mtume (saww)	54
22	‘Aaisha ummul muuminiin	85
23	Abuu Hurayrah	59
24	Imam Husayn bin ‘Ali (as)	61
25	Umm Salama ummul Muuminiin	62
26	‘Alqamah bin Qays bin ‘Abdullah	62
27	‘Abdullah bin ‘Umar	65
28	Abdullah bin ‘Amr bin Al ‘Asw	65
29	‘Abdullah bin ‘Abbaas	68
30	Zayd bin Arqam	68
31	‘Awf bin Maalik	73
32	Abuu Sa ‘id Al Khudhriy	74
33	Jaabir bin Samrah	74
34	Jaabir bin Abdillah Al Ansariy	78
35	‘Abdullah bin Ja’far Al Twayyaar	80
36	Abuul Amaamah Al Baahiliy	81
37	Bishr bin Al Mundhir bin Al Jaruud	83
38	‘Abdullah bin AlHaarith Al Zubaydiy	86
39	Sahl bin Sa ‘id AlSa’idiy	91
40	Anas bin Malik	93
41	Abuu Tufayl	100
42	Umm Habiibah	
43	Abul Juhhaaf	
44	Abu Salamiy mchungaji wa wanyama wa Mtume (saww)	
45	Abuu Laylaa	

46	Abuu Wail	
47	Hudhayfa bin Usayd	
48	Al Harth bin Rabi'i	
49	Abu Qataada AlAnswariy	
50	Zuraarah bin 'Abdullah	

3. Ulamaa waliohukumu kwamba hadithi za Imam Mahdi (as) ni Sahihi:

Hii ni orodha fupi ya wanazuoni waliothibitisha usahihi wa hadithi kuhusu Imam Mahdi (a.s.):

1. Al Imam Tirmidhiy, Muhammad bin Isa (209 H./824 M. - 279 H./892 M.) – Imam na mwanahadithi, alisafiri sana Khorasan, Iraq na Hijaz kutafuta hadithi.

Katika kitabu chake maarufu '*Sunanu Tirmidhiy*'. Alise-
ma kuhusu hadithi tatu za Mahdi (a.s.): "*Hizi ni hadithi
'Hasan' na 'Sahihi'*".

2. Al Haafidh Abu Ja'far Al 'Aqiiliy (kaf. 322 H.). - Baada ya kutaja hadithi dhaifu kuhusu Imam Mahdi (as) akasema: "*Zipo hadithi nzuri tofauti na hii, kuhusu Mahdi*".
3. Al Haakim Al Niisaabuuriy (kaf.405 H.)
4. Al Imam Al Bayhaqiy, Ahmad bin Husayn (kaf. 458 H./1066 M.)
5. Miongoni mwa maimamu wa hadithi. Miongoni mwa mafaqih wakubwa wa Kishafi. Alizaliwa Khusrujard na kukulia Bayhaq na kufia Naysaabuur. Miongoni mwa vitabu vyake ni: *Sunanul Kubra, Sunanus Sughra, Al Mabsuut...*

Alisema: “Na hadithi kuhusu kutokeza kwa Mahdi, sanadi zake ni sahihi Zaidi.”

6. Al Imam Al Baghwy (kaf. 510/516 H.)

Katika kitabu chake ‘*Maswaabiihus Sunnah*’ ametoa hadithi moja katika jumla ya hadithi sahihi, na tano katika jumla ya hadithi ‘hasan’.

7. Ibnul Athiir, Majduddin Abuu Sa‘adaat Al Mubaarak (1149 M. – 606 H./1210 M.) - Faqihi aliyeishi Mosul na kufia hapo. Alikuwa mjuzi wa Qur’an, Hadithi na Nahw. Nyumba yake ilikuwa ni sehemu ya kukutania masufi.

Katika kitabu chake ‘*Al Nihaayah Fii Ghariibil Hadith Wal Athar*’, kuhusu mada ya ‘hada = kuongoka’ aliandika: “Na kuhusu neno hilo ni hadithi isemayo: Sunna ya makhalifa wangu wema walioongozwa. Al Mahdi maana yake: Aliyeongozwa na Mwenyezi Mungu kwenye haki, na limetumiwa katika majina mpaka likashamiri. Na kwa jina hilo ndilo ameiwa yule Mahdi aliyebashiriwa na Mtume (saww) kwamba atadhihiri Akhirizamaan.”

Maneno kama haya kutoka kwa mwanazuoni mkubwa kama huyu ni dalili tosha kwamba anaamini usahihi wa hadithi zilizo-pokelewa kuhusu Imam Mahdi (as).

8. Al Qurtubiy Al Maaliky (kaf. 671H.)

Ni miongoni mwa wenye kuthibitisha kwamba ni ‘*mutawaatir*’. Alisema kuhusu hadithi aliyoitoa Ibnu Maajah kuhusu Mahdi kwamba sanadi yake ni sahihi.

9. Ibnu Taymiyah (kaf. 729 H.), katika ‘*Minhaju as-Sunnah*’ alise-

ma:

“Hakika hadithi anazotolea hoja Allaamah Al Hilli kuhusu kudhihiri kwa Mahdi ni sahihi.”

10. Al Dhahabiy, Muhammad bin Ahmad Shamsuddin (kaf. 748 H./1348 M), Yeye alinyamazia hadithi zote ambazo Al-Haakim aliziainisha kuwa ni sahihi. Hii ni dalili kwamba yeye pia amekubaliana na usahihi wa hadithi hizo.
11. Al Kanji Al Shafi ‘i (kaf. 658 H.) ambaye ndiye mwandishi wa kitabu ‘*Al Bayaan Fii Akhbaar Swahibiz Zamaan*’. Kuhusu hadithi ya Mahdi aliyoitoa Tirmidhiy na kuisahihi anasema: “Hii ni hadithi sahihi”. Pia kuhusu hadithi isemayo: “Mahdi ni kweli na ni katika kizazi cha Fatima”, anasema: “Hii ni hadithi hasan na sahihi”.
12. Ibnul Qayyim al-Jawziyyah (Muhammad bin Abi Bakr al-Zur‘iy) alifariki 751 H/1350 M, Faqihi wa kihanbali, ni miongoni mwa vigogo, aliyezaliwa Dimashki na kufia hapo. Alimfuata Ibnu Taymiyyah na kusambaza fikra zake. Katika kitabu chake “*Almanaarul Muniif Fii Swahiih wa Dhwaif*” baada ya kutaja baadhi ya hadithi za Mahdi Msubiriwa, akasema: “Hadithi hizi zimegawanyika katika makundi manne: sahihi, hasan, gharib na mawdhu‘u”.
13. Ibn Kathir, Imadudin: (1300 M. - 774 H./1373 M.)

Mwanahistoria, mwanahadithi wa Syria.

Katika kitabu ‘*AnNihaayah Fil Fitani Wal Malaahim*’, ameanadika: ‘Mlango kuhusu Mahdi ambaye atakuja Akhirizamaan: ‘Na yeye ni miongoni mwa makhalifa walioongozwa... na hadithi zimepokelewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kwamba lazima ata-

dhihiri.’ Kuhusu sanad ya hadithi ya Mahdi: “Hii ni sanad yenye nguvu, sahihi”. Kisha akanukuu hadithi kutoka kwa Ibnu Maajah na kusema: “Hadithi hii ni hasan na imesimuliwa na wengi kutoka kwa Mtume (saww)”.

14. At Taftaazaany, Mas ‘uud bin Umar Sa‘duddin (1312 M. - 793 H./1389 M.) - Mmoja katika maimamu wa kiarabu. Alizaliwa Taftazaan (Khorasaan) na kufia Samarqand. Ni hoja katika Bal-gha na mantiki, theiolojia, fiqh na elimu zingine.

Katika kitabu ‘*Sharhul Maqaaswid*’ ameanika: “Miongoni mwa yale yanayoongezwa kwenye mlango wa uimamu ni kule kudhihiri Mahdi na kuteremka Isa (as). Hawa wawili ni katika alama za Kiyama. Na katika mlango huu zimepokelewa *hadithi sahihi* pamoja ya kwamba ni ahad”.

15. Nuruddin Al Haythamiy (kaf.807 H.)

Alitoa baadhi ya hadithi na kukiri kwamba ni sahihi na wapokezi wake ni ‘wenye kutegemewa’.

16. Suyuti, Jalaluddin ‘Abdur Rahman bin Abi Bakr: (851 H./1445 M. - 911 H./1505 M.) Mwanazuoni aliyeshiriki katika aina mbalimbali za elimu. Alizaliwa Cairo na kufariki hapo. Mwandishi mahiri aliyeanika zaidi ya vitabu mia tano katika hadithi, fiqhi, lugha, tafsiri....

Katika ‘*Al Jaami‘u al Swaghiir*’ baadhi ya hadithi kuhusu Mahdi amezitia alama ya sahihi na zingine hasan. Anamnukuu As-Sahriy kwamba alisema hadithi za Mahdi ni mutawatir na nyingi kutoka kwa Mtume (saww).

17. As Shawkaany, Muhammad bin Ali

Alifariki 1250 H/ 1834 M, Faqihi mujtahid aliyekulia Sanaa, Yemen na kuwa Kadhi wa hapo. Aliandika zaidi ya vitabu mia moja. Anathibitisha kwamba hadithi za Mahdi ni ‘Mutawatir’. Alisema: “Ama hadithi tulizoweza kuzitazama, hamsini miongoni mwazo zimo ambazo ni Sahihi, Hasan, na Dhaifu. Bila shaka ni ‘Mutawatir’.” Al Qanuujy amenukuu kutoka kwake kauli ya kwamba hadithi za Mahdi ni sahihi bali ni Mutawaatir.

18. Muhammad Naasiruddin Al Baaniy (karne ya ishirini)

Katika makala yake yenye anuani ‘*haulal Mahdi*’ (kuhusu Mahdi) iliyotolewa ndani ya jarida ‘*at-Tamaddunul Islaamy*’ alisema: “Ama kuhusu Mahdi, ifahamike kwamba kuna hadithi nyingi sahihi kuhusu kutokeza kwake. Sehemu kubwa ya hadithi hizo zina sanadi sahihi.”

“Muhtasari wa maneno ni kwamba, itikadi ya kutokeza Mahdi ni itikadi thabiti tena mutawatir kutoka kwake Mtume Mtukufu (saww) na ni wajibu kuiamini kwa kuwa ni katika mambo ya ghaybu, na kuyaamini ni katika sifa za wachamungu kama alivyosema Mwenyezi Mungu: (2:1-2)

Kwa hiyo hakanushi itikadi hiyo ila jahili au mbishi. Namuomba Mwenyezi Mungu atufishe kwenye imani ya hilo na kwenye kila lililothibiti katika Kitabu na Sunnah”

19. Al Manaawy, ‘Abdur Rauuf, (alifariki 1031 H/1621 M.)

Imam wa Kishafii iliyeishi na kufariki Cairo. Kaandika kitabu ‘*Faydhwul Qadir*’.

Alisema: “Habari za Mahdi ni nyingi na mashuhuri kiasi kwamba wameziandika waandishi wengi”.

20. As Samhuudy, Ali Nuruddin, (alifariki 911 H./1506 M.)

Imam wa Kishafii, alizaliwa Misri na kufariki Madina.

Alisema: “Imethibiti katika hadithi kwamba Mahdi ni katika kizazi cha Fatima”

21. Aaluusy, Khayruddin

Aaluusy, ni familia ya kiiraki iliyotoa wanazuoni wakubwa, babu yao akiwa ni Mahmud bin Abdullah (1802-1854 M).

Katika ‘*Ghaliyatul Mawaa’idh*’ alisema: “Katika alama za Kiyama ni kutokeza Mahdi, kauli ambayo ni sahihi kwa ulamaa wengi. Na kuna hadithi nyingi katika kuja kwa Mahdi”. Baada ya kuonyesha baadhi ya hadithi kuhusu Mahdi, alisema: “Haya tulioyataja kuhusu Mahdi ni sahihi miongoni mwa kauli ya Ahlu Sunnah wal Jamaa”.

22. Muhammad Khidhri Husayn, *Shaykhul Azhar*;

Alisema katika makala yake ‘*Mtazamo Katika Hadithi za Mahdi*’ kwamba: “Katika vitabu vya hadithi, hadithi za Mahdi wamezirawi wanahadithi kama vile Imam Ahmad bin Hambal, Abuu Dawud, Tirmidhy, Ibn Maajah, Twabrany, Abuu Na‘im, Ibn Aby Shaybah, Abuu Ya‘la, Daraqtuny, Bayhaqy, Na‘im bin Hammaad na wengine...” pia akasema: “Hadithi hizi zimekusanywa katika vitabu maalum kama vile:

العرف الوردى في حقيقة المهدي

cha Mullah Ali al Qaary na

التوضيح في تواتر ما جاء في المنتظر و الدجال و المسيح

cha asShawkaany”.

22 - Al Adawy, Ali As-Swa‘idy), (Kaf. 1189 H/1775 M.)

Faqihi wa Kimaliki alizaliwa Misri na kufariki Cairo. Alikuwa Shaykh wa mashaykh wakati wa zama zake na mmoja katika vigogo wa al Azhar

Katika kitabu chake ‘*Mashaariqul Anwaar*’ anasema: “Imepokelewa kwamba atakapodhihiri, malaika atanadi juu yake: huyu ndiye Mahdi, Khalifa wa Mwenyezi Mungu, basi mfuateni ...”

23 – Ath Tha’labiy, Abu Ishaq Ahmad bin Muhammad Al Nisaburi (Kaf. 428/1035)

Mfasiri wa Qur’ani. Alikuwa kigogo wa zama zake katika Elimu ya Tafsiri.

Katika tafsiri ya kisa cha Ahlul Kahf anasema: “Wakalala na wataendelea kulala hadi Zama za mwisho, atakapodhihiri Imam Mahdi (as). Atawatolea salaam na Mwenyezi Mungu atawahuisa. Kisha Mwenyezi Mungu atawarudisha katika usingizi wao. Ha-wataamka hadi Siku ya Kiyama.”

4. Ulamaa waliothibitisha kwamba hadithi kuhusu Mahdi (as) ni Mutawaatir

1. Barbahaariy (kaf. 329 H.) sheikh wa Mahambali na mkubwa wao wakati wa zama zake.
2. Muhammad bin Husayn Al Aabiriy Al Shafi'i (kaf. 363 H.)
3. Al Qurtubiy Al Maalikiy (kaf. 716 H.)
4. Jamaaluddin Al Muziyy (kaf. 742 H.)
5. Ibnul Qayyim Al-Jawziyyah, Muhammad bin Abi Bakr Al-Zur'i (kaf. 751 H./1350 M.)
6. Ibn Hajar Al-Asqalaniy (kaf. 852 H)
7. Shamsuddin Al-Sakhaawiy (kaf. 902 H.)
8. Al Suyuutwiyy (kaf. 911 H.)
9. Ibn Hajar Al-Haythamiy (kaf. 974 H./1567 M.)
10. Al-Muttaqi Al-Hindiy (kaf. 975 H.) katika kitabu chake *Al Burhaan Fii 'Alamaat Mahdi Akhirizzamaan* (dalili kuhusu alama za Mahdi wa Akhirizaman) anatetea na kuthibitisha kwa hoja na dalili imani ya Mahdi. La muhimu katika kitabu hicho ni fatwa nne za ulamaa kuhusu anayekanusha kudhihiri kwa Mahdi. Ulamaa hao ni: Shaykh Ibn Hajar Haythamiy Al-Shafi'i, Shaykh Muhammad bin Muhammad Al Khatwaabiy Al-Maalikiy, Shaykh Yahya bin Muhammad Al-Hambaliy na Shaykh Ahmad Abu As-Suruur bin Al Swabaa Al Hanafiy.

Hawa ndiyo waliokuwa ulamaa wa watu wa Makka na mafaqih wa Waislamu kwa madhehebu nne. Wote waliwafikiana kwamba hadithi za Mahdi ni Mutawaatir na kwamba mwenye kuzikanusha lazima aadabishwe hata arejee kwenye haki na akikataa auliwe.

11. Muhammad Rasuul Al Barzanjiy (kaf.1103 H.), anasema: “Hadithi kuhusu kuwepo Mahdi na kudhihiri Akhirizamani na kwamba anatokana na kizazi cha Mtume (saww) kwa kupitia Fatima (a.s.) zimefikia daraja ya Mutawaatir. Hakuna sababu ya kuzikanusha.” Pia akasema:

“Fahamu ya kwamba hadithi zilizopokelewa kuhusu Mahdi ni nyingi sana. Muhammad bin Hasan Ad-Dastuury alisema ndani ya kitabu chake ‘*Manaqibu As Shafiy*’: Hadithi kutoka kwa Mtume kuhusu Mahdi ni mutawatir. Mahdi ni miongoni mwa Ahlul Bayt. Naye Shaykh (Muhyiddin ‘Arabiy) katika ‘*Al Futuhaat*’ alisema kwamba Mahdi ni maasumu (ametakasika, hawezi kutenda dhambi) katika hukumu yake akifuata nyayo za Mtume (saww), kamwe hawezi kukosea.

12. Muhammad bin Qaasim bin Muhammad Jasuus (kaf. 1182 H.)
13. Abul ‘Alaail ‘Iraaqiy Al Faasiy (kaf. 1183 H.)
14. Safaariiniy Al Hambaliy (kaf. 1188 H.)
15. Muhammad bin Ali Al Swabbaan (kaf. 1206 H.)
16. Al Shawkaaniy (kaf. 1250 H.), katika kitabu chake mahsusi ‘*Al Tawdhiihu fii Tawaaturi Maa Jaaa Fil Muntadhar Wad Dajjaal Wal Masiih* = kuweka wazi kuhusu hadithi mutawaatir za Mahdi Anaengojewa na Dajjaal na Masihi’.

17. Mu'min bin Hasan Al Shablanjiy (kaf. 1291 H.)
18. Sayyid Ahmad Zainiy Dahlaan (kaf. 1304 H.), Mufti wa kishafi wa Makkah.

Anasema: “Mtazamo wa hadithi na maelezo ya Ulamaa, Mahdi msubiriwa bado hajadhihiri... yeye atokana na kizazi cha Fatima na bila shaka atadhihiri” pia akasema: “Hadithi kuhusu Imam Mahdi ni nyingi na mutawaatir. Zipo ambazo ni sahihi, zingine ni hasan, na nyingi ni dhaifu. Lakini kwa uwingi wake, na uwingi wa wasimulizi na wapokezi, zinatiana nguvu.” (*Simtwi Nujuumil 'Awaalii*, 4/138)
19. Sayyid Muhammad Al Qanuujiy
20. Sayyid Al-Kattaani, Muhammad bin Ja'far bin Idris Al-Maaliqiy, (1858-1927) - Katika kitabu chake '*Nadhmul Mutanathir Minal Hadithil Mutawaatir*' anamnukuu Shaykh Ahmad As Safaariiniy al Hambaly aliyesema kwamba zimepokelewa hadithi za Mahdi kutoka kwa masahaba wengi na Tabiina baada yao kiasi ya kutosheleza yakini. Imani ya kutokeza Mahdi ni wajibu, kama walivyothibitisha wanazuoni na kuandikwa katika (vitabu) vya itikadi vya Ahl Sunnah wal Jama'a.

Fatwa Muhimu:

Hii ni fatwa iliyotolewa na Rabitatul `Alamul Islami (Muslim World League), tarehe 11. Oct.1976 (23 Shawwal 1396).

Fatwa hii inaelezea kwamba zaidi ya masahaba ishirini wamepokea hadithi za Mahdi. Pia imetoa orodha ya ulamaa wa hadithi waliosimulia hadithi hizo na pia wale walioandika vitabu kuhusu Mahdi. Fatwa inasema:

“Huffadh na ulamaa wa hadithi wamehakikisha kwamba kuna hadithi ‘sahih’ na ‘hasan’ miongoni mwa hadithi za Mahdi. Aghlabu ya hadithi hizo zimesimuliwa na wapokezi wengi (Mutawatir). Kwa hiyo hakuna shaka kwamba hadhi ya hadithi hizo ni Sahihi na Mutawatir.

Pia wamechunguza na kuthibitisha kwamba imani ya Mahdi ni wajibu na ni moja ya itikadi za Ahl al-Sunnah wal Jama’a. Ni wale tu wajinga wa sunnah na wazushi ndio wanakanusha itikadi hiyo.”

Rejea kitabu ‘*Al-Bayan*’ cha Al-Ganji Al-Shafi’i, Beirut, 1399/1979, utangulizi, Uk. 76-79

DALILI ZA KIHISTORIA

A - BAADHI YA WATU WALIODAI UMAHDI NA WALIOSINGIZIWA UMAHDI

Hadithi kama zilivyothibitisha ni dhahiri kwamba Mtume (saww) alielezea kwa upana na urefu habari za kuja Mahdi (a.t.f.). Historia inaonyesha kwamba imani hii muhimu kuhusu kuja kwa Mahdi imekuwa hai katika kila zama na kwamba baadhi ya wanamapinduzi wa Kiislamu waliitumia ili kufikia malengo yao ya kisiasa. Katika mlango huu tunazungumzia matokeo ya itikadi hii kwa kugusia baadhi ya watu waliosingiziwa umahdi na wengine waliodai umahdi.

Waliodai walikuwa na sababu:

- **Niya njema:** Kupata wafuasi wa kuwaunga mkono ili kufikia lengo lao la kurekebisha hali ya umma.

- **Niya mbaya:** Kutaka madaraka, kutaka kuharibu Uislamu.

Wengine hawakudai, bali wafuasi wao walidai hivyo.

⇒ 1 - WALIODAI UMAHDI

Waliodai umahdi hadi hivi sasa ni wengi zaidi ya 150 na wote Mwenyezi Mungu amewafedhehi na kuonyesha uongo wao.¹² Suala hili la umahdi ni vigumu kudanganya mbele ya wanaojua Uislamu kwa sababu zipo hadithi sahihi kutoka kwa Mtume (saww) na Ahlul Bayt (as) zinazoelezea kila kitu kuhusu sifa za Imam Mahdi (as) na alama za kudhiri kwake. Wanapotezwa tu wale wajinga wasio na msimamizi.

Wafuatao ni baadhi ya wale tulioweza kupata historia yao:

1. **Sālih ibn Tarīf**,¹³

Mtawala wa pili wa Barghawātah (Morocco). Zama za ukhalifa wa Hisham bin Abdil Malik, mwaka 748–749 M, alijitangaza kuwa mtume anayepata wahyi. Watu wake walimuita ‘Salihul Mu’minin’ na Mahdi wa mwisho. Alizusha mafunzo tofauti na Uislamu kama vile: kumuua mwizi, kuoia bila idadi, talaka bila idadi, kufunga mwezi wa Rajab na siyo Ramadhan, swala kumi na siyo tano...

2. Ubaydullah al Mahdi. (kaz. 261 H./873 M. - kaf. 322 H./934 M.) Khalifa wa kwanza wa Kifatimiyyah. Alifanikiwa kuanzisha ukhalifa mpya dhidi ya ule wa Kiabbasi mwaka 297 H./909 M. Alitawala hadi mwaka 322 H./934 M.
3. Muhammad bin Abdallah bin Tumart¹⁴ (alifariki mwaka 1130 M.). Muasisi wa dola ya *al-Muwahhidūn* (**Wanaumoja**) maarufu

¹² Dastaghaib, *Al-Mahdi al-Mau'ud*, uk. 46

¹³ Wikipedia, the free encyclopedia

¹⁴ “**Almohads.**” *Encyclopædia Britannica*. Ultimate Reference Suite. Chicago: *Encyclopædia Britannica*, 2008.

kalmohads) Dola ya Kiislamu Afrika ya Kaskazini (1130–1269 M.). Ibn Tūmart alisisitiza sana kuhusu Tawhid na kujitakasa kitabia. Mwaka 1121 Ibn Tūmart, alitangaza kwamba yeye ndiye Mahdi aliyebashiriwa. Pia alidai kwamba yeye ni Maasum (asiyefanya dhambi). Kama kiongozi wa kiroho na kijeshi alianzisha vita dhidi ya Al Murabitun (*Almoravids*). Alifariki mwaka 1130 na mfuasi wake Abd al-Mu'min, alidai cheo cha Khalifa na kudai uongozi wa umma katika Uislamu.

4. Mahdi Tahama

Mahdi Tahama alizaliwa Yemen takriban mwaka 1159 M. Alijitokeza naye akadai kwamba ndiye Imam Msubiriwa aliyetabiriwa na Mtukufu Mtume (saww). Kundi la mabedui walimfuata. Alifanikiwa kuziteka falme za Hamadani huko Sanaa na Najjahi huko Zubaid. Mjukuu wake Abdul Nabi aliendeleza utawala wake lakini alishindwa na Turan Shah na kukomesha utawala wake kwa niaba ya Salahuddin Ayyubi.

5. Sayyid Muhammad ibn Falāh¹⁵ (1400 – 1461)

Alizaliwa mwaka (1400 M.) huko Wāsīt, Iraq na kufariki mwaka (1461M.), huko Hoveyzeh, Iran. Mwanatheolojia wa Kiislamu aliyeanzisha kundi la Mushasha katika Ushia. Sayyid Muhammad ibn Falāh anatokana na kizazi cha Imam wa saba, Mūsā al-Kādhim. Kwa sababu ya fikra zake zilizo kinyume, Shaykh wake alimkana. Katika mwaka wa 1436 alifanikiwa kusambaza fikra zake baina ya makabila ya kiarabu mpakani mwa Iraq na Iran. Alidai kwamba ni Mahdi na kufanikiwa kuteka mji wa Hoveyzeh mnamo mwaka wa 1441, ambao uligeuka kuwa makao makuu ya harakati za Mushasha.

¹⁵ “**Muhammad ibn Falāh.**” *Encyclopædia Britannica. Ultimate Reference Suite*. Chicago: Encyclopædia Britannica, 2008.

6. Sayyid Muhammad Jaunpuri (1443 – 1505)

Alizaliwa India, Jaunpur (jimbo la Uttar Pradesh). Baba yake aliitwa Sayyid Abdullah na mama yake Amina. Alitokana na kizazi cha Imam wa saba, Imam Musa Kadhim (as).

Alidai kuwa ni Mahdi. Alitangaza madai yake kwanza akiwa Makka na tena baadaye akiwa India. Alipingwa na Ulamaa. Alifariki akiwa na miaka 63, Farah, afghanistan. Wafuasi wake wainaitwa Mahdawi, wengi wao wakiwa katika mji wa Hayderabad. Wengi wamehamia sasa Marekani.

7. Muhammad Ahmad (Mahdi wa Sudani, 1848 - 1885)

Alizaliwa katika kijiji cha Dolga, Sudani mwaka 1848. Zama hizo Sudan ilikuwa chini ya himaya ya Misri na Uingereza. Baada ya kumaliza elimu yake ya msingi alijiunga na tarika ya Kisufi ya Kisanusiya na kuanza mazoezi ya kiroho.

Kwa kudhihirisha uchamungu sana aliweza kupata heshima na utukufu akiwa tu na umri wa miaka 22. Alikuwa ni mzungumzaji hodari mwenye ufasaha aliyeweza kuzungumza dhidi ya utawala wa kimisri ukisaidiwa na waingereza. Alifanikiwa kuwahamasisha wasudani kupambana na utawala wa kimisri na Waingereza. Taratibu alidai kuhusiana na Mahdi (as) na mwishowe kudai kwamba yeye ndiye Mahdi (as) katika kizazi cha Mtume (saww), Imamu wa 12 mtoto wa Hasan Askari (as).

Mapambano yake dhidi ya Waingereza na Misri na kuitawala Sudan:

Mnamo Mei 1881, serikali ya Misri ilimtaka kwenda Khartoum na kubainisha msimamo wake. Alikaidi amri hiyo na kutangaza jihad. Mnamo Agosti 11, Rauf Pasha alitumwa na serikali ya Misri akiwa na jeshi la askari mia mbili kupambana na wafuasi wa Muhammad

Ahmad. Wafuasi wake walijificha na usiku wakazingira jeshi la Misri na kulifyeka.

Mnamo Mei 1882, serikali ya Misri ilituma jeshi la askari 6000 kumshambulia Muhammad Ahmad. Katika usiku mmoja, Muhammad Ahmad alishambulia jeshi la Yusuf Pasha na kuwaangamiza.

Mnamo mwisho wa Novemba 1882, Muhammad Ahmad, alishambulia ngome ya Misri ya Al-Abiid na kuiteka na kuifanya kuwa makao ya utawala wake. Mafanikio ya Muhammad Ahmad yalisababishwa na makabila mbalimbali ambayo yalimuunga mkono kwa kuchoshwa na utawala wa dhulma na uonevu wa Misri na Uingereza.

Alijifanya kusimamisha sheria za Qur'ani ili kuwavuta watu. Alikusanya Zaka na Khums ili kuendesha serikali. Alitilia mkazo watu kusoma Qur'ani lakini akazuia watu kuielewa na kuifahamu.

Mnamo Novemba 3, Muhammad Ahmad, alipambana na jeshi la watu 10,000 chini ya William hapo Kashgil na kuwapa kipigo kikali. Sudan yote ilikuwa sasa inaelekea kuwa chini ya utawala wake. Mnamo Desemba 1884, jeshi la Salahuddin Pasha baada ya mapambano ya takriban mwaka mmoja lilishindwa. Baada ya kushindwa, Waingereza walijiandaa kukimbia Sudan. Generali Charles George Gordon aliyewahi kuwa gavana mkuu wa Sudan alitumwa kurahisisha hilo. Aliwasili Khartoum tarehe 18 Februari 1884 na kuwa tayari kukubali utawala wa Muhammad Ahmad ikiwa atawaachia huru wafungwa wote. Na pia alitoa ofa ya kuruhusu tena biashara ya utumwa.

Muhammad Ahmad akatupilia mbali masharti hayo na akaamua kuvamia mji wa Khartoum na mnamo tarehe 22 Agosti akauzingira mji. Mnamo tarehe 25 Januari 1885 Muhammad Ahmad akafanikiwa kuingia ndani ya Khartoum na General Gor-

don akauliwa nje ya kasri yake. Sudan yote ikawa chini ya mam-laka ya Muhammad Ahmad na Khartoum kuwa makao makuu ya ukhalifa wake. Mahdi wa Sudan alifariki tarehe 22 Juni 1885 kwa sababu ya homa kali.

8. Mahdi wa Senegal

Mwaka 1828 M. alijitokeza mtu huko Senegal na kudai kuwa yeye ndiye Mahdi Msubiriwa. Alisimamisha uasi dhidi ya serikali lakini alishindwa na kuuliwa.

9. Mahdi wa Suus

Suus ni mji wa Morocco. Alijitokeza mtu na kudai kwamba yeye ndiye Imam anayengojewa. Watu wengi walianza kumfuata lakini alipigwa risasi na kuuliwa.

10. Muhammad bin Abdullah Hasan (Mahdi wa Somalia 1864-1920)

Sheikh wa kisomali mfuasi wa Tarika ya Salihyyah. Mwaka 1899 alidai kuwa naye ni Imam Mahdi anayengojewa. Alipigana na majeshi ya Kiingereza na kitaliani kwa takriban miaka 20. Alifariki mwaka 1920.

11. Bahāu Allāh (Mirza Husayn ‘Alī Nūrī, 1817 - 1892)¹⁶

Mwasisi wa imani ya Kibahai, alizaliwa mwaka 1817, Tehran, Iran na kufariki 1892, Acre, Palestine (Akko, Israel).

Mirza Husayn alikuwa mfuasi wa madhehebu ya Sha. Alijiunga na Mirza Ali Muhammad wa Shīrāz, kiongozi wa Mababi, aliyejiita kuwa ni Bab (mlango). Baada ya Bab kuuliwa na serikali ya Iran

¹⁶ “**Bahāu Allāh.**” *Encyclopædia Britannica. Ultimate Reference Suite*. Chicago: Encyclopædia Britannica, 2008.

(1850), Mirza Husayn aliungana na Mirza Yahya (mrithi wa Bab) kuongoza Mababi. Akiwa uhamishoni Istanbul, alitangaza mwaka 1867, kwamba yeye ni mteule Imam Mahdi aliyebashiriwa na Bab. Bahāu Allāh, aliachana na Uislamu na kutangaza dini mpya yenye taratibu zake maalumu (Ubahai).

12. Mirza Ghulam Ahmad, (1839 – 1908)¹⁷

Alizaliwa mwaka 1839, huko Qādiān, India na kufariki mwaka 1908, India. Alidai kusikia sauti na mwaka 1889 alitangaza kupata wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Baadaye alikusanya kundi la wafuasi na kuanza mahubiri yake.

Ghulam Ahmad alidai kuwa ndiye Mahdi aliyeahidiwa bali pia yeye ni Yesu (Isa) na Krishna. Wafuasi wake wanaitwa Maahmadiyya au Makadiyani

13. Juhayman bin Muhammad bin Sayf al-Utaybi

Alikuwa kapteni wa zamani wa jeshi la Saudi White Guards (walinzi wa taifa). Novemba 1979, aliongoza kundi la watu 1300 hadi 1500 na kuteka msikiti mtakatifu wa Makka. Alijitangaza kuwa ni Mahdi na mwokozi wa Uislamu. Baada ya wiki mbili za kuzingirwa na majeshi mahsusi ya kisaudi, majeshi kutoka nje – Ufaransa na Pakistan - yaliletwa kumaliza mapambano.

⇒ 2 - WATU WALIODHANIWA UMAHDI:

1. Muhammad bin Hanafiyya (637 M. - 700 M.):

Mtoto wa Imam Ali (as) kwa mkewe Khawlah. Baadhi ya mashia waliojulikana baadaye kama Makaysani (Kaysaniyya, Mukhtariyya)

¹⁷ “**Mirza Ghulam Ahmad,**” *Encyclopædia Britannica. Ultimate Reference Suite*. Chicago: Encyclopædia Britannica, 2008.

waliamini kwamba yeye ndiye imam baada ya ndugu yake Imam Husayn (as) kuuliwa hapo Karbala mwaka 61 H. Waliamini pia kwamba yeye ni Mahdi na kwamba yuko hai anaishi haonekani katika mlima Radhwa. Atakuja kudhihiri na kuondosha dhulma.

2. Muhammad bin ‘Abdullah bin Hasan (An Nafsu az Zakiyya 93 H./712 M. – 145 H./762 M.):

Huyu ni mjukuu wa Imam Hasan (as). Pamoja na ndugu yake Ibrahim waliasi utawala wa khalifa wa Kiabbasi Mansur na kufanya mapinduzi hapo Madina. Aliungwa mkono na wajukuu wa masahaba, matabiina, wachamungu, mafaqihi na maimamu... Aliuliwa katika mapambano maarufu kama ‘vita vya Fakh’. Mmoja katika maimamu wa Kizaidiy (Zaidiyya). Majarudi, kundi miongoni mwa Mazaidiy waliamini kwamba Muhammad bin ‘Abdullah bin Hasan ndiye Mahdi na kwamba alikuwa katika Ghayba. Walikuwa wakisuburi kurejea kwake.

3. Imam Muhammad Baqir:

Mabaqiriy, walimuona Imam Baqir kuwa ni Mahdi na yeye yuko hai.

4. Imam Ja’far Sadiq:

Manawusi waliamini kwamba yeye Imam Ja’far Sadiq ndiye Mahdi na anaishi katika ghayba.

5. Imam Musa bin Ja’far:

Mawaqifiy waliamini kwamba Imam Musa bin Ja’far hakufariki bali yuko hai katika ghayba atakuja kudhihiri baadaye na kueneza uadili-fu na haki kote duniani.

6. Ismail bin Imam Ja'far Sadiq:

Kundi miongoni mwa Maismailia wanaamini kwamba Ismail bin Imam Ja'far Sadiq hakufariki. Kule kutangaza kifo chake ilikuwa tu ni mbinu ya kuepuka mateso na dhulma ya watawala. Kwa hivyo aliingia ndani ya ghayba na atarejea Zama za mwisho kama Mahdi.

7. Muhammad bin Ismail:

Kundi la Mubaraki, miongoni mwa Maismailia walimtizama Muhammad bin Ismail kuwa ni imam hai katika ghayba. Nao Maqaramitwa (tawi la Ismailia lililoasi uongozi wa kiismaili mwaka 899H.) waliamini kwamba Muhammad bin Ismail ndiye Mahdi yuko hai na anaishi huko Anatolia.

8. Muhammad bin 'Ubaydullah bin Muhammad bin Ismail (Al Qaim bi Amrillah, alitawala 934 – 946):

Maismailia wanasema kwamba Mahdi aliyetabiriwa ni huyu Muhammad bin 'Ubaydullah aliyetawala Misri.

9. Muhammad bin Imam Ali Naqi:

Baada ya kufariki Imam Ali Naqi (as), baadhi ya watu waliamini kwamba mwanaye Muhammad ndiye Imam. Pamoja na kufariki zama baba yake yu hai, waliamini kwamba yuko hai na yeye ndiye Mahdi. Hao ndiyo akina Muhammadiy.

10. Imam Hasan Askariy:

Kundi katika mashia waliamini kwamba Imam Hasan Askariy yuko hai anaishi katika ghaiba na atadhihiri baadaye kusimamisha uadilifu na haki. Kundi lingine wanaamini alikufa, lakini atarejea hai na kusimamisha haki.

11. Mtoto wa Imam Mahdi:

Majawaziyya wanaamini kwamba Imam Mahdi alikuwa na mtoto na huyo ndiye Mahdi.

12. Umar bin ‘Abdulaziz bin Marwan, (alizaliwa 682 H., na alitawala 717 – 720):

Khalifa wa Kiumayyah ambaye alikuwa tofauti na watawala wa Kiumayyah. Alikuwa mchamungu na mwadilifu katika utawala wake. Yeye ndiye aliyepiga kifua na kukataza kulaaniwa Sayyidna Ali (a.s.), laana iliyowekwa na Muawiya na kufuatwa na watawala wa Bani Umayyah baada yake.¹⁸ Uadilifu wake uliwafanya baadhi ya watu kufikiria kwamba yeye ndiye Mahdi. Utawala huu wa uadilifu haukudumu kwani waovu wa Bani Umayyah kamwe hawakustahamia uadilifu wake. Aliwadhibiti na kuwanyang’anya mali walizopora. Walimpa sumu na kumuua. Alifariki mwaka wa 101 H. akiwa na umri wa miaka 39.¹⁹

13. Usman Dan Fodio²⁰ (alizaliwa 1754, Maratta, Gobir, Hausaland, na kufariki 1817, Sokoto, Mamlaka ya Fulani.):

Mmoja katika wanafalsafa na urafaa (sufi), mwanamapinduzi aliye-fanikiwa baada ya harakati za kijihadi, kuanzia mwaka 1804 hadi 1808, kusimamisha serikali ya Kiislamu huko Nigeria Kaskazini, maarufu kama mamlaka ya Fulani. Wengi waliomkubali, kama kiongozi, ni wakulima wa Kihausa. Dhulma na matatizo ya kiuchumi yaliyowakabili kutoka kwa watawala mbalimbali ziliwafanya wengi kumuona kama mwokozi aliyebashiriwa, Mahdi. Lakini alikanusha kwamba yeye siye Mahdi.

¹⁸ Suyuti, *Tarikhul Khulafa*, uk.243.

¹⁹ Suyuti, *Tarikhul Khulafaa*, uk. 246.

²⁰ “**Usman dan Fodio.**” *Encyclopædia Britannica*. [Ultimate Reference Suite](#). Chicago: Encyclopædia Britannica, 2008.

⇒ HITIMISHO

Historia inathibitisha kwamba:

- Imani ya Mahdi ilikuwepo **toka enzi za mwanzo wa Uislamu**, miongoni mwa masahaba, watoto na wajukuu wa masahaba, matabiina, wachamungu, ulamaa na mafuqahau wa hapo Madina.
- Imani hiyo imekuwepo miongoni mwa Waislamu wawe ni Sunni au Shia bila mipaka ya kimadhehebu.
- Maimamu wa Nyumba Ya Mtume (Ahlul Bayt) wamehusishwa zaidi na umahdi. Hii ni kielelezo cha hadithi kwamba Mahdi atokana na kizazi cha Mtume (saww).
- Itikadi ya umahdi ni mashuhuri katika Uislamu kiasi kwamba wanamapinduzi na watawala waliosimama kuondoa dhulma na kuweka uadilifu walitazamwa kuwa ni akina Mahdi kama vile Muhammad bin ‘Abdullah bin Hasan, Umar bin ‘Abdulaziz, Uthman Dan Fodio, Mahdi wa Sudan...
- Wanamapinduzi wakubwa kama vile Abu Muslim Khurasani aliyetokomezwa utawala wa Bani Umayyah pia walitumia itikadi ya umahdi kuwahamasisha Waislamu.
- Imani ya Mahdi ni itikadi sahihi ya Kiislamu iliyothibiti kwa dalili za Qur’ani, Sunnah, historia na akili. Kuikanusha ni ukafiri. (Fatwa ya Ibn Hajar Haythamy na ulamaa wengine wengi)²¹

²¹ Shaykh Ibn Hajar Haythamiy Al Shafi’i, Shaykh Muhammad bin Muhammad Al Khat-waabiy Al Maalikiy, Shaykh Yahya bin Muhammad Al Hambaliy na Shaykh Ahmad Abu Assuruur bin AlSwabaa Al Hanafiy. Hawa ndiyo waliokuwa ulamaa wa watu wa Makka na mafaqihi wa Waislamu kwa madhehebu nne. Wote waliwafikiana kwamba hadithi za Mahdi ni Mutawaatir na kwamba mwenye kuzikanusha lazima aadabishwe hata arejee kwenye haki na akikataa auliwe.

B. KAULI ZA ULAMAA WA KISUNNI KWAMBA IMAM MAHDI NDIYE BIN IMAM HASAN ASKARIY (AS)

Ulamaa wa Kisunni wamekubaliana –ila wachache- kuhusu kuwepo kwa Imam Mahdi (as) na kwamba ni yeye ndiye aliyebashiriwa na Mtume Mtukufu (saww) kuwa atadhihiri katika zama za mwisho na kusimamisha dola moja ulimwenguni kote. Wamekubaliana kwamba Imam Mahdi (as) ni Imam wa kumi na mbili mtoto wa Imam Hasan Al-Askariy. Hawa ni baadhi ya wanazuoni maarufu:

1. Muhammad bin Talha Shafei:

Muhammad bin Talha bin Muhammad Qarashi Naswiibi anasema:

“Muhammad bin Hasan Khalis, mwana wa Ali Mutawakkil, mwana wa Muhammad Qane’, mwana wa Ali ar-Ridha, mwana wa Musa Kadhim, mwana wa Ja’far Sadiq, mwana wa Muhammad Baqir, mwana wa Ali Zainul Abidiin, mwana wa Husayn Zaki, mwana wa Ali Murtadha, mwana wa Abu Talib. Ndiye Mahdi, Hujjah (Hoja, Dalili), Khalaf Salih (mrithi mwema), yule anayesubiriwa amani iwe juu yake.”

2. Ibn Arabi (kaf. 638 H.):

Muhyuddin Muhammad bin Ali maarufu kama Ibn Arabi Andulusiy, katika kitabu chake ‘*al Futuhaatul Makiyyah*’ amesherehesha kuhusu uimamu wa Imam Mahdi (as). Anasema: “Mahdi atadhihiri katika zama za mwisho kama vile alivyotabiri Mtukufu Mtume (saww). Yeye atokana na Ahlul Bayt (as) waliotoharishwa. Babu yake khalifa huyu ni Husayn bin Ali (as) na baba yake ni Hasan Askariy (as). ...”

3. Ibn Sabbagh, Nuruddin Ali bin Muhammad Maliki, (kaf.855 H.):

Katika kitabu chake *'Al-Fusulul Muhimma Fii Ma'rifatil Aimma'* anasema: “Imam wa kumi na mbili ni Muhammad bin Hasan.” Pia akaelezea tarehe ya kuzaliwa kwake na dalili ya uimamu wake.

4. Ibn Athir:

Ali bin Karam Muhammad bin Muhammad Shaybani, maarufu kwa jina la Ibn Athir Jazari katika *'Tarikh Ibn Athir, 5/373'* anasema: “Katika mwaka 260 H., Mtakaswa, Abu Muhammad Hasan Askariy Alawi alifariki. Alikuwa ni Imam wa kumi na moja wa Maimamu kumi na mbili wa Mashia Imamiyyah. Yeye ni baba yake Imam Mahdi (Muhammad) aliyezaliwa mwaka 232 H.”

5. Sibt Ibn Jawzi, Shamsuddin , Abu Muzaffar Yusuf bin Faza Ali, (kaf. 654):

Katika kitabu chake *Tadkiratul Khawas al-Aimma* ameandika: “Muhammad bin Hasan bin Ali bin Muhammad bin Ali bin Musa ar-Ridhwa bin Ja'far bin Muhammad bin Ali bin Husayn bin Ali bin Abi Talib (aS), ambaye kuniya yake ni Abu Abdillah na Abul Qasim, ndiye Khalifa, Hujjah, na Mwenye mamlaka ya zama, Qaim, na Msubiriwa wa mwisho wa Maimamu kumi na mbili.”

6. Abul Fida (kaf. 732 H.):

Abu Fida Ismail bin Ali katika kitabu chake *Tarikh Abil Fida, 2/152* ameandika “Imam Hasan Askariy ni mmoja katika Maimamu kumi na mbili wa Mashia. Yeye ndiye baba wa Muhammad, al Muntadhar aliyezaliwa mwaka 235 H.”

7. Qaramaani, Ahmad bin Yusuf, (1532 M. - 1610 M.), Mwanahistoria wa Dameshqi:

Qaramaani katika kitabu *Akhbaarud Duwal wa Aathaarul Uwal*, ameandika: “Imam Abul Qasim Muhammad bin Hasan Askariy ambaye alikuwa na umri wa miaka mitano pindi baba yake alipofariki, alikirimiwa na Mwenyezi Mungu hekima na elimu kama vile alivy-ombariki Nabii Yahya (as).”

8. Ibn Khallikan, Ahmad bin Muhammad (1211 M.- 1282 M.):

Mwanahistoria, kutoka Iraq. Aliandika kamusi maarufu kuhusu historia ya maisha ya watu ambao tu aliweza kuhakiki mwaka wao wa kufa. Ibn Khallikan katika kitabu *Wafayatul Ayan, 2/457*, ameandika historia ya maisha ya Imam Mahdi (as). Naye anasema: “Abul Qasim Muhammad bin Hasan bin Muhammad Jawwad, ni imam wa kumi na mbili miongoni mwa Maimamu kumi na mbili. Alizaliwa siku ya ijumaa tarehe 15 (15 Shaban) mwaka 255H.”

9. Dhahabi Muhammad bin Ahmad Shamsuddin, (1274 M.- 748 H./1348 M.):

Mwana historia wa Kiarabu na mwanathiolojia kutoka Dimashki. Kazi yake kubwa ni ile ya historia ya Uislamu hadi mwaka 1300.

Dhahabi, katika kitabu chake *Tarikh Dawlal-Islami, 5/115* ameandika kuhusu Imam Mahdi kwamba: “Tukio muhimu la mwaka 261H. ilikuwa ni kufariki kwa Imam Hasan bin Ali bin Jawwad bin Ridhwa (as) ambaye ni mmoja wa Maimamu kumi na mbili na baba wa Imam Msubiriwa, Muhammad bin Hasan.”

10. Sirajuddin Rufayi:

Shaykhul Islam, Abul Maali Sirajuddin Muhammad Rufayi katika kitabu chake *Swihaahul Akhbaar Fii Nasabis Saadatil Faatwimiyy-*

atil Akhyaar', aliandika kuhusu maisha ya Imam Ali Haadi: "Majina yake ya cheo (yaani Imam Ali Naqi) yalikuwa: Naqi (Mtakasifu), Aalim, (Mjuzi), Faqih (Mjuzi wa Sheria), Amir (Amiri), Daliil (Dalili, Hoja) na Askariy (Mkazi wa kambi ya jeshi)...alikuwa na watoto watano, Imam Hasan Askariy, Husain, Muhammad, Ja'far na Aishah. Ama Hujjah, Walii wa Mwenyezi Mungu, Imam Mahdi, Msubiriwa alizaliwa na Imam Hasan Askariy (as)." (rejea Sihahul Akhbar).

11. Shablanji , (kaf. 1255 H.):

Mu'min bin Hasan bin Mu'min Shablanji Shafiy, mwanazuoni aliyepambika.

Ameandika ndani ya kitabu chake maarufu, *'Nurul Absar Fii Manaaqibi Aali Nabyil Mukhtaar'*, mlango unahusu Imam Mahdi: "Muhammad bin al-Hasan al-Khalis bin Ali al-Hadi bin Muhammad al-Jawwad bin Ali ar-Ridhwa bin Musa al-Kadhim bin Ja'far as-Sadiq bin Muhammad al-Baqir bin Ali bin al-Husain bin Ali bin Abi Talib. Mama yake ni Ummul Walad, Narjis, Swaiqal, Susan. Jina lake la ubaba (kunya) ni Abul Qasim. Mashia Imamiya walimpa majina ya sifa yafuatayo: Hujjah, Mahdi, Khalaf Salih, Qaim, Muntadhar and Sahib-uz-Zaman."²²

12. Sulaiman Ibn Khwaja:

Shaykh Sulaiman bin Khwaja, mwanazuoni mkubwa wa Kihanafi na Sufi. Katika maelezo marefu alithibitisha kwa hoja na dalili ya kwamba Mahdi aliyetabiriwa na Mtume (saww) bila shaka ndiye Hujjah ya Mwenyezi Mungu, Muhammad bin Hasan Askariy.

²² Shablanji, Mu'min bin Hasan Mu'min, *Nurul Abswar fii manaaqibi Aali Bayti Nabyil Mukhtaar*, Molvi Mohammed Bin Gulamrasul Surtis Sons, uk. 185-189

13. Abdul Wahhab Sha‘rani, (897 M.- 973 M.):

Abdul Wahhab Ahmad bin Ali Sha‘rani, mwanazuoni mkubwa, Sufi, Qutbi wa tariqa Shadhiliyyah.

Anaandika katika kitabu chake Al-Yawaqit wal Jawaahir, “Imam Mahdi Msubiriwa ni mtoto wa Imam Hasan Askari alizaliwa tarehe 15 Shaban 255 B.H. na yuko hai hadi sasa. Umri wake ni miaka 703 (mwaka 958 H.) na ataendelea kuishi hadi atakapodhihiri na Isa bin Maryam atakuwa pamoja naye.

Shaykh Abdul Wahhaab As Shaaraaniy katika kitabu chake ‘*An-waarul Qudsiyyah*’ alisema: baadhi ya mashaykh wetu walisema: Sisi tumempa kiapo cha utii Imam Mahdi hapo Dameshq, Sham na tulikuwa kwake siku saba.

14. Khairuddin Zarkali:

Khairuddin Zarkali anasema: “Muhammad bin Hasan Askariy Khalis bin Ali al-Hadi, Abul Qasim ni imam wa mwisho wa Mashia Ithnaashariyyah ambaye ni maarufu kama Mahdi, Sahibuzzamaan, al Muntadhar, al Hujjat, Sahibu Sardaab. Alizaliwa Samarra na alipokuwa na umri wa miaka mitano baba yake alifariki. (Al Alaam, 6/309-310).

15. Baihaqi:

Ahmad bin Husayn, Abu Bakr (alifariki 458/1066) miongoni mwa maimamu wa hadithi. Faqih wa Kishafii miongoni mwa vigogo. Miongoni mwa vitiabu vyake: Sunanul Kubra, Sunanus Sughra, al Mabswuut.

Baihaqi Shafii anasema: “Watu wamehitilafiana kuhusu Mahdi. Wako wenye kuamini kwamba ni mmoja katika kizazi cha Fatima, Mwenyezi Mungu atamuumba atakapotaka. Wengine wakasema

Mahdi aliyeahidiwa alizaliwa siku ya Ijumaa tarehe 15 Shaabani 255, ambaye ni Muhammad mtoto wa Hasan Askariy... Umri wake mrefu siyo jambo muhali bali ni kama vile umri wa Isa bin Maryam (as) na Khidr (as). Kauli hii ni ya Shia Imamiya na pia wamekubaliana nao kundi miongoni mwa ‘Wenye kufunuliwa’. (Wafiyaatul A’yaan 3/316).

16. Al Kashifi, Husain bin Ali (kaf. 906 H.):

Husain, anasema: “Muhammad bin Hasan ni imam wa kumi na mbili na kun’ya yake ni Abul Qasim. Alizaliwa Samarrah.” (Raudhwatush Shuhada, uk. 326).

17. Salahuddin Safadi:

Shaykh Salahuddin Safadi anaandika: “Mahdi aliyeahidiwa ni yule yule imam wa kumi na mbili. Wa kwanza ni Bwana wa wachamungu Ali (as) na wa mwisho ni Mahdi.” (Yanabiul Mawaddah).

18. Muhammad Najjari:

Hafiz Muhammad bin Muhammad Najjari, mwanazuoni mashuhuri wa Kihanafi.

Anasema: “Abu Muhammad ndiye baba wa Imam Mahdi. Mwanaye ni Muhammad maarufu kwa watu wake wa karibu ambao ni waaminifu.” (Faslul Khitab).

19. Al-Haythamy, Shihabuddin Ahmad bin Hajar As Shafi, (kaf. 993 H.):

Katika kitabu chake ‘*As Swawa ‘iqul Muhriqah...*’ anaandika: “Abul Qasim Muhammad Al-Hujjah, na umri wake baada ya kufariki baba yake ni miaka mitano. Mwenyezi Mungu alimpa elimu na hikma ka-

tika umri huo mdogo. Anaitwa Al-Qaaim, Al-Muntadhar, kwa kuwa hakuonekana na alighibu na haikujulikana wapi alipo.”

**20. Al Kanji, Muhammad bin Yusuf bin Muhammad,
(kaf. 658):**

Katika kitabu chake ‘*Al Bayan fi Akhbar Sahibuz Zamaan*’: ‘Moja katika dalili zinazothibitisha kwamba Mahdi yuko hai katika Ghayba ni kuwepo Nabii Isa bin Maryam (as) na Nabii Ilyas (as) miongoni mwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuwepo Ibilis na Dajjal miongoni mwa maadui wa Mwenyezi Mungu.’

**21. Sayyid Khwaja, Muhammad Parsa Al Bukhariy
(746 H. - 822 H.):**

Mwanahadithi, Mwanairfani, aalim wa tafsiri. Mmoja katika ulamaa wakubwa wa Kihanafi na tarika Naqshabandiyyah.

Katika kitabu chake ‘*Faslul Khitab liwaswul Ahbaab*’: “Mwenyezi Mungu amempa Mahdi hekima katika umri mdogo kama vile alivyompa Nabii Yahya (as) na Nabii Isa (as). Mwenyezi Mungu amempa umri mrefu kama vile alivyompa Nabii Khidhr (as). Ukhalifa na uimamu umekoma na Mahdi. Yeye ndiye Imam toka alipofariki baba yake hadi Siku ya Hisabu. Nabii Isa (as) ataswali nyuma yake na atawaita watu wamfuata.”

22. Sa’aduddin Hamawi: Shaykh wa mashaykh:

“Mwenyezi Mungu amechagua wasimamizi kumi na mbili kutoka Ahlul Bayt kwa ajili ya umma huu na kuwafanya makhalifa (warithi) wa Mtume. Na mlinzi wa mwisho na mwakilishi wa kumi na mbili ni Mahdi Sahibuz Zamaan.”

23. 24. Shaykh Shihabuddin bin Umar al-Hindi, maarufu kama ‘Malikul Ulamaa’:

Katika kitabu chake ‘*Hidayatus Su’adaa*’: “Imam wa tisa kutoka ndani ya kizazi cha Imam Husayn ni Hujjah (Hoja) wa Mwenyezi Mungu Qaim Mahdi, aliyeghibu. Ataishi maisha marefu kama vile Isa, Ilyas na Khidhr (miongoni mwa waumini) na Dajjal na Samiri (miongoni mwa makafiri).

24. Kamaluddin Muhammad bin Twalha Al-Halabiy As Shafi’i (kaf. 652 H.):

Katika kitabu chake ‘*Matalibus Sauul Fii Manaakibi Aalir Rasuul*’ na pia katika kitabu chake ‘*Ad Durrul Munaddham*’ alisema: “Al-Mahdi (as) ni mtoto wa Abi Muhammad Al-Askariy. Alizaliwa Samaraa.

25. Muhammad bin Ibrahim Al Juzayniy Al Hamuwayniy, (kaf.722 H.):

Mwanahadithi wa Kishafi’i, mtaalam wa herufi.

Katika kitabu chake ‘*Faraaidus Simtwain*’, anaandika: Dibil Al Khuzai alipokea kutoka kwa Imam Ali Ridhwa (as) aliyesema: ‘Hakika Imamu baada yangu ni mwanangu Muhammad Al Jawad, kisha baada yake ni mwanaye Ali Naqi, kisha baada yake ni mwanaye Hasan Al Askariy. Baada yake Imam ni mwanaye Muhammad Al Hujjah, Al Mahdi, Al Muntadhar katika ghaiba yake na mtiwa wakati wa kudhihiri kwake’.

26. As Swafdy, Swalahuddin (kaf.764 H.):

Katika mashaykh wakubwa waliobobea katika siri za elimu ya herufi.

Katika ‘*Sharh Dairah*’ anasema: ‘Hakika Mahdi aliyeahidiwa ndiye imam wa kumi na mbili, wa kwanza ni Sayyidna Ali (as) na wa mwisho ni Mahdi (as)’.

27. Abdurahman bin ‘Ali Bastami (kaf. 858 H./1454 M.):

Alikuwa mjuzi kuliko ulamaa wote wa zama zake katika elimu ya herufi. Msufi, mwanahistoria. (Yanabiul Mawaddah).

28. Shabrawi ‘Abdullah bin Muhammad As Shafii (1091H. – 1171H.):

Katika kitabu chake: ‘*Al Ithaafu Bihubbil Ashraaf*’

29. Muhammad As Swabaan Al Miswriy:

Allamah wa zama zake. Katika kitabu chake ‘*Is ‘aafu ArRaaghibiin*’

30. Sharif Samhuudiy, Nuruddin Ali:

Katika kitabu chake *Jawaahirul Aqdayn Minal Quswaswil Ajiibah wa Barakaati Ahlil Bayt Nabawiy*.

31. Muhammad Amin Baghdady Suyedi, (kaf. 1830):

Mwandishi wa Iraq, mtaalamu wa nasaba katika ‘*Sabaikuz Dhahab Fii Maarifatil Qabail Arab*’.

**32. Sharif Hashim bin Sulayman Al Hasaniy Al Bahraaniy, ka-
tika kitabu ‘*Al Muhjatu fimaana nazala fiil Qaaimil Hujjah*’.**

33. Az Zarandiy, Shamsuddin Muhammad bin Yusuf:

Kitabu chake: ‘*Mi’raajul Wusuul ilaa Ma’rifati Fadhl Aali Rasuul*’.

34. Abdullah bin Muhammad Al Matwiiriy As Shafiy:

Katika kitabu chake: *‘Riyaadhu Zaahiirah fi Fadhl Aali Baytin Nabiy wa Itratihit Twaahirah.*

35. Jalaaluddin Suyutwiy:

Katika risala *‘Ihyaail Mayyit bifadhail Ahlil Bayt’*

36. Sulayman bin Khawaajah Al Qanduuziy:

Kitabu *‘Yanaabiiul Mawaddah’.*

37. Fadhl bin Ruuzabahaan:

Katika Sharh ya *As Shamaail cha Tirmidhiy.*

38. Muhammad bin Khawand Shah (kaf. 903 H.)

Katika kitabu chake *‘Rawdhwatu Safaah’* Juz. 3, Uk. 19, ameelezea habari za Imam Mahdi kuhusu kuzaliwa kwake na karama zake kwa upana.

39. Afandiy, Bahluul Bahjat:

Kitabu chake: *‘Al Muhaakamah fi Taarikh Aali Muhammad’.*

40. Shaykh Sadrudin Quunawiy:

Mmoja katika urafaa wakubwa

Kitabu chake: *‘Swihaahul Akhbaar fi Nasabis Saadatil Faatwimiyyatil Atwhaar’.*

41. Husayn bin Muhammad Ad Diyaar Bakry Al Maalikiy, (kaf. 966):

Katika kitabu Chake *‘Taariikhul Khamiis, Juz.2, Uk.321.*

NATIJA

Kauli za ulamaa hawa wakubwa ni hoja ya nguvu na ya kukinaisha kihistoria kwamba Imam Mahdi (as) ni Imam wa Kumi na Mbili katika kizazi cha Mtume (saww). Imam Mahdi alikwishazaliwa, ni yule yule mtoto wa Imam Hasan Al Askariy, ambaye alizaliwa tarehe 15 Shaaban 255 H.

Hii ni kwa sababu miongoni mwao wamo mafaqihi, wanahadithi, wanatafsiri, wanahistoria, wanairfani..... Hawa ni wataalamu ambao hawawezi kuandika ila baada ya utafiti na kupata dalili. Kauli zao zinatokana na Qur'ani, Sunnah na Historia.

VITABU KUHUSU GHAYBAH VILIVYOANDIKWA KABLA YA KUZALIWA IMAM MAHDI (AS)

Historia kamili ya Mahdi ikielezea kila hatua ya maisha yake ilisimuliwa na Mtume (saww), Imam Ali (as) na maimamu wote wa Ahlul Bayt (as) miaka mingi kabla ya yeye kuzaliwa. Ulamaa, wasimulizi wa hadithi na wafuasi wa maimamu waliandika vitabu kamili kuhusu ghaiba miaka mingi kabla ya kuzaliwa Imam Mahdi (as). Vitabu hivyo ni ushahidi wa kutosha kwamba kweli chimbuko la itikadi kuhusu Mahdi ni Mtume (saww) na maimamu wa Ahlul Bayt (as). Hii ni baadhi ya mifano:

1. **Ali bin Hasan bin Muhammad Ta'i**, sahaba wa Imam Musa Kadhim (as). Alikuwa faqihi na msimulizi wa hadithi mkweli. Aliandika kitabu kuhusu ghayba.
2. **Ali bin Umar Araj Kufi**, sahaba wa Imam Musa Kadhim (as). Aliandika pia kitabu kuhusu ghayba.
3. **Ibrahim bin Salih Anmati**, sahaba wa Imam Musa Kadhim (as). Aliandika pia kitabu kuhusu ghayba.
4. **Hasan bin Ali bin Abi Hamza**, aliishi zama za Imam Ali ar-Ridha. Aliandika pia kitabu kuhusu ghayba.
5. **Abbas bin Hisham Nashiri Asadi**, (alifariki 220 H./835 M.). Alikuwa mtu mashuhuri na maarufu. Alikuwa miongoni mwa masahaba wa Imam Ali ar-Ridha (as). Pia aliandika kitabu kuhusu ghayba.

6. **Ali b. Hasan bin Faddal**, alikuwa aalimu mkubwa na mkweli katika usimulizi wake wa hadithi. Alikuwa sahaba wa maimamu Ali Hadi (as) na Hasan Askariy (as). Aliandika pia kitabu kuhusu ghayba.
7. **Fadl bin Shadhan Nishaburi**, alikuwa miongoni mwa mafaqih na mmoja katika masahaba wa maimamu Ali Hadi na Hasan Askariy (as). Alifariki mwaka 260 B.H/873B.K. Naye aliandika kitabu kuhusu Mahdi na ghayba.

BISHARA KATIKA VITABU VINGINE

Mwenyezi Mungu katika kila zama alituma Mitume kuja kuwalingania watu njia iliyo sahihi na mfumo wa maisha anaouridhia (Uislamu). Lakini historia inashuhudia kwamba nidhamu ya kishetani ambayo inasimika misingi ya dhulma na uonevu imekuwa na nguvu na kutawala kiasi kwamba wale walio wema na wenye kutaka uadilifu hufikia kukata tamaa na kuvunjika moyo na kusema ‘Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itafika?’

Katika hali kama hii, Mitume walifundisha kanuni muhimu inayotawala maisha ya mwanadamu ambayo ni: ‘batili hata kama itakuwa na nguvu, lazima itaondoka na kuangamia itakaposimama haki, na hivyo mwisho mwema ni wa waja wema wanaojisalimisha kwake Mwenyezi Mungu.’

Kama zinavyohibitisha Aya tulizozitaja, Mitume wote katika maandiko matakatifu walitabiri zama za mwisho na kwamba ‘**batili**’ na nguvu zake zote itang’olewa na kuangamizwa na ‘**haki**’ kutawala dunia nzima. Zama hizi za ushindi na uokovu ndiyo zama za Imam Mahdi (a.t.f.). Kwa hiyo siyo ajabu kuona kwamba maandiko ya dini mbali mbali yanaelezea imani hii ya ushindi wa haki na kuja kwa

mwokozi atakayetawala dunia nzima na kusimamisha nidhamu na utawala wa Mwenyezi Mungu.

1. Imani ya MAHDI katika Umajusi (Uzorastri):²³

Umajusi ni dini ya Ufursi ya zamani (Iran kabla ya Uislamu). Mafunzo yake yanaashiria kwamba ni dini sahihi iliyoharibika baada ya kuletewa hoja na Mtume wao kama vile ilivyotokea kwa Mayahudi, Waarabu na Wakristo.

Moja katika imani za Umajusi ni kwamba mtu aitwaye Saoshyant (mwokozi wa ulimwengu) atadhihiri zama za mwisho (Zama za mwisho) na kuokoa ulimwengu na nguvu za kishetani (Ahriman), na kusimamisha nidhamu ya uadilifu itakayoleta neema, amani, utulivu kote duniani.

Kama vile Hadithi tukufu za Mtakaswa Mtume (saww) zinasema kuwa Imam Mahdi (as) atasafisha dunia na kila aina ya ushetani, maandiko ya kimajusi yanasema:

“... Pindi Astvat-ereta [hazrat Mahdi (as)] atakapodhihiri, kama khalifa wa Allah, atasafisha dunia na kila bati... atamtazama muumbaji kwa macho ya elimu...wasaidizi wake wenye ushindi watadhihiri pamoja naye...”
(Zamyad Yasht, Ibara 89-93)

Katika kitabu cha ‘Zand’, moja wapo ya vitabu vya Kimajusi, imeandikwa kuhusu zama za mwisho kwamba:

“Kisha, Izadan atasaidiwa na Ahura Mazda (Mwenyezi Mungu) na kupata ushindi mkubwa dhidi ya ma-Ahriman (mashetani). Baada ya ushindi wa Izadan ndiyo wanaadamu watakaponeemeka.”

²³ *Imam Reza network*

Kitabu cha Jamasb, mmoja wa ulamaa wa Kizorastri, kinaelezea sifa za mwokozi (Imam Mahdi (as)) kama ifuatavyo:

“Mtu mmoja atatokezea ardhi ya Tazian kutoka kizazi cha Hashim akiwa na dini ya mababu zake; atakuja Iran akiwa na majeshi mengi; atasimamisha ustaarabu na kueneza uadilifu juu ya ardhi.”

Mahali pengine anasema:

“Katika kizazi cha Mtume wa mwisho atatokeza mtu ambaye atafuata dini ya mababu zake. Kwa uadilifu wake, watu wote kote duniani watakuwa wafuasi wa ‘Mehr Azmay’ (Mtume Muhammad (s)).”

2. Imani ya MAHDI katika Agano la Kale (Uyahudi, Ukristo):

Katika Mwanzo 17:20, Mwenyezi Mungu alijibu dua ya kipenzi chake Nabii Ibrahim (as) kwa kumbariki mwanawe Nabii Ismail (Ishmael) na kwamba atakuwa na matunda mazuri na watoto wengi. Na pia atabarikiwa katika kizazi chake kupata masayyid kumi na mbili. Pia Mwenyezi Mungu atamfanya kuwa taifa kubwa. Hizi ni bishara zinazomhusu Mtakaswa Mtume Muhammad (saww) na kizazi chake (Aali Muhammad) waliotoharishwa ambao ni Maimamu, Masayyidi kumi na mbili. Huyu wa kumi na mbili (Wa mwisho) ndiye mbarikiwa Imam Mahdi (as) ambaye atakayesimamisha serikali ya Mwenyezi Mungu kote duniani.

Zaburi (kitabu cha Mtume Daudi (as), katika Agano la kale imeelezea matokeo ya mapambano baina ya ‘haki’ na ‘batili’ na kwamba batili itaangamizwa hapo zama za mwisho na Ulimwengu wote kutawaliwa na haki chini ya Mwokozi. Zaburi imeandika:

“Kwa sababu madhalimu wote wataangamizwa, ama watumishi wake Mwenyezi Mungu watarithi ardhi. Baada ya punde hapatakuwepo madhalimu...”

Zama za dhuhur, zinaelezwa:

“Mbwa mwitu ataishi na kondoo, chui atalala na mbuzi, ndama atafugwa pamoja na simba, na mtoto mdogo atawa-chunga. Hakutakuwepo hata chembe ndogo ya uharibifu wala ufisadi katika milima yangu mitakatifu kwa sababu dunia itaenea nuru ya Mwenyezi Mungu.”

Ama kuhusu ghaiba, inasema:

“Pamoja na kwamba matokeo ya haya yatachelewa, basi myasubiri, kwa sababu yatatokea kweli bila kusita.” – Re-jea pia Zaburi 72:1-20, Malaki 4:1-6, Isaya 11:1-9, zote ni bishara zinamhusu Mwokozi huyu mbarikiwa wa kizazi cha Nabii Ibrahim (as).

3. Imani ya MAHDI katika Agano Jipya (Ukristo):

Pia ndani ya Agano Jipya, zipo bishara ambazo tafsiri yake hai-kubaliani ila na shakhsiya ya Imam Mahdi (a.t.f.) kama mwokozi atakayedhihiri zama za mwisho. Baadhi ya bishara hizo ni: Ufunuo 22:1-2, pia Ufunuo 2:7, 11, 17, 26, pia Ufunuo 3:5, 12, 21. Katika Biblia neno ‘Mwana wa Adam’ limetajwa mara 80. Ni mara 30 tu ndiyo linamhusu Yesu (as). Mara 50 linamhusu mwokozi atakaye-dhihiri zama za mwisho.

4. Imani ya MAHDI katika maandiko ya Kihindu:

Katika kitabu cha Kihindu maarufu kama “Nask” imeandikwa kwamba: “Hapo karibu na mwisho wa zama (Akhirizzamaan),

kamanda mwadilifu ataweka mwisho wa dunia mbili. Kamanda huyu ni kiongozi wa malaika na binadamu. Haki ipo pamoja naye. Atamiliki kila kilichojificha ndani ya bahari, ardhi na mbingu.” Katika kitabu cha Kihindu “Shakmoni”, imeandikwa kwamba: “Ufalme katika dunia hii utamalizika kwa ujio wa mtoto wa mbora wa viumbe, “Koshen” (jina la Mtakaswa Mtume Muhammad (saww)). Atatawala milima ya Mashariki na Magharibi na kutembea juu ya mawingu...”

Yapo maandiko zaidi katika vitabu vya Kihindu kama vile: Vash-en-Jool, Dartek, Dideh Patkil, na Shaboohergan.

MLANGO WA 2

HISTORIA YA IMAM MAHDI (AS)

1 - IMAM MAHDI NI NANI?

2 - KUZALIWA NA KUONEKANA

3 - GHAYBA NDOGO (Sughra)

4 - GHAYBA KUBWA (Kubra)

1. IMAM MAHDI NI NANI?

Imam Mahdi (a.t.f.) ndiye Imam, Khalifa na Wasii wa 12 baada ya Mtume (saww). Yeye ndiye khalifa wa mwisho anayekamilisha idadi ya makhalifa kumi na mbili kama alivyowaelezea Mtume Muhammad (saww).

WAZAZI WAKE IMAM MAHDI (A.T.F.)

Baba yake ni Imam Hasan Askariy (as) ambaye ni mtoto wa Imam Ali Naqi (as), ambaye ni mtoto wa Muhammad Jawad (as), ambaye ni mtoto wa Imam Ali ar-Ridha (as), ambaye ni mtoto wa Imam Musa Kadhim (as), ambaye ni mtoto wa Imam Ja'far Sadiq (as), ambaye ni mtoto wa Imam Muhammad Baqir (as), ambaye ni mtoto wa Imam Ali Zainul-Abidin (as), ambaye ni mtoto wa Imam Husayn (as) mjukuu wa Mtume (saww).

Mama yake ni Bibi Narjis Khatun (r). Huyu Bibi mtukufu alikuwa kwa upande wa baba atokana na Kaizari wa Urumi. Kwa upande wa mama yake alikuwa ni katika kizazi cha Shamu'n

aliyekuwa wasii wa Nabii Isa (as). Bibi huyu alikuwa ni miongoni mwa wanawake watukufu wenye ukamilifu wa dini na imani. Yamtosha fahari kwamba yeye ndiye mama wa Imam huyu mtukufu ambaye atasimamisha serikali ya Mwenyezi Mungu kote duniani.

MAJINA YAKE

Jina lake ni Muhammad. Kuniya yake (jina la uzazi) ni kama ile ya Mtume: Abul Qasim

Lakabu zake (jina la sifa):

Mahdi, (aliyeongozwa). Hili ni jina wanalopewa wenye kuongoza kwenye haki.

Hujjat, (Hoja, dalili) hii ni kwa sababu yeye ni hoja ya Mwenyezi Mungu juu ya waja na viumbe Wake.

Qaim, (mwenye kusimama) hii ni kwa sababu atasimamisha haki.

Muntadhar, (anayesubiriwa) hii ni kwa sababu waumini watamsubiri sana kwa hamu.

Sahibuzzaman, (mmiliki, bwana wa zama) hii ni kwa sababu yeye kama Imam ndiye mwenye mamlaka ya Mwenyezi Mungu juu ya walimwengu.

Khalafu Salih, (mrithi, khalifa, kizazi, bakishomwema) hii ni kwa sababu yeye ni bakisho la familia tukufu iliyobarikiwa ya Mtume (saww) na khalifa wake wa mwisho.

Baqiyyatullah (salio la Mwenyezi Mungu), yeye ndiye khalifa wa Mwenyezi Mungu aliyebaki ndani ya ardhi hadi Kiyama.

TAREHE YA KUZALIWA KWAKE

Imam Mahdi (as) alizaliwa Ijumaa majira ya alfajiri, tarehe 15 Shaabani 255 H. /869 M. katika mji wa Saamarraa (Surra man ra-a) huko Iraq.

2. KUZALIWA NA KUONEKANA MUJIZA KAMA ILI-VYOKUWA KWA NABII IBRAHIM (AS) NA NABII MUSA (AS)

Historia inaonyesha ya kwamba zama za kuzaliwa Nabii Ibrahim (as), mnajimu mkuu wa mfalme Namrudh wa zama zile, alimpa taarifa ya kwamba atazaliwa mtoto wa kiume na ataangamiza ufalme wake. Namrudh alikabiliana na hali hiyo kwa kuamrisha wanawake wote wenye mimba wachunguzwe na watoto wa kiume wanaozaliwa wauliwe. Pamoja na ukatili wote huo, mama yake Nabii Ibrahim alichukua ujauzito na hakuwa na dalili yoyote ya mimba. Ilipowadia wakati wa kujifungua alitoka nje ya mji na kujifungua pangoni.

Historia hii inajirudia kwa Nabii Musa (as) na Firauni. Baada ya kupewa taarifa na mnajimu wake kwamba atazaliwa miongoni mwa Bani Israil mtoto wa kiume ambaye ataangusha utawala wake, Firauni aliamuru wanawake wote wachunguzwe na watoto wote wa kiume wauliwe. Kwa kudra ya Mwenyezi Mungu Nabii Musa (as) alizaliwa, na ajabu ya maajabu akaokotwa na mke wa Firauni na kulelewa ndani ya nyumba ya Firauni mwenyewe!

Mujiza kama huo ndio uliojitokeza pia kwa Imam Mahdi (as).

Baada ya Muawiya kushika madaraka katika mwaka wa 41 H., kizazi cha Mtume (saww) – Ahlul Bayt – walifikwa na mitihani na misiba isiyo na mfano. Pia wafuasi wao (Shia wa Ali) walifikwa na madhila na kila aina ya balaa. Muawiya aliamrisha Imam Ali

alaaniwe juu ya mimbari. Ni yeye ndiye aliyemghilibu Ju'dah binti Ash'ath (l.a.), mke wa Imam Hasan (as), na kumuua kwa kumpa sumu mjukuu huyu kipenzi cha Mtume (saww), bwana wa vijana Peponi, mwaka wa 50 H.

Hakuna unyama na ukatili na uadui dhidi ya Mtume (saww) na Uislamu kama ule aliyofanyiwa bwana wa vijana wa Peponi, mjukuu wa Mtume (saww) na kipenzi chake, Imam Husayn (as) na familia ya Mtume (saww) hapo Karbala na maluuni Yazid bin Muawiya mwaka wa 61 H. Imam Ali Zaynulabidin (as) alipewa sumu na Walid bin Abdul Malik Marwaan (l.a.) na kufariki mwaka wa 95 H. Imam Muhammad Baqir (as) alipewa sumu na Hisham bin Abdul Malik Marwaan (l.a.) na kufariki mwaka 114 H.

Hawa walikuwa ni Bani Umayyah ambao waliwaua Maimamu wa Nyumba ya Mtume (saww) na kufanya kila aina ya uovu dhidi ya kizazi chake. Wafuasi na wapenzi wa Nyumba hii ya Mtume (saww) (Mashia) walifikwa na misiba na mitihani adhimu. Sababu kubwa ni kugombea utawala na dunia. Walijua fika kwamba nafasi yao ya kutawala umma huu ni ndogo ikiwa Waislamu watawatambua viongozi wa haki ambao wamepambwa na kila sifa: elimu, uchamungu, ukamilifu, ushujaa, uadilifu n.k. Siasa waliyoitumia ndio hiyo ya kuwaua Mawalii wa Mwenyezi Mungu bila dhambi na pia kuwatesa na kuwaua Mashia wao. Hii ndiyo chachu iliopelekea Mashia kuitwa makafiri na kihalalisha damu zao na mali zao.²⁴

²⁴ Sera hizi hivi sasa zinaendelezwa na serikali ya kisaudi inayoongozwa na itikadi za kiwahabi. Mawahabi wamejitahidi sana kufuta alama na kumbukumbu za Mtume (s) na Ahlul Bayt (a.s.) kwa madai kwamba alama hizo zinapelekea Waislamu kufanya Shirk! Aya na hadithi zinazowatukuza Ahlul Bayt (a.s.) zimekuwa zikipewa maudhui tofauti. Uadui huu unadhihirika wazi katika msahafu aliyotafsiri Sh. Abdallah Saleh Farsi. Hakuna mahala Ahlul Bayt (a.s.) wamesifiwa. Uchochezi wa kuwaita mashia makafiri na kutoa fatwa ya kuwaua umedhihiri wazi huko Irak katika matukio mbalimbali ya kujitoa muhanga na kuua wanawake na watoto wasio na hatia. Waislamu tuamke tujee dini yetu na viongozi wetu tuliousiwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s) kabla hajaondoka nao ni maimamu kumi na mbili ambao ni matunda bora ya mti wa utume. Tuache kufuata watu ambao wana-

Bani Abbas waliangusha utawala wa Bani Umayyah mwaka 132 H./750 M. kwa kutumia nembo ya Ahlul Bayt (as). Lakini pindi tu walipopata utawala waligeuka na kuwa waovu na wabaya kwa Ahlul Bayt (as) na Mashia wao kuliko Bani Umayyah.

Imam Ja'far Sadiq (as) alifariki mwaka 148 H. kwa kupewa sumu na Mansur Dawaniqi (l.a.),²⁵ Imam Musa Kadhim (as) alifariki mwaka 183 H. kwa kupewa sumu na Harun Rashid (l.a.),²⁶ Imam Ali ar-Ridha (as) alifariki mwaka 203 H. kwa kupewa sumu na Ma'mun Rashid (l.a.),²⁷ Imam Muhammad Taqi (as) alifariki mwaka 220 H. kwa kupewa sumu na Mu'tasim Billah Rashid (l.a.),²⁸ Imam Ali Naqi (as) alifariki mwaka 254 H. kwa kupewa sumu na Mu'taz Billah (l.a.), Imam Hasan Askariy (as) alifariki mwaka 260 H. kwa kupewa sumu na Mu'tamad (l.a.).

Kwa sababu za utawala na kisiasa, watawala hawa madhalimu hawakuogopa kumwaga damu ya Mtume (saww) ambayo ni ya kizazi chake kilichotoharishwa na Mwenyezi Mungu. Pia wakawatesa na kuwaua wengi miongoni mwa wafuasi wao waliokuwa wema waliopambika kwa uzuri wa imani na tabia. Huu ni ukafiri wa sampuli gani na husuda iliyoje dhidi ya Mtume (saww). Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيَّ بِغَيْرِ
حَقٍّ وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ يَأْمُرُونَ بِالْقِسْطِ مِنَ
النَّاسِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٥٦﴾

lenga kusimika utawala wao wa kidhalimu na kusaliti Uislamu. Waliyoyafanya watawala wa Bani Umayyah, Bani Abbas na Uthmaniyyah yatutoshe kuwa ni funzo.

²⁵ Abdullah bin Muhammad bin Ali bin Abdillah bin Abbas khalifa wa pili wa kiabbasi

²⁶ Harun bin Mahdi bin Mansur khalifa wa 5 wa kiabbasi

²⁷ Abdullah bin Harun Rashid, khalifa wa 7 wa kiabbasi

²⁸ Muhammad bin Harun Rashid, khalifa wa 8 wa kiabbasi

**“Hakika wale ambao wanazikufuru aya za Mwenyezi Mungu kisha wakawaua mitume pasi na haki na wakawaua wale ambao wanaoam-risha mema miongoni mwa watu, basi wabashirie adhabu aliyo kali.”
(3:21).**

Kwa hiyo mtawala wa Kibani Abbasi al Mu‘tamad bin al Mutaw-akkil, alikuwa bila shaka ana taarifa kuhusu Imam Mahdi (as) kwamba ni Imam wa kumi na mbili na lazima azaliwe na Imam Hasan Askariy (as) ambaye ni wa kumi na moja. Kama walivyokuwa mafirauni wenzake hakumuogopa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Imam Hasan Askariy (as) alifungwa na kuteswa ili asipate nafasi ya kuongoza umma. Wafuasi wake (mashia) walisakamwa popote walipokuwa, waliteswa na kuuliwa vibaya. Kipindi hiki kilikuwa kibaya sana, kwa kutawaliwa na machafuko ya kisiasa, na mapambano ya kialawi²⁹ dhidi ya utawala. Katika hali kama hii utawala uliongeza tahadhari na udhibiti ili kuhakikisha nani Imam baada ya Hasan Askariy (as). Uchunguzi ulifanywa kwa wake zake kama wana ujauzito. Lakini pamoja na jitihada zote hizo, nuru ya Mwenyezi Mungu ilidhihiri, Imam Mahdi (as), Imam wa zama hizi, alizaliwa tarehe 15 Sha’ban 255 hapo Saamarra bila ya mtu yoyote kutambua.

RIWAYA KUHUSU KUZALIWA KWAKE

Al-Mas‘udiy³⁰, pia Shaykh Sadduq na Shaykh Tusi wameandika riwaya hii kuhusu kuzaliwa kwa Imam Mahdi (as):

Bibi Hakima binti Imam Jawad (as), shangazi yake Imam Hasan Askariy alikuwa mwanamke mtukufu aliyekamilika kiimani na kita-

²⁹ Mapambano ya kialawi: mapambano yalioongozwa na Masayyid wa kizazi cha Mtume (s). Alawi ni kwa kunasibishwa na Imam Ali (a.s.) ambaye ndiye mume wa Bibi Fatima (a.s.).

³⁰ Al-Mas‘udy, Abul Hasan ‘Ali bin Husayn, 893-956 M. Mwanahistoria, mwanajeografia. Kaandika vitabu katika elimu mbali mbali. Kaandika historia ya Imam Ali (a.s.), na Ah-lul Bayt (a.s.) katika *Ithbatul waswiyyah lil Imam Ali bin Abi Talib (a.s.)*. Nasaba yake inafika kwa sahaba wa Mtume (s) Ibn Mas‘ud (*AlMunjid*)

bia kama alivyokuwa bibi yake Sayyida Fatima Zahraa (as). Bibi Hakima anaelezea kwamba: “Baada ya kufariki Abul Hasan (Imam Ali Naqi (as), mwanawe Abu Muhammad (Imam Hasan Askariy (as), alichukua nafasi yake ya Uimamu. Nilikuwa niki mzuru mpwa wangu kama ilivyokuwa ada yangu kumzuru ndugu yangu. Siku moja Bi Narjis akaja kunivua viatu akisema: Ewe bimkubwa wangu acha nikuvue viatu vyako, lakini nikamjibu: ‘hasha, wewe ndiye bimkubwa wangu na Wallahi kamwe sitokuruhusu univue viatu wala unihudumie, bali mimi nitakuhudumia’. Imam Hasan Askariy (as) akayasikia hayo na akasema: ‘Mwenyezi Mungu akujaze kila kheri ewe shangazi yangu’. Nikakaa hapo hadi ulipowadia wakati wa magharibi, nikaomba nguo zangu ili niondoke. Imam (as) akaniambia: ‘Ewe shangazi yangu leo ulale hapa kwani usiku huu atazaliwa mtoto mtukufu kwa Mwenyezi Mungu ambaye Mwenyezi Mungu atamtumia kuhuisha ardhi baada ya kufa.’ Baada ya kuambiwa kwamba ni Bi Narjis ndiye atakayemzaa nilistaajabu kwani sikuona dalili za mimba. Nilimchunguza bila kuona chochote na niliporejea kwa Imam (as) alitabasamu na kuniambia: ‘Itakapofika wakati wa alfajiri, Mwenyezi Mungu atadhihirisha mimba yake kwani mfano wake ni kama ule wa mama yake Musa (a.s.)...’

Ilipofika alfajiri, Bi Nargis alishtuka na kuwa mwenye fadhaha. Nilimkumbatia na kumsomea. Imam alipaza sauti na kusema: ‘Msomee *innaa anzalnaahu fi laylatil qadr*’... nikamsomea na mara nikasikia mtoto tumboni ananitolea salamu na kusoma kama ninavyosoma. Niliingiwa na hofu na kufadhaika. Imam (as) akapaza sauti na kusema: ‘Usistaajabu na amri ya Mwenyezi Mungu, hakika Yeye hututamkisha ya hikma tukiwa wadogo na kutujalia kuwa ni hujjah (hoja) katika ardhi yake tukiwa wakubwa.’ Punde tu nikashtukia simuoni Nargis kana kwamba imeteremshwa pazia baina yangu na yeye. Nilikimbilia kwa Imam (as) nikipiga yowe.

Imam (as) alinifariji na kuniambia: ‘Ewe shangazi yangu rejea kwani utamkuta bibiye mahala pake.’ Nilirejea na kuona ile pazia imeondoka, naweza kumuona. Alikuwa amefunikwa na nuru. Hapo nikamuona mtoto amesujudu, amepiga magoti... na huku akisema : ‘*Ash hadu an la ilaaha illa LLAH wahdahu laa shariika lahu* (nashuhudia ya kwamba hakuna mungu ila Allah peke yake hana mshirika) na kwamba babu yangu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake, na kwamba baba yangu ni Amiri wa waumini.’ Kisha akataja Imam baada ya Imam hadi kufikia kwake. Baada ya hapo akasema: ‘Ewe Mwenyezi Mungu nitekelezee ahadi yangu na uthibitishe nyayo zangu na (kwa kunitumia mimi) ijaze ardhi uadilifu na usawa.’ Imam Hasan Askariy (as) akamuomba shangazi yake amlete mtoto huyo mtakatifu. Alipofika mbele ya baba yake alimtolea salaam...

KUTAMBULISHWA RASMI

Imam Hasan Askariy alimtambulisha rasmi Imam Mahdi (as) mbele ya wafuasi wake waadilifu ili wawe ni mashahidi wa haki kuhusu kuzaliwa kwa Imam Mahdi (as). Hii ilikuwa ni kukamilisha hoja ili asiye yeyote akakanusha kuhusu kuzaliwa kwake.

Baada ya kuzaliwa, jambo hili liliwekwa siri sana. Imam Hasan Askariy (as) aliwafahamisha wachache tu miongoni mwa wafuasi wake ambao ni waaminifu. Abu Ghanim, mmoja katika wahudumu wa Imam Hasan Askariy (as) alisema: ‘Siku ya tatu, baada ya kuzaliwa Imam Mahdi (as), baba yake Imam Hasan Askariy (as) alimleta mbele ya wafuasi wake na kumtambulisha kwa kusema: “Huyu ndiye *Waliyul Amr* wenu (bwana mwenye mamlaka ya kuwatawalia mambo yenu) na wasii wangu. Yeye ndiye ‘Qaim’ anayesubiriwa na walimwengu. Pindi ulimwengu utakapojaa dhulma na jeuri, basi atadhihiri na kuuajaza haki na uadilifu.”

Muawiyah bin Hakim, Muhammad bin Ayyub, Muhammad bin Uthman, kila mmoja wao anashuhudia ya kwamba Imam Hasan Askariy alimtambulisha Imam Mahdi mbele yao wakiwa nyumbani kwake watu arobaini.³¹

3. GHAYBA NDOGO (SUGHRA)

“Mahdi atokana na kizazi changu. Atakuwa ndani ya Ghayba na atakapodhihiri, ardhi yote itafunikwa na uadilifu kama ilivyokuwa imejaa dhulma. (Mtume Mtukufu (saww)).

Imam Mahdi (as) alizaliwa zama za ukhalifa wa kidhalimu wa Bani Abbas. Khalifa wa zama hizo alikuwa ni al Mu‘tamid (870 - 892 M.). Hadithi za Mtukufu Mtume (saww) na bishara zake kuhusu Imam Mahdi (as) kwamba ni Imam wa kumi na mbili na ataondoa dhulma na jeuri hazikuwapa usingizi watawala hawa dhalimu.

Hila za utawala na mbinu za kumuuwa Imam Mahdi (as):

Kama walivyouliwa Maimamu waliotangulia, utawala huu jeuri ulipanga mbinu za kumuua Imamu huyu wa kumi na mbili tu pale atakapozaliwa! Lakini ni nani atakayeweza kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu? Ili kuhakiki kwamba Imam Mahdi (as) anauliwa, walimuweka baba yake Imam Hasan Askariy (as) chini ya uangalizi mkali na upelelezi. Pamoja na hila zote hizo, Imam Mahdi alizaliwa na wala utawala haukuweza kupata taarifa yoyote.

Kufariki baba yake Imam Hasan Askari (as):

Utawala wa kidhalimu wa Bani Abbas hukuridhika kumuona hai Imam Hasan Askari (as). Walimuua kwa sumu Ijumaa tarehe 8 Rabbiul Awwal 260 (873 M). Imam Mahdi (as) alijitokeza ghafla na kumswalia baba yake. Utawala ulimtafuta ili umuue lakini hakuna

³¹ Qarshy: *Biography of Imam Mahdi (a.s.)*

aliyeweza kumpata. Imam (as) akiwa na umri wa miaka mitano alimpoteza baba yake mtukufu. Kwa hiyo akachukua jukumu la kuongoza ummah. Tayari kwa umri huo, Imam alikuwa na sifa zote za uimamu na uongozi wa Mwenyezi Mungu kama walivyokuwa Maimamu wengine. Hii siyo ajabu kwani Mwenyezi Mungu aliwatunuku baadhi ya Mitume utume wakiwa wadogo. (Surah Mariam:12, 30).

Ghaiba ya Imam Mahdi:

- **MAANA YA GHAIBA:**

Ghaibah (غيبية) ni neno la kiarabu linalomaanisha kutokuwepo, kutohudhuria, kutoonekana.

Ghaiba ya Imam (as) ni kule kutoonekana na kutofahamika na watu. Watu watamuona lakini hawatamjua kama vile ndugu zake Nabii Yusuf (as), walimuona lakini hawakumtambua. Kwa hiyo Ghaiba haimaanishi kujitenga au kukaa mbali na watu. Kuna ghaiba mbili: Ghaiba ndogo na kubwa. Mtume (saww) na Maimamu walitabiri na kuelezea suala la ghaiba kwa uwazi ili kuepusha ummah kupotoshwa na madajjal. Imam Ja'far (as) alisema: “Kuna ghaiba mbili kwa Qaim (as). Moja ni fupi na ya pili ndefu.

- **GHAIBA NDOGO (Sughra):**

Ghaiba ndogo ilianza mwaka wa 260 H. na kuendelea kwa miaka 69.³² Katika ghaiba ndogo Imam hakuoneka wala kuwasiliana na watu moja kwa moja. Bali aliwasiliana na watu kwa njia ya wawaki-lishi, wanne ambao walikuwa miongoni mwa wafuasi watukufu wa Imam (as) na watiifu kwake. Waliwasilisha maswali na matatizo ya

³² Wapo baadhi ya ulamaa kama Shaykh Mufid na Sayyid Mohsin Amin Amili wanaosema ghaibah ilianza tu alipozaliwa Imam (a.s.). Kwa mtazamo huo ghaybah ndogo inakua miaka 74.

watu kwa Imam (as) na kuwaletea majibu. Wawakilishi wanne hao ni:

- * - Uthman Bin Sa'iid Amri: Pia alikuwa mwakilishi wa Imam Hasan Askariy (as). Siku ya 40, Imam Hasan Askariy (as) akiwa amekaa na wafuasi wake, alimtambulisha Imam Mahdi (a.t.f.) kwao. Mtoto mzuri aliyefanana naye aliletwa na hapo akasema: "Huyu ndiye Imam baada yangu na mrithi wangu juu yenu. Mtiini na msipotee baada yangu, vinginevyo dini yenu itaangamia nanyi pia. Fahamuni kwamba baada ya hapa hamtamuona tena hata kama maisha yenu yote mtajitahidi kuhakiki hilo. Basi, mkubali yale anayowaambieni Uthman. Mtii amri zake na msikilize anayoyasema, kwani yeye ni mwakilishi wa Imam wenu."
- * - Muhammad bin Uthman:
- * Baada ya kufariki Uthman bin Saiid, nafasi yake ikachukuliwa na mwanawe mchamungu Muhammad bin Uthman. Alifariki mwishoni mwa Jamadi-ul-Awwal mwaka wa 304 / 305 H.
- * - Husayn ibn Ruh ibn Bahr Nawbakhti:
- * Wakati akiwa mgonjwa, Muhammad bin Uthman alimtambulisha Husayn bin Ruh kuwa ndiye naibu wa Imam baada yake. Husain Ibn Ruh Nawbakhti, alikuwa mmoja katika mawakala wa Muhammad bin Uthman Baghdad. Alifanya naye kazi kwa karibu na kwa muda mrefu. Husain Ibn Ruh Nawbakhti alifariki katika mwezi wa Shaban 326 H.
- * - Ali Ibn Muhammad Samarri:
- * Naibu wa mwisho wa Imam (as) Ali bin Muhammad Samarri alifariki baada ya miaka mitatu tarehe 15 Shabani 329 H.

Siku sita kabla ya kufariki, Ali bin Muhammad Samarri, alipata ujumbe kutoka kwa Imam (as) ukimuelekeza: "... sasa jitayarishe, na wala usimteue yeyote nafasi yako kwani baada yako kipindi cha ghaiba kubwa kitaanza." – Makaburi ya manaibu hawa watukufu wanne wa Imam (as) yapo Baghdad.

4. GHAYBA KUBWA (KUBRA)

Mwaka 329 H. baada ya kufariki naibu wa nne, ghaiba kubwa ilianza. Hii ilikuwa ni mwanzo wa Imam (a.t.f) kutoonekana wala kuwa na mawasiliano na yeyote (kama wakili wake). Kama vile jua lina- vyokuwa nyuma ya mawingu na kuendelea kuangazia ulimwengu ndivyo Imam (as) wa zama hizi, khalifa wa Mtume (saww) alivyo- toweka machoni mwa walimwengu akisubiri siku ya kudhihiri. Ka- tika mlango huu tutachambua nukta zifuatazo:

- Umri mrefu,
- Anaishi wapi?
- Kuna faida gani kuwa na Imam asiyeonekana?
- Nafasi ya ulamaa wachamungu,
- Msaada na miujiza ya Imam Mahdi (as)

A. UMRI MREFU KINYUME NA MAUMBILE

Historia inaonyesha kwamba Imam Mahdi alizaliwa mwaka 255 H. Hivi sasa mwaka 1431 H. (2010) umri wake ni miaka 1176. Umri kama huu unastaajabisha! Hivi inawezekana mwanadamu kuishi umri kama huo? Je! Jambo hilo linakubalika kielimu?

Kwanza, wako binadamu ambao Mwenyezi Mungu amewajalia umri mrefu hapa hapa duniani. Miongoni wa watu hao ni:

- Nabii Nuh (as). Baadhi ya wanahistoria wanasema aliishi miaka 2500. Qur’ani inathibitisha kwamba alilingania watu wake miaka elfu kasoro hamsini (19:14)

- Nabi Adam (as) aliishi miaka 930.

Wako watu wengi ambao wameishi umri mrefu kwa kuzidi kiwango cha kawaida maradufu.

Pili, tuelewe sio jambo la ajabu. Mwenyezi Mungu (swt) amewabakiza hai baadhi ya waja Wake kwa siri maalum ambayo Yeye anajua hekima yake. Miongoni mwa Mitume:

- Nabii Khidhr (as)

- Nabii Idris (as)

- Nabii Ilyas (as)

- Nabii Isa (as)

Miongoni mwa waja wema wa Mwenyezi Mungu, ***Ashabul Kahf***, hawa Mwenyezi Mungu amewabakiza hai wamelala katika pango kwa miaka mia tatu na tisa (rej. Sura Kahf, 18:9-25). Kisha wakazinduka na watu wakashuhudia uwezo wa Mwenyezi Mungu. Baada ya miaka mia tatu na tisa waliamka na huku hawakubadilika! Hivi wako bado pangoni na watazinduka Zama za mwisho na kujiunga na Imam Mahdi (as).

Tatu, sayansi za viumbe hai zinathibitisha kwamba inawezekana kuongeza umri wa binadamu kwa njia ya lishe bora na dawa. Wanasayansi bingwa wanathibitisha kwamba mwanadamu anaweza kuiishi kwa maelfu ya miaka ikiwa tu kamba ya uhai wake haitakatwa.

Kwa hiyo hakuna sababu yoyote ya mtu kustaajabia umri mrefu wa Imam Mahdi (as) au akakanusha umahdi kwa sababu hiyo. Sisi kama waumini, tunaamini bila ya shaka ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila jambo. Ni Yeye ndiye aliyefanya moto kuwa baridi na salama kwa Mtume wake Ibrahim al-Khalil (as). Ni Yeye ndiye aliyedhihirisha uungu Wake kwa kuwapa Mitume wake hoja na miujiza.

B. ANAISHI WAPI?

Katika mambo ya uzushi na mbinu za kuwapaka watu matope ni ule uongo ulioenezwa kwamba Mashia wanaamini kwamba Imam wa 12 alitoweka hapo Samarra na kujificha ndani ya ‘Sardab’ (ghala chini ya ardhi). Kwa hiyo hapo ndiko anakoishi na kutokea hapo ndiko atakapodhihiri. Huu ni uongo na uzushi. Hakuna mwanazuoni wa Kishia aliyeandika hayo.

Hadithi sahihi zinaonyesha kwamba Imam anaishi miongoni mwa watu na kushirikiana nao bila ya wao kumtambua.

C. KUNA FAIDA GANI KUWA NA IMAM ASIYEONEKANA?

Suala la kuwepo Imamu ambaye haonekani linatatanisha waumini wengi. Na sababu ya msingi ni vipi Imamu aliye ughaibuni, haonekani, atanufaisha umma wake? Je kuna faida gani kuwa na Imamu usiyemuona wala huwezi kuwasiliana naye?

Utata huu unajitokeza kwa sisi kutokuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu nafasi ya Imamu kama *hujjah (hoja)* na kiongozi wa Mwenyezi Mungu juu ya ardhi. Kuweka wazi suala hili tutachambua nukta mbili muhimu:

1- Ulazima wa kuwepo Imam kama Khalifa wa Mwenyezi Mungu juu ya ardhi:

Hadithi nyingi zilizopokelewa kutoka kwa Maimamu wa Ahlul Bayt (as) zinathibitisha kwamba ardhi kamwe haiwezi kubaki bila kuwepo mtu ambaye ni Hoja ya Mwenyezi Mungu.

“Ardhi haiwezi kamwe kubaki bila ya kuwa na (mtu ambaye ni) Hoja ya Mwenyezi Mungu, awe dhahiri au haonekani. Ni kwa sababu yake ndiyo hoja za Mwenyezi Mungu na dalili zake hazipotei.”(Amirul Muminiin Ali (as)).

“Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkuu na Mwenye nguvu, kamwe hajaiacha ardhi bila Imam mwadilifu.” (Imam Ja’far Sadiq (as))

“Bila shaka, ardhi haiwezi kubaki bila mmoja wetu.” (Imam ar-Ridha (as))

Imam kama kiumbe kamili ndiye kiungo baina ya ulimwengu wa kiroho na ule wa kihisia (kimada). Akikosekana Imam basi ulimwengu utatoweka. Kukosekana yeye, watu hawawezi kumjua na kumwabudu Mwenyezi Mungu ipasavyo. Roho ya Imam ni kama vile chanzo cha umeme ambacho kinagawa nishati na nuru. Nuru na nishati kutoka ulimwengu usiyoonekana kwanza inaakisi kwenye roho ya Imam na ndipo inapozifikia nyoyo za walimwengu. Imam ni kiongozi na msimamizi wa walimwengu. Kwa hiyo Imam kama mrithi wa utume ni rehema kwa walimwengu. Wakati wa Ghayba watu wanafaidika naye kama vile watu wanavyofaidika na jua pindi linapofunikwa na mawingu.³³

Hadithi zifuatazo zinaweka wazi umuhimu wa watu hawa:

1. Imepokelewa kutoka kwa Imam Ali (as) kwamba Mtume (saww) alisema: “Nyota ni amani kwa viumbe wa mbingu.

³³ Ayatollah Ibrahim Amini, *Al Imam Al Mahdi, the just leader of humanity*, Qum, Ansariyan Publications, 1997, pp 154-146

Zikiondoka nyota, basi na viumbe vya mbingu vinatoweka. Basi na Ahlul Bayt (as) ni amani kwa viumbe wa ardhi. Wakitoweka Ahlul Bayt (as), basi na ardhi inatoweka.”

2. Imepokelewa kutoka kwa Imam Ja'far Sadiq (as) kutoka kwa babu yake, Imam Ali Zaynulabidin (a.s.) kwamba alisema: “Sisi ndiyo Maimamu wa Waislamu, pia sisi ndiyo Hoja za Mwenyezi Mungu juu ya walimwengu, na mabwana wa waumini, na viongozi.... Na Mawalii (wasimamizi, walinzi,...) wa Waislamu. Sisi ndiyo amani kwa watu wa ardhi kama vile ambavyo nyota ni amani kwa viumbe wa mbinguni. Ni kupitia sisi ndiyo mbingu inashikwa haiwezi kuanguka juu ya ardhi ila kwa idhini yake Mwenyezi Mungu. Ni kupitia sisi pia ndio ardhi inashikwa isitikisike, ni kupitia sisi ndio mvua inanyesha na rehema kuenea na Baraka za ardhi kutoka. Kama angekosekana juu ya ardhi katika sisi (Ahlul Bayt) basi ardhi ingetoweka na watu wake.” Kisha akasema: “Ardhi haijawahi toka Mwenyezi Mungu amuumbe Adam (as) kukosa Hoja ya Mwenyezi Mungu (Mwanadamu aliye na ukamilifu) ima mashuhuri (anafahamika) au asiyeonekana (amefichwa). Na kamwe haitamkosa mtu kama huyo hadi kitakaposimama Kiyama. Na kama isingekuwa hivyo, asingeabudiwa Mwenyezi Mungu”. (Al Qanduziy, S.I., uk. 75).

3. Imepokelewa kutoka kwa Mtume (saww) kwamba alisema: “Wana nini hawa watu ambao anapotajwa Ibrahim na Aali zake basi hufurahi, na iwapo hukumbukwa Muhammad na Aali zake nyoyo zao huchukia! Naapa kwa Yule ambaye mkononi mwake ipo nafsi ya Muhammad, lau kama mmoja wenu angekuja na vitendo vya mitume sabini, lakini asiwe na wilaya

ya Ahlul Bayt wangu basi angeingia motoni na huku dhalili na kufufuliwa ndani ya Jahannam mwenye hasara. Enyi watu! Sisi ni msingi wa imani na ukamilisho wake. Sisi ni wasia wa Mwenyezi Mungu katika wa mwanzo na wa mwisho. Na sisi ndiyo kiapo cha Mwenyezi Mungu aliapa kwa sisi aliposema: ‘Kwa tini na zaituni na mlima Sinai na huu mji wa amani.’ Kama sio sisi Mwenyezi Mungu asingeumba kiumbe, na isingekuwepo Pepo wala Moto”. (Al Barsiy, R. uk. 72).

2 MAANA YA GHAIBA

Ghaiba haina maana ya kwamba Imam hayupo, amewekwa mahala anasubiri kudhahiri na kwa maana hiyo hana msaada wowote wala kazi. Bali maana sahihi ni kama alivyosema Imam Sadiq (as) akimjibu Sulayman kwamba: “Watu wanafaidika na Imamu kama vile wanavyofaidika na jua linapokuwa nyuma ya mawingu.” Katika nidhamu ya jua (solar system), jua ndiyo muhimili wa kati wa nidhamu hiyo. Nguvu za mvutano zinawezesha sayari kuwa thabiti na kuendelea kuzunguka jua. Pia nishati ya jua ndiyo sababu ya uhai hapa kwenye ardhi. Faida hizi zinapatikana kwa jua kuwepo, iwe kuna mawingu au hakuna. (Amini, I. uk. 156/7).

Kisa cha Nabii Khidhr ndani ya Qur’ani, - ambaye yuko hai haonekani -kinaelezea jinsi alivyotoa msaada na mwongozo kwa Mtume aliye dhahiri naye ni Nabii Musa (as) (rejea: Surah Kahf, 18:65 -82). Waliiofaidika hapa ni maskini wamiliki wa safina na mayatima wawili. Ni kwa mithili hii Imam Mahdi ndivyo anawajibika na kuishi na umma wake na kutoa msaada unaohitajika.

Riwaya nyingi zimethibitisha wachamungu na watu wema kuku-tana na Imam na kunufaika naye. Na kwa njia hiyo umma kufaidika na mwongozo wake. Kwa maana hii ni kwamba Imam Mahdi (as)

yupo bali huwezi kumtambua kama ilivyokuwa hali kwa Nabii Khidr (as). Kwa hiyo anahudhuria mikutano, mikusanyiko na kuzungumza na watu na kuwaongoza na kuwasaidia. Msimu wa Hijja, anahiji na kuzuru sehemu takatifu. Anakaa na wanazuoni, mafaqihi na kujadiliana nao kuhusu masuala ya dini. Anazuru na kusaidia wagonjwa, wenye maafa, maskini... (Sadr, S. uk. 298-302).

3. GHAIBA INA FAIDA NA FADHILA NYINGI:

- A. Hili linawafanya waumini wawe katika hali ya tahadhari na msimamo wa kufuata sheria na kuiheshimu na kujiepusha kudhulumu wengine na kunyang'anya haki zao. Hii ni kwa sababu kudhihiri Imam Mahdi maana yake ni kusimamisha kiongozi na dola yenye uadilifu yenye kupambana na madhalimu na kila aina ya dhulma.
- B. Kila muumini anakuwa daima katika hali ya tahadhari na kujiandaa kujiunga na jeshi la Imam na kuwa tayari kujitoa muhanga katika njia ya kusimika utawala wa Imam kote ulimwenguni ili kusimamisha nidhamu na sheria ya Mwenyezi Mungu pekee. Mtazamo na hisia kama hizi zinajenga kwa waumini hali ya umoja na mshikamano wa safu kwa kuwa wote ni jeshi la Mwenyezi Mungu chini ya kiongozi mwadilifu, walii wa Mwenyezi Mungu Imam Mahdi (as).
- C. Ghaiba inamsukuma muumini kubeba majukumu hususan katika uwanja wa kuamrisha mema na kukataza maovu kwa kuwa wanaomsuibia kiongozi wao lazima wawe ni

wenye harakati za kuweka msingi na kuandaa mazingira ya mapinduzi hayo makubwa.

- D. Waumini kwa kuwa na kiongozi mtukufu kama huyu ambaye wanamtaraji wakati wowote, wanaishi daima wakiwa na hisia za matumaini, kujiamini na utukufu, kamwe hawako tayari kunyenyekea na kudhalilika mbele ya nguvu za mataghuti na majabari wanaohukumu kwa dhulma na jeuri. Kwa waumini hawa yote wanayoyamiliki makafiri ni duni na dhalili.

Hisia kama hizi zinampa muumini msukumo wa kupambana na maadui wa Mwenyezi Mungu na kujitoa muhanga bila kuogopa. Hili ndilo linalowapa woga maadui wa haki na sababu kubwa ya kukanusha ukweli kuhusu Imam Mahdi (as). Hii ndiyo siri kubwa ya kununua baadhi ya vibaraka na kalamu zao na kuzusha itikadi potofu kama vile Ubabi, Ubahai, Ukadiani, Uwahabi nk...

D. KAZI YA MAFAQIHI WACHAMUNGU

Kabla hajafariki, Naibu wa nne Ali bin Muhammad as-Samarry alipewa maagizo na Imam Mahdi (as) kwamba asichague yeyote kuchukua nafasi yake. Sasa wakati wa Ghayba kubwa ulikuwa umewadia. Akatoa maagizo kwamba kwa matatizo yoyote, watu warejee:

- ‘Kwa wasimulizi wa hadithi za Ahlul Bayt (as)’, yaani wale wanaopambanua baina ya hadithi sahihi na zile za uongo na dhaifu’.
- ‘Kwa wale ulamao ambao wanafamu HALALI na HARAMU kisha wakawa wamejitakasa na matamania ya nafsi na kuabudu dunia’. Hizo ndizo sifa za mujtahid anayekubalika kutoa fatwa.

Katika ghaiba kubwa Mafaqih wachamungu ambao wanajiepusha na madhambi na wanadhibiti matamano yao, ni mawakili wa Imam Mahdi (as). Ni wajibu kwa waumini kuwafuata na kuwatii.

E. KUONANA NAYE, MIUJIZA YAKE NA MSAADA WAKE

Imam yuko hai anaishi nasi bila ya sisi kumtambua. Hutokea ikawepo haja au dharura ya yeye kujidhihirisha na kutoa msaada wake. Wako watu wengi miongoni mwa ulamaa na wachamungu ambao walibahatika kukutana naye. Haya tunayoyaandika hapa na yale mengi yaliyoandikwa ndani ya vitabu ni tone katika bahari kuhusu msaada na miujiza ya Imam Mahdi (a.t.f). Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayejua wangapi katika sehemu mbalimbali za dunia hii wamepata msaada wa Imam huyu mtukufu wa zama hizi.

VISA VYA KWELI KUHUSU KUKUTANA NAYE

1. SAYYID HASHIM RASHTI:

Katika mwaka 1280 H., Sayyid Hashim Rashti aliamua kwenda kuhiji. Sayyid anasimulia kwamba walipokuwa wanapanga kwenda Tarabazun, hujaji mwingine aitwaye Haji Jabbar aliwaandea na kuwaonya kwamba mahali hapo walipo siyo salama na kwamba wahamie kwenye makundi makubwa ya watu ambayo yalikuwa yanaondoka saa mbili au tatu kabla ya swala ya alfajiri.

Walikubali ushauri wake na wakajiunga na kundi kubwa usiku uliofuatia. Hawakufika mbali, hali ya hewa ikabadilika na mvua

kubwa ya mawe ikaanza kunyesha. Sayyid anasema: “Nilijaribu kadri ya uwezo wangu niwe pamoja na marafiki zangu, lakini juhudi zangu zote hazikufanikiwa. Muda mfupi nikagundua kwamba nimeachwa peke yangu, kwa hofu nikashuka kwenye farasi na huku nimetahayari na kuduwaa.

“Nikajiuliza nitafanya nini? Baadaye, nikaamua nitafute sehemu nikae hadi kutakapopambazuka, ili wakati wa asubuhi nitafute njia nielekee mahali tulipoondokea na wenzangu. Nilianza kutembea baadaye nikamuona mtu katika bustani anaondoa barafu juu ya miti. Mtu huyo akanijia karibu yangu na akaniuliza kwa kifarsi. Wewe ni nani? Nikamweleza kuwa nimepoteana na marafiki zangu na njia hii siifahamu vizuri. Mtu huyo akaniambia niswali swala ya usiku (swalatul layl) nitaiona njia. Kwa hiyo nikafuata ushauri wake, nilipomaliza kuswali, yule mtu akaja na kuniuliza bado hujaondoka? Nikamjibu, bado sijapata njia. Akaniambia soma Ziarat Jami‘a.” Sayyid anasema pamoja na kuwa alikuwa akisoma Ziarat Jami‘a kama ada, lakini hakuwa anajua kwa moyo. Kwa usiku huo alisi-mama na kuisoma ziara Jami‘a yote kwa moyo.

Anaendelea kusimulia kwamba baada ya muda mfupi yule mtu alikuja tena akamuuliza wewe bado umekaa hapa, hujaondoka? Sayyid Rashti anaeleza kwamba alishindwa kujizuia alitokwa machozi na kulia kwa masikitiko. Akamwambia bado sijapata njia. Safari hii akamwambia asome Ziarat Ashurah. “Kama nilivyokuwa sijui Ziarat Jami‘a kwa moyo ndivyo nilikuwa sijui Ziarat Ashurah. Lakini niliweza kuisoma Ziarat yote na dua Alqamah. Yule mtu akarudi tena, akaniuliza bado uko hapa? Nikamwambia hapana nitakaa hadi patakapopambazuka.”

Yule mtu akaniambia njoo hapa nitakupeleka kwa marafiki zako. Akapanda farasi wake akaniambia nikae nyuma yake. Nika-shika hatamu ya farasi wangu na kujitahidi kumpeleka mbele, lakini

hakuondoka hata kidogo. Akachukua hatamu mikononi mwake na yule farasi akaanza kutembea. Tulipokuwa njiani yule mtu akaweka mkono wake kwenye paja langu na akaniuliza: ‘Kwa nini huwezi kuswali swala ya usiku?’ Halafu akarudia mara tatu swala ya usiku, swala ya usiku, swala ya usiku. Kwa nini huwezi kusoma Ziarat Ashurah? akarudia tena mara tatu Ashurah, Ashurah, Ashurah. Baadaye akasema: ‘Kwa nini huwezi kusoma Ziarat Jami‘a’? Kisha akarudia mara tatu Jami‘a, Jami‘a, Jami‘a. Muda mfupi baadaye akanionyesha rafiki zangu akasema angalia wanatawadha kwa ajili ya swala ya asubuhi.

Nikateremka kwenye farasi wake na nikajaribu kupanda farasi wangu lakini nikashindwa. Akanisaidia na akaelekeza kichwa cha farasi wangu kueleka kwenye mto. Nikaanza kushangaa huyu mtu ni nani na amejuaje kifarsi kwani watu walioishi hapa ni waturuki Wakristo. Nikabaki naduwaa jinsi alivyoweza kuniunganisha na watu wangu kwa muda mfupi sana. Nikageuka nyuma nikaona hayupo. Sikumuona sehemu zote nilipoangalia.

2. SHAYKH MUHAMMAD TAHIR NAJAFALI

Katika kitabu cha *Najmu Thaaqib* kuna tukio lingine lilosimuliwa kuhusu Sheikh Muhammed Tahir Najafali. Sheikh aliyekuwa anahudumia msikiti wa Kufa. Kwa miaka mingi alikuwa anaishi pale pamoja na familia yake. Alikuwa mcha Mungu sana. Baadhi ya wanafunzi wake wanasimulia tukio hili kama ifuatavyo: Miaka michache iliopita ilizuka vita baina ya makabila mawili katika mji wa Najaf. Kwa sababu ya hali hii ya vita, wanafunzi na watu waliokuwa wanatembelea Najaf walikuwa hawawezi kwenda msikiti wa Kufa. Palikuwa kimya kwa muda huo katika mji wa Najaf, mahoteli ambayo watu walijaa yalionekana matupu kwani mahujaji

hawakuhiji kwa sababu ya vita. Na hata wanafunzi hawakwenda Najaf. Kwa sababu hiyo Sheikh Mohammad Tahir Najafi akawa na wakati mgumu wa kuihudumia familia kubwa aliyokuwa nayo. Aliongeza majukumu ya kulea watoto yatima. Hali ilikuwa ngumu sana. Shaykh Tahir Najafali anasema: “Siku moja ya Ijumaa ilitokea kwamba hakuna kitu chochote cha kula. Watoto walikuwa wanalia kwa ajili ya njaa. Wakati huo nilijawa na simanzi kubwa. Nikaondoka nyumbani nikaanza kutembea huku nikimshtakia Allah kuhusu hali yangu. Nikamwambia Allah, ewe Allah nimeridhika na hali yangu na yote uliyonipa, lakini nitafanyaje kwani nataka nibarikiwe kwa kumzuru bwana wangu Imam wa Zama (a.t.f.).

“Kama ukinipa ruhusa kuona uso mtukufu wa Imam wa Zama (a.t.f.), naahidi kwamba siwezi kukuomba chochote tena na nitakuwa na furaha na nitaridhika na umaskini uliyonipa. Ghafila nikanyanyuka kutoka mahali hapo nikaona nguo nyeupe mikononi mwangu (kwa kawaida nguo hizi huchukuliwa na watu kwa ajili ya kutandikwa wakati wa swala). Mkono wangu mwingine ulikuwa umeshikwa na kijana mmoja mzuri sana. Haiba kubwa aliyokuwa nayo ilinisisimua na kunipa hisia kuwa alikuwa mfalme fulani. Akili yangu ilikuwa katika bumbuwazi na sikujua kipi kinachotokea.

“Hivyo nikamuona mtu amevaa kilemba cha kijani na amevaa nguo nyeupe amesimama karibu yangu. Tulipofika pale yule mtu aliyeshika mkono wangu akanigeukia na kuniambia, ‘Ewe Tahir, tandika nguo tusali. « Nikatandika ile nguo. Ilikuwa ni nyeupe nzuri ambayo sijapata kuiona kama hiyo. Na nilishindwa kujua ni malighafi gani iliyotengeneza kitambaa hicho. Nilipotandika kitambaa kuelekea kibla, huyu kijana mzuri Sayyid alisimama juu ya kitambaa hicho na akaanza kuswali. Nilivutiwa sana na kuwepo kwake. Taratibu nuru kutoka katika uso wake ikaongezeka sana mpaka ikawa vigumu

kuuona uso wake moja kwa moja. Na sahaba wake nao wakasimama nyuma yake, nikasimama mbele yao na kuwaangalia. Nikajiuliza hawa watu ni akina nani? Nikashangaa walipomaliza swala yao nikaona mtu aliyeswali nyuma yake hayupo tena nasi. Kabla sijapata jibu la hili nikaona kiti kimeletwa ambacho ni kama urefu wa futi 4 hivi kikiwa kimeambatanishwa na kivuli. Bwana mheshimiwa Sayyid ambaye alikuwa anaswali juu ya ile nguo nyeupe alikuwa amekalia kiti hicho. Mwanga kutoka katika kiti hicho na uso wa mtu huyo ilifanya vigumu macho kuangalia. Bwana mheshimiwa akasema: ‘Ewe Tahir unanichukulia kuwa mfalme gani?’ Nikamjibu ewe bwana wewe ni mfalme wa wafalme. Wewe unaongoza kwa elimu na sio kama wafalme wengine.

Kisha akasema: “Ewe Tahir, ombi lako limekubaliwa la kuku-tana na Imam wa Zama (a.t.f.). Sasa sema unataka nini? Je hatuangalii mahitaji yako ya kila siku? Je hatuletewi amali (matendo) yako?” Baadaye mheshimiwa Sayyid akaniahidi kwamba hali yangu itabadilika na siwezi kuwa maskini tena. Kwa wakati huohuo mtu mmoja muovu akaingia ambaye nilikuwa namfahamu kwa jina na tabia zake, akaingia msikiti wa Kufah kutokea upande wa uwanja ya Muslim (as). Mara nikaona Imam amebadilika kwa hasira. Akamwangalia yule mtu na kumwambia mpaka lini utakimbia na kujificha? Je mbingu na ardhi siyo himaya yetu? Fuata sheria ulizopewa kwani huna uchaguzi.

Kisha akanigeukia mimi akatabasamu na kusema haja zako zimetimizwa. Kisha akaniuliza kuna kitu kingine unachotaka? Uzuri wake na utukufu uliniduwaza kiasi kwamba nilishindwa kuongea chochote. Alirudia swali lake mara kwa mara nilibaki katika hali hiyo hiyo sikuweza kujibu. Sikuweza kueleza furaha niliyokuwa nayo kwa maneno. Hivyo kufumba na kufumbua nikajikuta niko peke yangu katika msikiti na Imam wa Zama ametoweka. Nikaan-

galia Mashariki tayari asubuhi imeshaingia.” Baada ya tukio hili Sheikh anasema kuwa milango ya riziki ilifunguliwa na hakupungukiwa na chochote katika maisha yake.

Ukweli ni kwamba mapenzi kwa Imam wa Zama (a.t.f.) kwa kiwango cha kutamani kukutana naye ndiyo njia ya usalama kwa dunia hii na akhera. Na kwa kukutana naye umaskini wa duniani na akhera huondoka. Kwa tukio hili Imam wa Zama (a.t.f.) ameyafafanua mambo mawili muhimu: Moja ni tuwe waangalifu wa amali zetu kwa sababu matendo yetu yanaripotiwa kwake. Imesimuliwa kwamba kama matendo yetu ni mazuri Imam (a.t.f.) anafurahi na kutuombea tupate thawabu zaidi, na iwapo matendo yetu ni mabaya Imam (a.t.f.) baada ya kuyatazama huhuzunika.

Lingine ni kwamba Imam anajua fika mambo yetu na matatizo yanayotusibu. Kwa hiyo, kwa njia ya Imam maasum matatizo yetu yanatatuliwa na tunapata baraka za hapa duniani na kesho Akhera.

3. SAYYID MUHAMMAD JABAL AMILI

Alikuwepo mtu mmoja mwema aliyeitwa Sayyid Muhammad Jabal Amili, alikuwa anasafiri katika msafara kupitia jangwani, akapotea njia.

Sayyid Amili akawatafuta wenzake aliopoteana nao lakini hakufanikiwa kuwaona. Taratibu likaingia giza la usiku. Alikuwa yupo peke yake ndani ya jangwa huku akiwa amechoka na mwenye njaa. Akiwa mwenye kukata tamaa huku akisubiri kifo chake ghafla akaona maji. Akayaendea maji akanywa na mengine akachukua udhu. Baada ya swala hakuwa na nguvu tena. Akalala chini huku akisubiri mauti yake. Muda kidogo akamuona mtu anakuja na farasi akimkaribia taratibu. Yule mtu alipofika karibu na Sayyid Amili alitoa salamu kisha akamuuliza ana matatizo gani. Sayyid Amili akamweleza kuwa amepoteana na msafara wake na ana njaa.

Yule mtu akamuuliza kwa nini hali tikiti maji na zipo karibu naye. Sayyid Amili akamwambia asifanye utani kwani ametafuta chakula sehemu zote hakupata kitu. Yule mpanda farasi akasema mimi sikudanganyi. Sayyid Amili alipoangalia karibu yake aliona tikiti maji tatu.

Yule mtu akamwambia ale tikiti mojawapo. Na matikiti mawili mengine aondoke nayo. Na akamwonyesha njia ya kufuata. Pia akamwambia Sayyid Amili kwamba karibu na magharibi atafikia hema fulani na hapo ataongozwa wapi ulipo msafara wake.

Baada ya hapo yule mtu akatoweka. Sayyid Amili akasema kwamba hapo ndipo alipotambua kwamba huyo alikuwa Imamu wa 12. Imam Muhammad al-Mahdi (a.t.f.).

Fundisho: Hata kama hatumuoni, Imam wetu wa 12 yeye anatona na tunapokuwa na shida anakuja kutusaidia.

4. WARAKA WA SIFA KWA MFUASI WA KWELI

Hii ni kuhusu aalimu mkubwa na faqihi aliyesifiwa na Imam katika mawasiliano yake naye. Imam (as) aliandika: “Amani iwe juu yako ewe rafiki mwaminifu katika dini, wewe ambaye ni msaidizi mkweli wa haki. Wewe unawaita watu katika ukweli kwa njia iliyonyooka. Amani iwe juu yako ewe rafiki mwaminifu unayepata ufunuo kutoka katika haki.”

Bila shaka maneno haya yaliandikwa na Imam (a.t.f.) kumsifu Shaykh Mufid (339 - 414 H.) (r.a). Shaykh Mufid alikuwa ni mtu mtukufu sana. Imam wa Zama (a.t.f.) alikuwa akimwandikia barua mara nyingi na kumtatulia matatizo mbali mbali ya sheria za Kiislamu. Pia alikuwa akimpa heshima kubwa bwana huyu kama histo-

ria inavyoeleza. Imam aliandika barua tatu kumtukuza mwanazuoni huyo. Barua hizo zilijaa maana na hekima na zilijaa baraka na mapenzi kutoka kwa Imam (a.t.f.).

Barua hii ni kwa ajili yako ewe ndugu muumini mpendwa na kwa rafiki aliyeongozwa sawa sawa Abu Abdullah Muhammad bin Muhammad bin Nuuman, Shaykh Mufid, ambaye ni mwakilishi mwaminifu mwenye kuongoza kwa agano la Mwenyezi Mungu.

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Amani iwe juu yako ewe bwana mtukufu ambaye imani yako imekuweka katika nafasi ya juu pamoja nasi. Namshkuru Allah ambaye hana mwenza. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuteremsha rehema Zake kwa bwana wetu Mtume Muhammad (saww) na kizazi chake kitakatifu. Mwenyezi Mungu azidi kutupa tawfiki tuusaidie na kuunga mkono ukweli. Yote utakayosimulia kutoka kwetu utapata ujira wake kwa msingi wa ukweli wake. Kwa hiyo tumepewa ruhusa kukutukuza wewe kwa kuwa na mawasiliano nawe kwa kukuandikia barua. Ni wajibu wako kupeleka ujumbe kwa wafuasi wetu.

“Namuomba Mwenyezi Mungu awapende kwa utiifu wao, awaondolee ugumu na awalinde kwa ulinzi Wake. Wale ambao wanataka kufanya urafiki wetu kuwa ni njia ya kupitia (wasila) na wanatamani kuwa karibu nasi lazima wafanye matendo mema. Wajiweke mbali na matendo tunayoyachukia na ambayo yanamuudhi Mwenyezi Mungu. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu huchukua roho za watu ghafla, na toba wakati huo haina msaada, na wala majuto hayataweza kumwoko. Mwenyezi Mungu aendeleo kukubariki kwa baraka Zake. Hii ni barua yako ewe ndugu mpendwa, mtu anayetupenda kwa ukweli na utakasifu moyoni mwake. Wewe ni msaidizi mwema, Mwenyezi Mungu asiyelala akulinde daima.”³⁴

³⁴ *Al-Ihtijaj*, Allamah Tabarsi uk. 322 na kuendelea.

- Maneno haya ya upendo yanaongeza furaha isio na kifani na yanasisimua hisia za msomaji.
- Imam ametufundisha njia sahihi ya kuishi.
- Kamwe Imam hawasahau au kuwatupa wafuasi wa babu yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
- Ulamaa wachamungu wenye kumsubiri Imam kwa dhati wana daraja yao kubwa. Mwenyezi Mungu atupe taufiki ya kufuata njia hii.

BAADHI YA MIUJIZA

1. AZALIWA KUTOKANA NA MAOMBI YA IMAM WA ZAMA (A.T.F.).

Hili ni tukio lililotokea katika karne ya nne linamhusu mmoja katika wanazuoni wakubwa wa Kishia aliyetunukiwa jina la Muallim (Mwalimu). Kitabu chake '*Man la Yahdhuruhul Faqih*' ni moja katika vitabu vinne vya hadith vinavyotegemewa na Shia. Ni kitabu cha kutegemewa ambacho maulamaa wa Kishia wanakitumia kwa marejeo. Kupata daraja ya juu kwa Sheikh Suduq aliyefariki 381H., kunaweza kutathminiwa na ukweli kwamba alizaliwa kutokana na dua ya Imam wa Zama (a.t.f.), uhai wetu uwe fidia yake. Maisha yake yote alikuwa ni kituo cha msaada na baraka za Imam (a.t.f.).

Tukio lenyewe ni kama lifuatalo:

Baba yake Shaykh Saduq (r.a) alikuwa akijulikana kwa jina la Ally bin Babawayh. Alikuwa ni mmoja katika mafaqih maarufu na mwanazuoni mkubwa wa hadith katika mji wa Qum. Alikuwa amemuoa binamu yake, na kwa miaka mingi walikuwa hawajabarikiwa kupata watoto.

Mnamo mwaka 305 AH, alitembelea Baghdad na akakutana na mwakilishi maalum wa Imam (a.t.f.) akiitwa Husayn bin Ruh Nawbakhti (r.a.). Bin Babawayh akatuma barua kupitia kwa Muhammad bin Aswad kumuomba aipeleke kwa Imam wa Zama (a.t.f.) amuombe kwa Mwenyezi Mungu ili apate mtoto. Majibu yalijibiwa mara moja kutoka kwa Imam kama ifuatavyo: ‘Huwezi kupata mtoto kwa mke huyu uliye naye. Nimeshakuombea kufuatana na maombi yako karibuni Allah atakujalia kupata watoto pacha wa ki-ume ambao watakuwa wanasheria, kutoka kwa mwanamke wa kabila la Kidaylami.’ Kama alivyoambiwa na Imam wa Zama (a.t.f.), Ibn Babawayh alimuoa mwanamke wa kabila hilo na akamjalia kupata watoto wawili pacha. Mmoja akamwita jina la Muhammad na mwingine akampa jina la Husayn. Wote watoto wake wakawa ulamaa wakubwa wa Kishia katika mji wa Qum. Ni ulamaa wachache wa wakati huo waliofikia daraja ya juu kama yao.

Uwezo wa kipekee aliokuwa nao na akili ya kusimulia na kuhifadhi hadithi na uaminifu aliokuwa nao ulimwezesha kupata jina la Saduq. Baadaye akajulikana sana na kuwa mashuhuri kwa jina hili la heshima. Ulamaa wa zama zake, wanafunzi na marafiki zake walis- hangazwa sana na elimu yake, uwezo wake wa kumbukumbu yenye uhakika. Huu ni uthibitisho kwamba akili yake na mafanikio yake makubwa yasiyo na mwisho aliyapata kutokana na kubarikiwa na Imam wa Zama (a.t.f.). Mwenyewe aliukubali ukweli huu na kujihisi mwenye heshima kubwa kwa Baraka hiyo. Mara nyingi Shaykh Saduq alikuwa akisema: ‘Nimezaliwa kwa Baraka ya dua ya Imam wa Zama (a.t.f.).’

2. SHAYKH SADUQ NA KITABU CHAKE 'KAMALUDDIN WA ITMAAM NI'MAH.'

SABABU ILIOMFANYA KUANDIKA KITABU HICHO:

Nilipata heshima kubwa ya kuzuru kaburi la Imam Abul Hasan Ridha (as) na nilipokuwa narudi nyumbani, nilipumzika katika mji wa Nishapur kwa siku chache. Mashia wengi wakanitembelea, kwa ajili ya majadiliano. Kwa bahati mbaya walikuwa na mtizamo wa shaka juu ya Imam. Nilijaribu kadri nilivyoweza kujadiliana nao na kuwaongoza katika njia sahihi. Niliwaita na kuwaeleza hadithi za uhakika na ukweli za Mtume (saww) na kizazi chake kitukufu kili-chotoharishwa.

Siku moja nilikuwa natafakari jinsi nilivyoishi maisha mazuri katika mji wangu wa Rayy pamoja na familia yangu. Ghafla nika-pata usingizi, nikaota ninaizunguka Kaaba. Nilipoizunguka mara ya saba nikalifikia jiwe jeusi (*Hajar al Aswad*), nikalibusu na kusema: 'Hii ni amana ninayoisalimisha na ahadi ninayoitekeleza kikamilifu ili utoe ushahidi wa utii wangu.' (dua inasomwa kwenye jiwe jeusi na mahujaji). Wakati huo huo nikamuona bwana wangu Sahibuz Zaman (a.t.f.) amesimama kwenye mlango wa Kaaba. Nikamsogelea huku nina majonzi na simanzi. Imam kwa kuangalia uso wangu akajua nina hisia gani. Nikamsalimia naye akanijibu kisha akaniuliza: "Kwa nini huandiki kitabu kuhusu ghaiba, ili uondokane na simanzi na majonzi?" Nikamjibu: Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimekwisha kusanya baadhi ya habari zinazohusu ghaiba. Hapo akaniambia: "Sivyo hivyo ninavyotaka kiandikwe. Nataka uandike kitabu kinachofahamisha kwa upana ghaiba na ndani ya kitabu hicho

andika ghaiba ya Mitume wa Allah.” Baada ya kusema haya Imam akatoweka.

Nilipoamka asubuhi nikatumia muda wangu wote kuandika tangu asubuhi hadi jioni. Nikafuata maelekezo yake kama alivyo-niagiza. Nikaendelea kumuomba Allah anisaidie, pia anisamehe madhambi yangu.³⁵

Tukio hili linatufundisha kuwa:

- Tukiwa na matatizo tutafute msaada wake Imam (a.t.f.) atusaidie.
- Tujitahidi kuwafahamisha watu kuhusu Imam Mahdi (a.t.f.).
- Tunatakiwa kadri iwezekanavyo kuondoa shaka na wasiwasi kuhusu Imam katika fikra za watu.

3. IMAM WA ZAMA AKAMILISHA KITABU

Allama Hilli (648 - 726 H.) (r.a.) ni mmoja katika ulaamaa mashuhuri katika ulimwengu wa Kishia. Zama zake, alikuwa hana mfano, na pia alikuwa mwandishi hodari. Ni mtu muhimu aliyebarikiwa tuzo maalum na Imam wa Zama (a.t.f.)³⁶. Mojawapo ya tukio la kipekee zama za Allamah Hilli ni kwamba mtu mmoja aliandika kitabu ambacho kilikuwa dhidi ya ushia na alikuwa akikitumia na kukinukuu katika hadhara za watu na akafanikiwa kuwapotosha watu wachache, hivyo watu wakatilia shaka uongozi wa Uimamu. Lakini haku-muazima mtu yeyote kitabu hicho kwa kuhofia kwamba watakipata Mashia na watajibu na kupinga hoja zake.

³⁵ Sheikh Sadduuq.Utangulizi wa kitabu *Kamaluddin*.

³⁶ Kutoka *Majalisul Muminiin* ya Shahiid Salis Qazi Nurullah Shustari

Allamah Hilli akaanza kuhudhuria mikutano ya huyu mtu. Na akajitambulisha kuwa ni mwanafunzi wa huyu mtu. Baada ya kuku-balika na mwalimu akamuomba amwazime kitabu kwa muda. Ilikuwa vigumu kwa yule mtu kukataa kumwazima kitabu. Yule mtu alimweleza kwamba alikuwa ameahidi kutompa yeyote kitabu hicho zaidi ya usiku mmoja. Allamah Hilli akakubali kuazima kitabu kwa usiku mmoja kwani alikuwa hana budi, ilikuwa hamna njia nyingine. Usiku huo alianza mara moja kukopi hicho kitabu akidhamiria kuchukua kwa wingi kadri iwezekanayo na hivyo kumwezesha kukanusha hoja zilizomo. Ilipofika usiku wa manane hakuweza kustahamili usingizi. Wakati huo huo mgeni mmoja wa heshima aliwasili, baada ya kusalimiana kwa furaha akamwambia Allamah Hilli aende kulala kwani yeye huyo mgeni atakamilisha kitabu. Allamah akakubali bila kuuliza chochote. Baada ya muda alipoamka, hakuona alama ya kuwepo mgeni yule. Baada ya kukikagua kitabu akakuta kitabu chote tayari kimeandikwa na yule mgeni wake. Mwishoni mwa kitabu maandishi ya ziada yalikuwa yameongezwa. Alipoangalia kwa karibu akakuta maneno yafuatayo: “Imeandikwa na Imam Hujjah.”³⁷

4. MTOTO WANGU MAHDI YUPO NDANI YA MSIKITI WA KUFA

Mwanazuoni mkubwa Muqaddas Ardebeli (alifariki 993 A.H.) ni miongoni mwa watu watukufu waliopata hadhi ya kukutana na Imam (a.t.f.) na kutatuliwa matatizo yake. Alikuwa anajulikana sana kwa uchamungu wake kiasi kwamba ilikuwa ni vigumu kupata mfano wake. Ni maarufu kwamba pindi alipokuwa akikabiliwa na maswali magumu alikuwa akienda kwenye kaburi la Amirul Mumi-

³⁷ *Rawzatul Jannat*, Juz. 2, uk. 282, *Jannatul maawa* tukio na. 22, *Najmas Thaaqib* tukio na. 15.

niin Ali (as) ili kutafuta jawabu la matatizo hayo. Imam Ali (as) alikuwa akimpa majibu ya maswali hayo. Alikuwa amefikia daraja la uthabiti wa imani, kwa sababu ya uchamungu wake kiasi cha kuweza kuwasiliana na Imam. Mmoja wa wanafunzi wake ambaye pia ni mwanazuoni mkubwa alikuwa anajua uwezo wa mwalimu wake. Aliandika tukio hili ambalo ni mashuhuri katika vitabu vingi vya Rijali³⁸ ambavyo vina maelezo kuhusu Muqaddas Ardebeli:

“Siku moja nilikuwa nimechoka baada ya kusoma kwa muda mrefu kwa hiyo nikazuru viwanja vya kaburi la Amirul Muminiin Ali (as) ili kujipumzisha. Mara niliona kivuli kinasogelea kaburi ilhali ya kuwa milango ya jengo ilikuwa imefungwa. Nilikuwa na shauku ya kujua kinachoendelea, kwa hivyo nikafuata hicho kivuli. Pindi kilipofika kwenye kaburi kiligusa kwa mkono wake milango ikafunguka yenyewe na ikabaki wazi. Alisimama karibu na kaburi la Imam Ali (as) na akatoa salamu kisha nikasikia akijibiwa salamu yake. Hapo wakaanza kuongea katika sauti ile ile. Baada ya muda kivuli hicho kilitoka na kuelekea mjini Kufa. Nilimfuatilia mtu huyo na kumuona anaingia ndani ya msikiti wa Kufa. Hapo akaelekea ilipo mihrabu na akaanza kuongea na mtu mmoja. Mazungumzo yalipokamilika alitoka na kuelekea mjini, wakati huo mwanga wa asubuhi ukaanza kuenea na watu walianza kujitayarisha kwa swala ya asubuhi. Niliendelea kumfuata yule mtu kimyakimya lakini mara sikuweza kujizuia kupiga chafya. Yule mtu alistuka na kuangalia nyuma na akanitazama. Nilimuona kuwa ni mwalimu wangu Ayatullah Muqaddas Ardebeli. Nikamsalimia na nikamjulisha ya kwamba nilikuwa namfuata usiku mzima tangu alipokuwa kwenye kaburi la Amirul Muminiin (as). Nilimsihi anieleze alikuwa anaongea na nani ndani ya msikiti mtakatifu wa Kufa. Mwalimu Muqaddas Ardebeli akanitaka nimuahidi kuwa sitafichua siri katika uhai wake. Kisha akaniambia: ‘Mwanangu wakati mwingine matatizo ambayo siwe-

³⁸ Vitabu vinaelezea wapokezi wa hadithi na maisha yao.

zi kuyatatua nayapeleka kwa Amirul Muuminin Ali bin Abi Talib (as) na kupata jawabu. Amirul Muuminin akaniambia: “Mwanangu Mahdi yupo ndani ya msikiti wa Kufa. Ni Imam wa zama zako. Nenda kwake atakupata majibu ya maswali yako.” Kwa hiyo nikaelekea katika msikiti wa Kufa nikamkuta Imam Mahdi (a.t.f.) amesimama juu ya mimbari nikamuuliza maswali na nikapata majibu yake.³⁹

5. ZAWADI YA IMAM WA ZAMA HIZI

Allamah Muhammad Taqi Majlisi (r.a), (1594 - 1659 M.), alikuwa ni mwanazuoni mwenye maadili mema na mchamungu kweli kweli. Yeye ndiye baba yake Mulla Muhammad Baqir Majlisi (Allamah Majlisi), (r.a), (1627 - 1698 M.) ambaye alikuwa mwanazuoni mkubwa wa Mashia zama zake. Alitumia uhai wake wote kukusanya na kuelezea hadithi za watu wa Nyumba ya Mtume (Ahlulbayt) (as), waliotakaswa. Mtoto huyu mtukufu anaandika kuhusu baba yake kwamba: “Mbali na Ahlul Bayt mtu mwingine aliyenisaidia kufikia daraja hii ni mpendwa baba yangu...”

Muhammad Taqi Majlisi, akieleza ndoto zake za kweli, anaandika kuhusu ukarimu wa Imam wa Zama (a.t.f.)⁴⁰:

“Kwa kuwa sikuhitaji chochote katika ulimwengu huu isipokuwa radhi ya Imam wa Zama (a.t.f.) na sikupata amani ila kwa kumkumbuka, Imam alinikaribisha na kujibu maswali yangu magumu ya elimu ambayo yalinitatiza. Imam aliniamuru niwe thabiti katika Swala ya Usiku. Nilipomwomba anipe ushauri ni kitabu gani niwe nasoma mara kwa mara, alinionyesha kitabu cha Sahifa as-Sajadiya na akaniambia kwamba kipo mahali fulani kwa mtu fulani na

³⁹ Kutoka katika kitabu “*Those who were succesful in the search of Qaim (a.s.)*.” uk. 27, 30).

⁴⁰ *Sharh Man la yahdhuruhul faqih*, kitabu cha nne, ndani ya maisha ya Mutawakkil bin Umair msimulizi wa Sahifatu Sajadiya, kuhusu ukarimu wa Imam wa Zama (a.t.f.)

akaniambia ameacha nakala yangu, ni zawadi kutoka kwake, hivyo niende kuichukua. Katika ndoto hiyo nikaona naenda kuchukua kitabu hicho. Baadaye nilipoamka nikaenda kwenye nyumba kama nilivyoelekezwa katika ndoto na nikapata nakala ya kitabu ambacho niliachiwa na Imam (as).” Daima alikuwa akimkumbuka Imam (a.t.f.) na akilia sana kwa mapenzi yake.

Baada ya tukio hili, alimkurubia sana Mwenyezi Mungu kwa kusoma mara kwa mara dua zilizomo katika kitabu hicho. Alijita-hidi daima kutangaza nakala hii ya Sahifa as-Sajadiyyah kama jua linavyong’aa na kutoa nuru ya njia sahihi kwa wasafiri. Hii ilikuwa kwa ajili ya muujiza na fadhila ya Imam wa Zama na baraka ya kitabu alichopewa zawadi.

Tunapata mafunzo yafuatayo kwa wapenzi wenye shauku na Imam wa Zama:

- Katika wakati wa usiku mshtakie Allah matatizo yako. Swali swala ya usiku.
- Tunatakiwa tuangalie kwa makini dua za Sahifa as-Sajadiyya kwa sababu ni maneno halisi ya Imam Sajjad (as).
- Tunatakiwa tuwe na matumaini ya kupata msaada wa Imam Mahdi (atf).

6. DAWA IPONYAYO

Sheikh Hurr al-Amili (1033 - 1104 H.) ndiye mkusanyaji wa kitabu cha hadithi ‘*Wasailush Shia*’. Alikuwa mwanazuoni mkubwa wa sheria aliyekuwa na taathira juu ya ulamaa wa zama zake na wa baadaye. Alisimulia muujiza wa Imam wa Zama (as) kuhusu mtu mmoja akiitwa Sulayman aliyepewa dawa na Imam wa Zama.

Anasimulia: “Nilipokuwa na umri wa miaka 10 nilikuwa mgonjwa sana mahtuti hadi ndugu zangu walikata tamaa wakajua kwamba sitapona. Kila mmoja alinikumbatia huku akitoa machozi wakiwa wamejiandaa kifikra kwamba usiku huo ndio utakuwa mwisho wangu. Usiku ule katika ndoto zangu nilimuona Mtume Muhammad (saww) na Maimamu, nikawatolea salaam na nikapeana mikono na kila mmoja wao. Nilipomfikia Imam Ja’far Sadiq (as) tukabadilishana maneno. Sikukumbuka chochote tulichoongea naye isipokuwa nakumbuka aliniombea dua kwa Allah. Nilipomfikia Imam wa Zama (as), nikatoa kilio changu kwake huku nikimwambia kuwa nitakufa kwa haya maradhi kabla sijafikia lengo langu katika elimu na ucha Mungu. Imam (as) akanijibu: ‘Usiwe na hofu huwezi kufa kwa maradhi haya. Allah atakuponya maradhi haya na atakupa maisha marefu.’ Kisha akanipa bakuli alilokuwa ameshika, ndani yake mlikuwa mna dawa. Nikanywa na mara moja nikapona kabisa. Ndugu zangu walipatwa na mshangao mkubwa kwani nilipona kabisa.”⁴¹

7. SAUTI YA IMAM WA ZAMA (A.T.F.)

Allamah Bahrul Uluum (r.a) (1155 - 1212 H.) ni mmoja kati ya wazuoni aliyepata msaada wa Imam (as). Alikutana na kuongea naye zaidi ya mara moja. Wazuoni wote walimtukuza kwa uchamungu na walimkubali kwa ubora wa elimu aliyokuwa nayo. Ulama wamesimulia mafanikio yake katika maandishi. Muhaddith Qummi alinukuu katika kitabu chake ‘*Rijal*’ matukio manane ambapo Bahrul Uluum alikutana na Imam wa Zama (a.t.f.s). Hapa tunanukuu tukio mojawapo ambapo Imam (a.t.f.) alimkalisha karibu naye na akazungumza naye kwa siri.⁴² Ni daraja gani kubwa ya uchamungu aliofikia mfuasi huyu wa *Wilayah* mpaka Imam wa Zama (as) akamkumbatia!

⁴¹ *Najmus Thaqib* tukio na. 61, *Jannatul Maawa* tukio na. 3-8)

⁴² *Fawaidu Ridhawia* uk. 679

Siku moja watu walimuona Allamah Bahrul Uluum katika hali isiyo ya kawaida. Amesimama karibu na kaburi ya Imam Ali (as) badala ya kusoma Ziyara kwa hali ya uchangamfu, macho yake yalijaa machozi aliposoma mistari ifuatayo: “*Ni furaha ilioje kusikia kisomo cha Qur’ani katika sauti yako nzuri.*” Baadaye alipoulizwa ni kitu gani kimemsibu, alijibu: “Nilipokuwa karibu kuingia maeneo matukufu ya Amirul Muuminiin (as) nilimuona Imam wa Zama (as) amekaa kwenye kaburi la Imam Ali (as) huku akiwa anasoma Qurani kwa makini sana. Nilipoona hivyo nikawa narudia yale aliyokuwa akitamka. Lakini nilipoingia ndani ya *dharah* (sehemu alipozikwa), Imam alikuwa amemaliza kusoma na kuondoka...”⁴³

Wakati Allamah alipokuwa anaishi Makka alikuwa mbali na ndugu zake na wafuasi wake. Lakini pamoja na hayo alijipa moyo na hakuacha kuwatekelezea wanafunzi wake na maskini haja zao. Siku moja msaidizi wake akamwambia kwamba pesa zote zimekwisha na hakuna kilichobakia. Ilibidi sasa afikirie sana juu ya jambo hili. Hebu tupate maelezo kutoka kwa msaidizi wake mwenyewe:

“Sayyid hakujibu jambo lolote. Ilikuwa ni kawaida yake asubuhi kufanya tawafu na baadaye kurejea chumbani kwake peke yake. Nilikuwa nikimtarishia *hookah* na akivuta kila siku. Baada ya hapo alikuwa akienda chumba kingine ambapo alikuwa akiwafunza wanafunzi. Katika siku hiyo Sayyid akasikia sauti kutoka nje. Nikamuona ni mwenye wasiwasi. Akaniambia nifiche *hookah* wakati akijitayarisha kama mtumishi mnyenyekevu. Akaenda Kwa haraka kufungua mlango. Mwarabu mmoja mwenye haiba na sharafu akaingia na kwenda chumbani kwa Sayyid na kuketi. Sayyid akamfuata na kuketi karibu naye kwa unyenyekevu. Wakaongea karibu saa nzima baadaye mwadhama huyu akaaga na kuondoka. Sayyid akamsindikiza hadi mlangoni akambusu mikono yake na kumsaidia

⁴³ *Najmus Thaqib* tukio na. 29, *Jannatul Maawa* tukio na.45)

kupanda ngamia wake. Mgeni akaondoka na Sayyid akarudi lakini rangi ya uso wake ikabadilika. Akanipa waraka wa ahadi (ya kulip-wa pesa) aliokuwa nao mkononi kisha akaniambia chukua waraka huu mpelekee mwenye duka fulani pale kwenye mlima wa Safa. Yeye ni mbadilishaji pesa, kwa hiyo chukua chochote atakachokupa mbadala wa waraka huu.

“Nilimpelekea mbadilishaji waraka huo. Aliuchukua na kuubusu kwa heshima na taadhima kisha akaniomba nilete makuli (wabebe mizigo). Nikaleta makuli wanne ambao aliwapakia mifuko ya pesa kiasi walichoweza kubeba na tukarejea nyumbani. Siku moja nikaamua kwenda kuchunguza sehemu ile tulipochukua pesa na kuchunguza kuhusu aliyetoa ule waraka lakini sikukuta duka lolote sehemu ile. Nilimkuta mtu maeneo yale nikamuuliza habari ya mbadilishaji pesa. Akanijibu kuwa hajawahi kuwepo mtu kama huyo hapo. Kisha nikatambua kwamba hii ni miongoni mwa siri takatifu na yote ilikuwa ni kwa sababu ya msaada wa Imam wa Zama (a.t.f.).”⁴⁴

Huyu mwanazuoni mkubwa aliyejitakasa na mchamungu alifanikiwa kuondosha pazia baina yake na Imam (as). Alikuwa yupo karibu sana na Imam kiasi kwamba alionekana kama anaishi pamoja naye. Hivi ndivyo Imam wa Zama (a.t.f.) anavyoonyesha mapenzi yake kwa watu wanaoepukana na ubinafsi na tamaa. Wakati mwingine Allamah alikuwa na uwezo wa kusikia dua zinazosomwa na Imam wa Zama (a.t.f.) zinazotoka katika midomo iliyobarikiwa ya Imam. Pia alifanikiwa kupata sharafu ya kukutana na Imam (a.t.f.) kwenye ghala ambapo hakuwepo hata mtu mmoja karibu. Amani iwe juu yake msaidizi mheshimiwa wa Imam (a.t.f.).

⁴⁴ *Najmus Thaaqib* tukio na.76, *Jannatul Maawa* tukio na.12, *Fawaidur Ridhawia* uk. 280).

8. KUOMBA RUHUSA KUIINGIA

Shaykh Murtaza Ansari (r.a), (1214 - 1281 H.) ni mwanazuoni mashuhuri sana katika ulimwengu wa Kishia na kutizamwa kama muhuri wa mafaqih. Alikuwa ni katika kizazi cha swahaba mtukufu wa Mtume (saww), Jabir bin Abdullahi Ansari. Allamah Muhaddith Nuriy anaandika hivi kuhusu mwanazuoni huyo: “Mwenyezi Mungu alimjalia Jabir ambaye katika kizazi chake alitokeza mtu mchamungu, mwenye elimu na mtukufu, aliyetumikia umma kwa elimu yake, utafiti, uchamungu na ibada yake.

Alikuwa kiongozi mkubwa wa Kishia kwa wakati wake na alikuwa naibu mtiifu wa Imam (a.t.f.). Alimpenda sana Imam (a.t.f.). Kamwe fikra zake na malengo yake hayakuwa mbali na Imam (a.t.f.). Mmoja wa wanafunzi wake anasimulia kuwa siku moja usiku alipokuwa Karbala, bwana huyu alitoka nyumbani kwake huku amechukua taa kwa sababu ilikuwa giza sana. Mitaa ilikuwa imejaa matope. Kwa mbali nikamuona mtu anakuja, na nilipomsogelea nikamuona ni mwalimu wangu, Shaykh Ansari (r.a). Nilipata wasiwasi na kujiuliza sana kumwona usiku kama huu katika mitaa michafu na huku macho yake yalikuwa hayaoni vizuri. Sikuweza kukisia wapi anakwenda, lakini nilimfuata ili kumnusuru ikiwa litatokea jambo. Baada ya kutembea kitambo akafika mahali kuna mlango. Akasimama mlangoni akasoma Ziyarat Jamiah kwa heshima kubwa kisha akaingia ndani. Baada ya hapo sikuona kitu tena.

Hata hivyo nilisikia sauti ya Shaykh kama anaongea na mtu. Baada ya saa moja nilipoingia katika haramu ya Imam Husayn (as) nikamuona Shaykh pia yupo pale. Baada ya siku chache nikakutana naye. Nikajaribu kumuuliza yale niliyoyaona usiku ule. Baada ya kung’ang’ania sana kumuuliza akanijibu: ‘Wakati mwingine huwa ninaomba ruhusa kuwa pamoja na Imam (as). Kwa hiyo nakwenda

kwenye nyumba maalum (ambayo huwezi kuipata) na kusoma Ziyarat Jamiah. Ninapopata ruhusa mara ya pili ninakutana na Imam wa Zama (a.t.f.), na hapo ninamuuliza maswali muhimu yanayoni-tatiza na kumuomba msaada wake...’ Sheikh akanitaka nitoe ahadi kwamba sitatoa siri hii kwa yeyote katika kipindi cha uhai wake. Bila shaka moyo wa huruma na mapenzi ya Imam (a.t.f.) kwa wa-saidizi wake ni makubwa. Wao ni mawakili wake. Imam wa Zama (a.t.f.) wakati wote anawasikiliza na kuwasaidia pindi unapohitajika msaada wake.”⁴⁵

Lazima tukumbuke kwamba Imam wa Zama (a.t.f.) hawasaidi tu wasaidizi wake na mawakala wake lakini pia anasaidia watu wa kawaida kama sisi ikiwa tutashikamana na watu watakatifu wa Nyumba ya Mtume (Ahlul Bayt) na kuwapenda bila kipingamizi. Tunatakiwa tuwe na imani thabiti kwamba ikiwa tutaendelea kupita katika hatua za kumsaidia Imamu na kumfuata, basi naye hatofanya ajizi kutusaidia sisi...


9. WATU WA BAHRAIN WAOKOKA NA HILA ZA MANASIBIY⁴⁶

Bahrain ni kisiwa kidogo (707 km²) chenye wakazi wapatao laki saba, asilimia themanini wakiwa ni Mashia. Bahrain imekuwa chini ya uangalizi wa Waingereza toka mwaka 1861 hadi 1971 walipopata uhuru.

Pindi kisiwa hiki kilipokuwa chini ya utawala wa wazungu, walimuweka Gavana Mwislamu ambaye alikuwa Nasiby (mtu mwenye uadui na Ahlul Bayt na mashia wao).

⁴⁵ *Murtadha Ansari* uk. 105-107

⁴⁶ Naswiby: Ni mtu yeyote ambaye anayefanya uadui dhidi ya Ahlul Bayt (a.s.) au wafuasi wao (mashia)v



Waziri wake alikuwa na uadui zaidi. Kwa hivyo alikuwa anapanga kila hila ili kuwaangamiza Mashia. Siku moja Waziri huyu akaingia kwa Gavana na huku akiwa na komamanga mkononi. Juu yake limeandikwa *‘Hakuna Mungu ila Allah, Muhammad ni Mtume wake, Abubakr; Umar, Uthman na Ali ni Makhalifa wake.’*

Gavana akalichunguza lile komamanga vizuri na kuona kwamba maandishi hayo si ya kuchorwa bali ni ya asili (tunda limeumbika hivyo). Gavana akastaajabu sana na kumwambia waziri wake: ‘Huu ni muujiza na hoja ya nguvu dhidi ya madhehebu ya marafidha (mashia), unaonaje kuhusu watu wa Bahrain?’ Waziri akamjibu kwamba watu wa Bahrain ni wakereketwa wa madhehebu yao na hawakubali hoja. Kwa hiyo waite na uwaonyeshe komamanga hii, ikiwa watakubali na kurejea kwenye madhehebu yetu basi itakuwa ni thawabu juu yako. Na ama ikiwa watakataa na kushikilia upotofu wao, basi wape khiari tatu: Ima walipe jizya (kama vile wasio Waislamu), au walete jawabu la muujiza huu au uwaue wanaume wao na kuwachukua mateka wanawake na watoto wao na kuchukua ngawira.

Gavana akaipenda rai hiyo na akawaita ulamaa, masharifu wachamungu wa Bahrain na kuwaonyesha komamanga hilo. Baada ya kuwaonyesha aliwataka walete jawabu, vinginevyo watafikwa na balaa la kuuliwa, kutekwa watoto na wanawake, kuchukuliwa mali zao na kulipa jizya kama vile makafiri. Watu walitahayari na nyoyo zao zilijaa woga kwa balaa hii iliyoteremka kuwaangamiza. Wakuu wao waliomba wapewe muda wa siku tatu ili walete jawabu au wakishindwa wahukumiwe.

Baada ya kutoka hapo walikaa kikao na kuamua wachague miongoni mwa wachamungu wa Bahrain watu kumi walio bora na baada ya hapo wakawachuja na kupata watatu. Wakamtaka wa kwanza aende jangwani na kumwabudu Mwenyezi Mungu na kumtaka msaada Imam (a.t.f.). Usiku wote alisimama kwa ibada na dua kwa unyenyekevu na kulia. Hadi alfajiri hakuona chochote. Alirejea, na wa pili wao akatoka kama wa kwanza na kujitahidi kuomba na kutawasali kwa Imam wa Zama. Lakini naye alirejea bila habari yoyote. Hili liliwazidishia wasiwasi na kutahayari. Wa tatu wao, Muhammad bin Isa akaletwa. Akatoka usiku huo wa tatu, pekupeku na kuelekea jangwani. Ulikuwa usiku wa giza, akamuomba Mwenyezi Mungu na kulia sana awaokoe na balaa linalowakabili. Akamtaka Imam wa Zama (a.t.f.) msaada. Ukiwa usiku unakaribia kumalizika, mara akasikia mtu anazungumza na kusema: “Ewe Muhammad bin Isa kuna nini nakuona katika hali kama hii na kwa nini umetoka nakuja hapa jangwani?” Akamjibu: “Ewe bwana, niache kwani nime-toka kwa ajili ya jambo la hatari na janga kubwa siwezi kulisimulia ila kwa Imam wangu na wala simshitakii ila yule anayeweza kutuondolea hilo.” (huyo mtu) Akamwambia: “Ewe Muhammad bin Isa, mimi ndiye Swahibul Amri, elezea haja yako.” Akamjibu: “Ikiwa wewe ndiye basi waelewa fika kisa changu na wala huhitaji mimi kukushehereshea.”

Mtu huyo akasema: “Naam, tatizo lenu ni fitna ya lile komamanga na vitisho vya gavana.” Niliposikia hayo nilimwelekea na kusema: “Naam, ewe bwana wangu, wajua yaliyotusibu na wewe ndiye Imam wetu na mlinzi wetu na muweza wa kutuhami.”

Imam akasema: “Ewe Muhammad bin Isa, huyo waziri (laana iwe juu yake) nyumbani kwake ana mkomamanga (mti). Pindi ulipoanza kuzaa, alichukua udongo na kutengeneza umbo la komamanga kisha akaukata vipande viwili na kuandika maneno hayo na baadaye akavisha tunda ndogo ambalo liliathirika na maadishi hayo kadri linavyokuwa. Kwa hiyo kesho mtakapokwenda kwa gavana, mwambie nimekuja na jawabu lakini sitoeleza chochote ila nikiwa ndani ya nyumba ya waziri. Mtakapokwenda nyumbani kwake, angalia kuliani kuna chumba, mwambie gavana kwamba hutompa jibu ila katika chumba hicho. Waziri atakataa hilo, lakini shikilia na usikubali akutangulie. Utakapoingia utaona mfuko mweupe kwenye chanja, panda uchukue na ndani yake utakuta ule udongo aliyotumia. Muonyeshe gavana ili ashuhudie. Pia ewe Muhammad bin Isa, mwambie gavana kwamba tuna muujiza mwingine nao ni kwamba tunda hili la komamanga ndani yake hamna chochote ila jivu na moshi. Ukitaka ukweli muamuru waziri alikate.”

Muhammad bin Isa baada ya kupata ufumbuzi huo alibusu mkono ya Imam na kurejea na bishara njema na furaha isiyo na kifani. Asubuhi walielekea kwa Gavana na Muhammad bin Isa alifanya vile alivyoelekezwa na Imam (a.t.f.). Kila kitu kilikuwa kama alivyoosema. Gavana alistaajabu na kutaka kujua nani alimpa taarifa hizo. Muhammad akamwambia kwamba ni Imam wa Zama na Imam wa kumi na mbili. Akamtajia Maimamu wote. Gavana alipopata maelezo yote hayo alimwambia anyooshe mkono wake na hapo akatamka: “Nashuhudia ya kwamba hakuna Mungu ila Allah na Muhammad ni mja wake na Mtume wake na kwamba Khalifa baada yake

bila mwanya ni Amiri wa Waumini Ali na baada yake ni Maimamu wa Ahlul Bayt.” Baada ya hapo aliamuru Waziri wake auliwe na akawaomba msamaha watu wa Baharain na akawatendea mema. - Kisa hiki ni mashuhuri kwa watu wa Bahrain. Kaburi la Muhammad bin Isa ni maarufu kwao.

10. ABU RAAJIH AL HIMAAMIY⁴⁷

Katika mji wa Hillah, Abu Raajih al Himaamiy alikuwa miongoni mwa Mashia wachamungu wapenzi wa Ahlul Bayt (as) walioshi-kamana na Imam wa Zama (a.t.f.). Mtwala wa Hillah alikuwa aki-itwa Marjaan al-Swagir. Walimletea shitaka kwamba Abu Raajih al Himaamiy anatukana Masahaba. Kwa sababu ya hilo, huyu aligha-dhibika na kuamuru ashikwe, apigwe kisha auliwe. Kwa hiyo Abu Raajih alipigwa mpaka meno yake yote yakatoka na akapata ma-jeraha mwili mzima. Ulimi wake ukatolewa na kutiwa sindano ya chuma. Hayo hayakutosha bali aliamrisha wamtoboe pua yake na wakaingiza kamba ndani yake na wakamburuza mahututi mitaani na sokoni hadi alipokuwa anazirai, yule mtawala akaamuru wamuue. Watu waliokusanyika wakasema huyu maskini sasa anakata roho, hakuna haja ya kusumbuka mwacheni afe mwenyewe. Wakamwa-cha na kusuburi. Jamaa zake wakaja na kuchukua kiwiliwili chake nyumbani.

Asubuhi ilipowadia, watu walipigwa na butwaa kwa kumuona Abu Raajih amekaa juu ya msala buheri wa afya akishughulika na uradi baada ya swala. Watu wakakusanyika kushuhudia maajabu hayo; mwili wake ulikuwa hauna jeraha hata moja, meno yake ya-likuwa kamili, na zaidi ya hayo alikuwa amependeza, amenawiri kama kijana. Akawaeleza kwamba usiku uliopita alitaka kumuomba

⁴⁷ Al Hairiy, Ali Y.: *Ilzaamun Naaswibi fii Ithbaatil Hujjatil Ghaaib*, Juz. 2, hekaya ya 3, uk. 11

msaada Imam wa Zama (as) lakini akaona hana ulimi. Kwa hiyo kwa moyo wenye majonzi makubwa alimuelekea Imam (a.t.f.) na hapo akahisi kwamba mahala hapo pamenawirika. Imam alifika na kunigusa mwili mzima na kuniponya. Abu Raajih alikuwa pia na ugonjwa wa ndui, lakini baada ya tukio hili alibadilika na kuwa mzuri kiasi kwamba watu wa Hillah walikuwa hawakatiki kuja kumuona.

Mtawala alipopata habari aliogopa, alitahayari na kutetemeka. Alitubia na kuanzia hapo akawa anakaa akielekea Maqaam ya Mahdi (a.t.f.)⁴⁸ kwa unyenyekevu na kuwafanyia watu wa Hillah mema. Lakini hilo halikusaidia kwani hakuchukua muda alikufa. Zaidi ya neema hiyo, Mwenyezi Mungu alimpa Abu Raajih umri na watoto wengi wa kiume.

11. ISMAIL BIN HARQALIY

Ismail bin Hasan Harqal alikuwa anaishi zama za utawala wa Khalifa wa Kibani Abbasi, Mustansir. Shamsuddin, mtoto wa Ismail bin Hasan Harqal anaelezea kisa cha baba yake alichowaelezea: “Zama za ujana wangu nilikuwa na kidonda kikubwa kilichochimba kwenye mguu wangu wa kulia. Wakati wa majira ya baridi, kilikuwa kikitooa damu na usaha. Nilisafiri kwenda Hillah kumuona Mujtahid Radhiuddin Ali Bin Taus na kumlilia hali yangu. Agha Radhiuddin aliwaita matabibu wa hapo Hillah na kuwaelezea hali yangu. Baada yaku-nichunguza, wote kwa pamoja walisema kwamba kidonda changu ni hatari sana na kimefikia kwenye mshipa kiasi kwamba wakati wa matibabu ikiwa mshipa huo utaathirika au kukatwa ninaweza kufa.

“Agha Radhiuddin akaniambia kwamba anaelekea Baghdad kwa ajili ya kazi kidogo na angependa nimsindikize kwa kuwa angeweza kuwaona watu wengine kwa ajili ya tiba yangu. Tulipowa-

⁴⁸ Maqaamul Mahdi: ni sehemu iliyopo Hillah (Iraq) na watu hupazuru.

sili Baghdad aliwaita madaktari bingwa wakristo. Baada ya kutazama kidonda, walikiri kwamba hawawezi kukitibu. Hapo nikaamua kurejea Harqal na njiani nikaona ni vyema nizuru Sammara ili kutoa salaamu kwa Maimamu. Agha Radhiuddin akafurahi kwa fikra hiyo, akanifanyia safari na akinipa pesa kiasi. Nilifika Samarra na baada ya kutoa salaam, niliingia ndani ya chumba ambamo Imam (a.t.f.) alitowekea. Hapo nilitoa salamu na kulia sana huku nikimuomba Imam msaada. Ilikuwa Alhamisi, nikaenda ufukweni mwa mto nika-fua nguo zangu kisha nikaoga... Niliporejea Samarra, kwenye lango la kuingilia mjini nikaona watu wanne juu ya farasi wakiwa wanaondoka. Walikuwa vijana wawili, mzee mmoja na wa nne alikuwa ni kijana mwenye uso wenye nuru. Wote walikuwa na panga. Nilidhania ya kwamba ni wafugaji (wamiliki wa wanyama) wanaoishi nje ya mji wa Samarra. Waliponiona walinisogelea na kunisalimu. Yule kijana mwenye nuru akaniuliza: ‘Je Ismail unataka kwenda nyumbani kwako kesho?’ Nikamjibu kwamba nataka na kwamba lengo langu ni mimi nipone. Akanitaka nimkaribie na hapo akainama na kuweka mkono wake juu ya kidonda kisha akaminya, jambo ambalo lilinisababishia maumivu makali. Baada ya hapo, yule mtu mzima akaniambia: ‘Ewe Ismail umekwisha pata faraja (umepona), tumepata faraja nanyi mmepata faraja.’ Nikajibu InshaAllah sote tutapata faraja. Nilistaajabu vipi hawa watu walivyojua jina langu kwani nilikuwa mgeni hapo mahala. Yule bwana mtu mzima akaniambia ya kwamba kijana huyo mtakatifu mwenye nuru ndiye Mahdi Sahibuz-zaman. Niliposikia hilo haraka nilimkimbilia na kumbusu.

“Wote waliondoka na kuniacha... sikustahamili nilianza kuwafuata. Imam akaniambia niende nyumbani, lakini sikuweza kujizuia, nilimlilia: ‘Ewe Maula, vipi nitaondoka nikuache wewe?’ Imam alinitaka tena niondoke nirejee nyumbani. Lakini nikang’ang’ania kuwafuata. Yule bwana mtu mzima akanigeukia na kuniambia: ‘Ewe

Ismail, huoni aibu kwamba kwa mara ya pili Imam wako anakutaka urejee (wende nyumbani) kisha unaendelea kutufuata?!’ Nilivunjika moyo, lakini nilikuwa sina jinsi, ni lazima nitii amri ya Imam. Imam Mahdi (a.t.f.) aligeuka na kuniambia: ‘Utakapofika Baghdad, Khalifa Mustansir atakuitisha na atapenda kujua jinsi kidonda chako kilivyopona. Atakupa begi lenye dinar 1000, usilikubali. Mfikishie mwanetu Mujtahid Sayyid Ali bin Tawus ujumbe kwamba amwandikie mfanyabiashara Sayyid Ali bin Awdh kuhusu pesa unazohitaji. Pia nami nitamweleza Sayyid Ali ili akulipe pesa hizo.’ Baada ya hapo walitoweka.

“Nilibaki katika hali ya majonzi. Nililia sana na kuingia Samarra. Watumishi wa Dharih⁴⁹ waliponiona katika hali kama hiyo waliniuliza kulikoni? Niliwaambia hakuna tatizo lolote. Niliwauliza kama wanawafahamu wale watu wanne waliokuwa juu ya farasi. Wao pia walikisia kuwa ni masharifu wafugaji. Nikawaeleza kwamba sivyo walivyodhania bali mmoja wao alikuwa ni Imam wetu Imam Mahdi (a.t.f.) na kwamba ameniponya. Nilifungua bendeji na kuwaonyesha. Kulikuwa hakuna athari yoyote wala kovu. Mwenyewe sikuumini. Nilifikiria nimekosea, nikaanza kuangalia mguu mwigine na kuukuta ukiwa salama salimini. Watu waliokuwa wamenizunguka walisoma Salawaat na kuanza kuchana nguo zangu kila mtu akitaraji kupata kipande cha nguo ili kutabaruku na Imam Mahdi (a.t.f.). Walinzi wa Dharih walilazimika kuniondosha hapo na kuniweka ndani ya moja ya vyumba, na baadaye msimamizi wa jeshi alikuja na kunihoji.

“Kesho yake niliondoka na kuelekea Baghdad. Habari za kuwasili kwangu zilikuwa zimekwishafika Baghdad na kulikuwa kuna halaiki ya watu wananisubiri kwenye daraja. Pindi tu nilipofika hapo

⁴⁹ Dharih: jengo zuri linalogengwa kwenye kaburi. Hususan kutukuzwa mahala walipozikwa watu watakatifu.

walianza kunichania nguo na kunizunguka. Maaskari waliniokoa na nikaingia mjini. Pia hapa halaiki la watu lilikuwa linanifuata. Sayyid Ali bin Tawus alikuja na kuniuliza kilichotokea. Nilimweleza kila kitu na kumuonyesha mahali palipokuwepo donda langu. Alizimia, baada ya kupata fahamu, alilia kama mtoto mdogo na akanishika mkono na kunipeleka kwa Waziri wa Khalifa Mustansir. Waziri huyu alikuwa ni Shia kutoka Qum (Iran). Baada ya kuniona aliwaita matabibu wa kikristo waje waone muujiza huu. Walipofika, Waziri aliwauliza kama wananifahamu na kama waliona donda langu. Wali-kubali na kukiri kwamba lilikuwa haliwezi kutibika ila kwa upasuaji ambao ulikuwa pia ni hatari kwa maisha yangu. Waziri aliuliza zaidi kwamba kama lingekuwa linaweza kutibika bila upasuaji donda hilo lingepona baada ya muda gani? Wakajibu kwamba ingechukua miezi miwili na lazima pangebaki kovu kubwa na shimo.”⁵⁰

12. MASJID JAMKARAAN

Msikiti uliopo kilomita sita Magharibi ya mji wa Qum. Ulijengwa kwa amri ya Imam Sahibuz Zamaan (a.t.f.). Kisa chake kwa muhtasari: Sheikh Hasan bin Muthlah wa kijiji cha Jamkaraan anasimulia: Tarehe 17 Ramadhan 373 H., usiku wa Jumanne, watu walikuja nyumbani kwangu na kuniamsha kwamba niitikie mwito wa Imam Mahdi (a.t.f.). Walinipeleka mahala ambapo leo umejengwa msikiti wa Jamkaraan. Hapo niliona zulia zuri sana, juu yake walikuwa wamekaa kijana mmoja na mzee. Huyu mzee ambaye ni Nabii Khidhr akaniambia nikae chini. Imam Mahdi (a.t.f.) akaniita kwa jina langu na kunipa maelekezo yafuatayo: “Nenda kwa Hasan bin Muslim anayelima ardhi hii na umwambie kwamba ardhi hii ni tukufu na Mwenyezi Mungu ameichagua. Kwa hivyo asiilime tena.”

⁵⁰ Kisa hiki kimenukuliwa ndani ya kitabu ‘*Kashful Ghumma*’. Kilitokea zama za mwandishi, mwaka wa 635H. Hillah ilikuwa chini ya uongozi wa Sayyid bin Taus.

Niliomba ushahidi ili watu waweze kuniamini. Imam alinitaka niende nitekeleze maagizo, ama suala la ushahidi yeye mwenyewe atalifanya. Na Imam (a.t.f.s.) akaongeza: “Pia nenda kwa Sayyid Abul Hasan mmoja katika ulamaa wa Qum na umwambie amwit-ishe (Hasan bin Muslim) na achukue kutoka kwake faida aliyoiipata kutokana na ardhi hiyo kwa miaka mingi na kisha ajenge msikiti mahala hapo.”

Imam alielekeza ibada ya kufanywa hapa nayo ni:

- Rakaa nne, mbili kwa ajili ya heshima ya msikiti.

Kila rakaa soma sura Hamd na sura Ikhlasw mara saba. Katika rukuu na sijda soma dhikr mara saba. Katika rakaa mbili nyingine soma sura Hamd, aya ‘*Iyyaka na ‘budu wa Iyyaka nasta ‘iin*’ soma mara mia moja kisha malizia sura. Kisha soma sura Ikhlasw. Katika rukuu na sijda soma dhikr mara saba.

Baada ya kumaliza rakaa nne, soma

- *Lailaaha illa llah* (mara moja),
- Tasbiih ya Bibi Fatima Zahraa. Kisha fanya sijda na usome
- ‘*Allahumma Swalli Alaa Muhammad wa Aali Muhammad*’ (mara 100). – Imam akasema: “Atakayeswali rakaa mbili hizi ni kama vile mtu aliyeswali ndani ya Kaaba.”

Nilipoanza kuondoka, Imam (a.t.f.) aliniita na kuongeza: “Kuna mbuzi katika zizi la Ja’far Kashani. Mnunue na umlete hapa kisha umchinje na wape wagonjwa nyama yake, watapona kwa kuila.”

Baada ya kurejea nyumbani, Hasan bin Muthlah alitafakari ya-liyojiri usiku huo. Asubuhi baada ya swala, alikwenda kwa rafiki yake Ali al-Mundhir na kumhadithia. Walikwenda pamoja mahala

hapo na kukuta vipande vya minyororo ya chuma vinavyoashiria eneo la msikiti. Walifunga safari pamoja na kwenda Qum kuonana na Sayyid Hasan bin Ridha. Walimkuta tayari ana taarifa na anawa-subiri kwa hamu. Sayyid aliwakaribisha na kuwafahamisha kwamba aliota ndoto usiku akiambiwa kwamba atakuja mtu kwako anaitwa Hasan bin Muthlih. Kubali kila atakachokuelezea. Kauli yake ni kauli yetu. Baada ya hapo, Hasan bin Muthlih alimuelezea Sayyid kila kitu. Pamoja walielekea Jamkaraan. Njiani waliona zizi la Ja'far Kashan. Walipoteremka tu, mbuzi mmoja akamkimbilia Hasan bin Muthlih. Ja'far ilitaajabu kwani alikuwa hamjui mbuzi huyo. Walimchukua na kumchinja mahala pa msikiti. Kila mgonjwa aliyekula nyama yake alipona kwa Baraka za Mwenyezi Mungu na Walii Wake Imam Mahdi (a.t.f.). Baada ya hapo, Sayyid alimuita Hasan bin Muslim na kuchukua kwake kile kiasi cha fedha na kuanza ujenzi wa msikiti. Alichukua ile minyororo ya chuma na kuiweka nyumbani kwake. Kila aliyekuwa akiigusa alipona maradhi yake. Baada ya kufariki Sayyid, minyororo hiyo ilitoweka.

13. DUA AL FARAJ

Abul Hasan bin Abil Baghl anasimulia kwamba yalitokea matatizo baina yake na Abu Mansur bin Swaalihan ikabidi ajifiche, kwani huyu alikuwa anamtishia maisha yake. Usiku wa Ijumaa akaamua kwenda kuzuru Makaburi ya Maquraysh na kukesha hapo kwa dua na ibada. Ulikuwa ni usiku wa mvua na upepo. Anasema: “Nilim-omba mlinzi afunge milango asiingie mtu. Nikajishugulisha na dua, Ziyara na swala. Katika hali kama hii nikamsikia mtu sehemu ya Imam Musa al-Kadhim (as) anazuru na kutoa salaam kwa Nabii Adam (as) na Mitume Ulul Azm, kisha kwa Maimamu mmoja baada ya mwingine hadi alipofika kwa Imam wa Zama (a.t.f.) hakumtaja. Hapo nikastaajabu na kufikiria kwamba huenda kaghafilika au hajui

au hiyo ndiyo madhehebu yake. Alipomaliza Ziyara yake, aliswali rakaa mbili kisha akaenda kumzuru Abu Ja‘far (as) kwa Ziyara kama ile ile ya mwanzo kisha akaswali rakaa mbili. Nilikuwa na hofu kwani nilikuwa simjui. Alikuwa ni kijana amevaa nguo nyeupe, amefunga kilemba na joho... mara aliniambia: ‘Ewe Abul Hasan bin Abil Baghl, uko wapi wewe na dua al-Faraj?’ Nilimuuliza: Ewe bwana wangu ni dua gani hiyo? Akanielekeza: “Unaswali rakaa mbili kisha unasema: kisha baada ya hapo soma dua utakayo na uombe haja yako. “Kisha weka shavu lako la kulia kwenye ardhi na useme mara mia moja katika sijda: Ewe Muhammad, ewe Ali, ewe Muhammad nitoshelezeni hakika nyinyi ni wenye kunitosheleza na mminusuru hakika nyinyi ni wenye kuninusuru. Kisha weka shavu lako la kushoto kwenye ardhi na useme mara mia moja: ‘Adrikni’ (unidiriki) kariri sana kisha sema: ‘alghawth’ (msaada) (3x) hadi inapokatika pumzi, kisha inua kichwa chako, Mwenyezi Mungu kwa ukarimu Wake atakidhi haja yako Insha’Allah.”

Nilishughulika na swala na dua, baada ya kumaliza ibada zangu nilimfuata Abu Jafar ili kujua vipi yule mtu aliingia. Niliona milango imefungwa. Nilistaajabu, lakini nikadhania kwamba huenda kalala hapo. Abu Jafar akanithibitishia kwamba hakufungua milango abadan. Nilimuelezea kisa changu na yale nilioyashuhudia naye akasema huyo ni bwana wetu Sahibu Zamaan (a.t.f.). Mimi nime muona mara nyingi katika usiku kama huu pindi panapokuwepo faragha. Nilisikitika kwa fursa iliyoniponyoka. Alfajiri nilitoka na kurejea mahala pangu nilipokuwa najificha. Baadaye nilipata taarifa kwamba Ibn Salihan amewatuma masahiba wake kuja kunitafuta wakiwa na waraka wa amani. Nilikwenda kwake na akanipokea vye ma kisha akiniambia: “Imekuwaje hali yako mpaka unanishtaki kwa Imam wa Zama (a.t.f.)? Nilimuona jana (yaani usiku wa Ijumaa) bwana wangu katika ndoto akiniamuru wema na alikuwa mkali katika hilo kiasi kwamba ya kunitia hofu.” Hapo mimi nikasema *Laila-*

ha illallah, nashuhudia ya kwamba wao ni haki na mwisho wa haki. Mimi nilimuona usiku uliopita bwana wetu nikiwa macho na akanielekeza kadha wa kadha. Nilimuelezea niliyoyaona katika dharah takatifu. Alistaajabu na akanifanyia wema mkubwa na nikafikia hali niliyokuwa sitarajii kwa Baraka za Swahibuz Zamaan (a.t.f.).

14. DUA AL-ALAWY AL-MISRI, (SAYYID MUHAMMAD BIN ALI AL-ALAWY AL-HUSAYNY WA MISRI).

Sayyid Muhammad bin Ali al-Alawy wa Misri anaelezea kwamba: Tatizo kubwa lilitokea baina yangu na mtawala wa Misri kiasi cha kunizulia fitna kwa Ahmad bin Tuluun⁵¹. Nilihofia maisha yangu kwa hivyo nikatoka Misri na kwenda hijja na baadaye nikaelekea Iraq nikikusudia kaburi la bwana wangu Imam Husayn (as). Hapo penye kaburi lake takatifu nilimtaka ulinzi, hifadhi na msaada dhidi ya jeuri ya huyo niliyekuwa namuogopa. Kwa siku kumi na tano nilikuwa naomba kwa kunyenyekea usiku na mchana. Mara nika muona Bwana wa Zama nikiwa katika hali baina ya kulala na kuwa macho. Akaniambia: Imam Husayn (as) anasema: ‘Ewe mwanangu hivi unamhofia fulani?’ Nikajibu: ‘Naam, anataka kuniangamiza na nimekimbia kwa bwana wangu namshitakia makuu ya balaa analonitakia adui huyo.’ Imam akanielekeza niombe dua ambayo Mitume waliomba pindi walipokuwa katika shida na Mwenyezi Mungu akawaondolea balaa. Dua yenyewe inaombwa usiku wa Ijumaa, unaoga, unaswali swala ya usiku, unasujudu sijda ya kushukuru kisha unaomba dua hiyo ukiwa umepiga magoti.

Alinjia usiku katika hali ile ile kwa siku tano mfululizo akikariri haya maelezo na dua hii mpaka nikaihifadhi. Usiku wa Ijumaa

⁵¹ Ahmad bin Tuluun: (alitawala 868-884), mtawala binafsi na huru wa Misri na Syria chini ya Ukhalifa wa ki-Abbasi wa Baghdad.

hakuja. Nilioga na kubadilisha mavazi yangu na kujipaka uturi na kuswali swala ya usiku. Nikasujudu sijda ya kushukuru kisha nikapiga magoti na kumlilia Mwenyezi Mungu kwa dua hii (niliyo-fundishwa). Usiku wa Jumamosi alinjia na kuniarifu kwamba dua yako imejibiwa ewe Muhammad na huyo adui yako ameuliwa pindi tu ulipomaliza kusoma dua.

Nilipokuwa narejea nyumbani nilikutana na jirani yangu huko Misri naye akanifahamisha kwamba Ahmad bin Tuluun alimshika hasimu wangu na kuamuru akatwe shingo na kutupwa ndani ya mto Naili na ilikuwa ni usiku wa Ijumaa.

F. WAJIBU WETU KIPINDI CHA GHAYBA KUBWA

Dharura ya kumtambua Imam wa zama hizi:

Uthman al Amri alimsikia baba yake akisimulia ya kwamba aliulizwa Abu Muhammad Imam Hasan bin Ali Askariy (as) kuhusu kauli ya mababu zake inayosema: ‘Ardhi haiwezi ikabaki bila Hoja ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe Wake hadi siku ya Kiyama. Na hakika amekufa kifo cha kijahiliya yule asiyemjua Imam wa zama zake.’ Akasema: “Hii ni kweli kabisa kama vile mchana ulivyo kweli.” Kisha aliulizwa (as): “Ewe mtoto wa Mtume (saww), baada yako nani atakuwa Imam na Hujjah?” Akajibu: “Mwanangu Muhammad. Yeye ndiye Imam na Hujjah baada yangu mimi. Yeyote anayekufa bila kumtambua, basi amekufa kifo cha kijahiliya”. (*Kamaaluddin Jz. 2 uk. 409, Kifayatul Asar uk. 292*).

Hii ni hadithi inayodhihirisha dharura ya kumtambua Imam wa Zama. Asiyemjua Imam wa zama zake anaishi maisha na kufa kifo cha kijahiliyyah. Kumjua kiongozi wa Hizbullahi na kumnusuru ndiyo kusimamisha Tawhidi. Kutowatambua hawa ni kuwatambua

mataghuti ambao ndiyo viongozi wa hizbushaytani ambao ndiyo wenye kusimamisha ujahiliyyah. Mwenyezi Mungu anasema:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ
وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى
الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

“Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutawala wale walioamini, huwatoa katika giza na kuwapeleka kwenye mwangaza. Na wale makafiri, wenye kuwatawala wao ni mashetani, huwatoa katika nuru na kuwaingiza kwenye giza...” (2:257).

Historia ya Kiislamu imejaa vituko na mabalaa ya ujahiliyyah uliofanywa na hizbushaytani na kusaidiwa na Waislamu kwa kukataa kumtambua Imam wa zama zao. Huu ni mfano muhimu kama kielelezo:

Muawiyah bin Abi Sufyan, ni Sahaba wa Mtume (saww) aliyesilimu kwa kuzidiwa nguvu, wakati wa Fathu Makka mwaka wa 8 H., alisilimu yeye na baba yake Abu Sufyan, adui mkubwa wa Mtume (saww). Bila shaka alishuhudia utukufu na ushujaa wa Ali (as) katika vita mbalimbali. Alijua nafasi ya Ali (as) kwa Mtume (saww) kuwa nafsi yake, kama walii wa Mwenyezi Mungu aliyepewa tuzo pekee la kumuoa mwanamke bora kwa walimwengu, Bibi Fatima (as). Masahaba wote walikataliwa heshima hiyo, kwa sababu hawakuwa na daraja ya mwanamke huyo aliyetoharishwa, maasumu. Pekee aliyekamilisha sifa ni Ali. Hiki ni kielelezo cha daraja ya juu ya imani yake na utakasifu wake. Alishuhudia elimu,

hekima na uchamungu wa Ali. Alisikia masahaba wakisema: ‘Anayemchukia Ali ni mnafiki.’ Alishuhudia Mtume (saww) hapo Ghadir Khum akitangaza: “Kwa yeyote Yule ambaye mimi ni bwana wake, Ali ni bwana wake...”

Baada ya yote haya yaliyosemwa na Qur’ani na Hadithi kuhusu Ali (as) na Ahlul Bayt, Muawiya mwaka wa 35 H. alisimama dhidi ya Ali (as) na kupinga ukhalifa wake. Isitoshe hilo akawalazimisha Waislamu wamlaani Walii wa Mwenyezi Mungu huyo na nafsi ya Mtume (saww), mume wa Fatima na baba wa Hasan na Husayn. Kisha akawaua wapenzi wa Ali na Ahlul Bayt kwa kosa tu la kumfuata Mtume (saww) na Mwenyezi Mungu aliyeamrisha kuwapenda Ahlul Bayt (as). Je hii ndiyo inaitwa ijthadi ya Masahaba? Kupambana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake? Baada ya ukafiri huo akatuma sumu ya kumuua Imam Hasan (as) kwa kumghilibu mkewe Ju’dah binti Ash’ath. Hakutosheka hadi alipokanyaga kichwa cha Uislamu kwa kumtawalisha mtoto wake Yazid maarufu kwa ufuska wa kila aina kuwa khalifa wa Mtume (saww). Akavunja ukhalifa na kusimika utawala wa kifalme wa Bani Umayyah!

Pamoja na madhambi yote haya ya uasi dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na kuudhili Uislamu na Waislamu, Muawiya alitetewa na baadhi ya Waislamu na kutukuzwa kiasi cha kuyafanyia taawili maovu yake kwamba ilikuwa ni ijthadi na hivyo kama alikosea, basi anasamehewa! Kweli usipomjua Imamu wa zama zako, utamshika mkono Shetani akuongoze... na bila shaka utatetea nidhamu ya kijahiliyyah na kufa kifo cha kijahiliyyah. Waislamu tuamke...

Wajibu wetu kwa Imam:

Baada ya kumtambua Imam Mahdi (a.t.f.) kuwa ndiye Imam wa zama hizi, na khalifa wa Mwenyezi Mungu ndani ya ardhi, nini wajibu wetu? Tunamnuku hapa Sayyid Muhammad Taqi Musawi Isfahani na kutoa maelezo:

1. Kupata elimu kuhusu sifa mahsusi za Imam (a.t.f.)

Ni wajibu kwa muumini kumjua Imam ambaye ni wajibu kumtii. Kwa kuzijua sifa zake inakuwa vigumu kwa mzushi yeyote kuwapotosha waumini.

Pia kwa kujua sifa zake na daraja yake ndiyo tutaelewa upeo wa Uimamu wake na hivyo kumfuata. Usipojua thamani ya kitu huwezi kukithamini.

2. Kuwa na adabu pindi tunapomtaja

Tunapomtaja Imam (a.t.f), tunatakiwa kutumia majina yake kama vile Hujjah, Qaim, Mahdi, Sahibul Amr and Sahibuz-Zaman, n.k. Tunatakiwa kujiepusha na kumtaja kwa jina lake ambalo ni kama la Mtume (Muhammad).

3. Kumpenda

Kuwapenda Ahlul Bayt (as) ni wajibu. Kuwapenda ni moja ya misingi ya imani yetu na moja katika masharti ya amali zetu kukubaliwa. Ni vipi utamfuata usiyemjua wala usiyependa? Mwenyezi Mungu amewapa Mtume na Ahlul Bayt wake baraka, karama na utukufu ili waumini wavutike kwao na wawapende na kuwafuata.

4. Kumtukuza na kumtangaza miongoni mwa watu

Wengi wamepotea kwa kutomjua nani Imam wa Haki. Laiti watu wangewajua Ahlul Bayt (as) wasingemfuata yeyote isipokuwa wao. Katika amali njema hakuna kama kujitahidi kuwaongoza watu kumjua Imam wa Haki anayeongoza kwenye njia iliyonyooka. Imam Sadiq (as) alisema: “Mwenyezi Mungu amrehemu yule anayetufanya sisi kupendwa na watu na ambaye hafanyi jambo linalowafanya watu kuwa maadui wetu na kutuchukia.”

5. **Kusubiria kudhihiri kwake (*Intidhaar*)**

Ni wajibu kwa waumini kuwa daima katika hali ya kumsubiri Imam (a.t.f.) na kutarajia kudhihiri kwake.

Maana halisi ya *Intidhaar* ni sawa na ile hali ya nafsi anayokuwa nayo mtu anapokuwa anamsubiria mtu muhimu. Kadri unavyotarajia mgeni huyo muhimu kufika, ndivyo unavyojitayarisha ipasavyo (kufanya maandalizi) kumpokea. Maandalizi na shauku ya kumsubiria mgeni hutegemea umuhimu wa mtu huyo na uhusiano uliopo. Kwa hiyo kadri yatakavyozidi mapenzi yako kwa Imam (a.t.f.) ndivyo utakavyozidi kumtarajia na kutamani haraka kudhihiri kwake. Mtume (saww) alisema: ‘Mwombeni Mola Wenu kwa rehma Yake na ukarimu Wake, kwani kwa hakika Mwenyezi Mungu anapenda kuombwa. Na ibada ya juu kabisa ni kusubiria kudhihiri (kwa Qaim wa Nyumba ya Mtume (saww)).’

6. **Kutamani na kuwa na shauku ya kumuona**

Unapompenda mtu lazima unatamani kumuona na kuwa naye. Shauku ya dhati ya kumuona Imam (a.t.f.) ni moja ya dalili ya kumpenda. Moyo unaungua na kwa shauku ya kukuona machozi yanatiririka. Kwa sababu ya kufarikiana karibu machozi yatatuzamisha na shauku ya kukuona karibu inatuunguza. Ni lini tutakuona na wewe ukatuona?

7. **Kuwa na huzuni kwa kuwa mbali na Imam**

Ni kawaida mtu anapokuwa mbali na mpenzi wake kuwa na majonzi na kuugua. Muumini wa kweli lazima awe na huzuni moyoni mwake kwa kumkosa Imam wake.

8. Kuelezea sifa zake tukufu

Maadui wa Uislamu walijitahidi kuzima nuru ya Ahlul Bayt (as) na utukufu wao. Ni wajibu wetu kuzielezea na kuzitangaza sifa hizo ili Waislamu wawatambue na kuwafuata. Kumnusuru Mtume (saww) na kupigania Uislamu ni kuwafuata Ahlul Bayt (as). Uislamu kuwa na viongozi waovu ndiyo hasara kubwa kwa umma huu.

9. Kuhudhuria, kushiriki majalis za Imam (a.t.f.) zinazoelezea utukufu na fadhila zake.

Hii bila shaka ni dalili ya mapenzi na njia ya kuhuisha utajo wao.

10. Kuandaa mikutano kwa ajili ya kumzungumzia Imam (a.t.f.)

Hii ni kuandaa mikutano, kongamano, semina, majlis... kwa ajili ya watu kukutana na kuhuisha utajo wa Imam na Ahlul Bayt (as).

11. Kutunga na kusoma mashairi ya kumsifu Imam (a.t.f.)

12. Kusimama kwa adabu na heshima pindi Imam anapotajwa

13. Kulia na kuwaliza watu

Ni wajibu wetu kukumbuka misiba na balaa zilizowafika Watu wa Nyumba ya Mtume (as) na kulia

14. Kumuomba Mwenyezi atupe maarifa ya Imam (a.t.f.).

A. DUA YA KUOMBA MAARIFA:

اللَّهُمَّ عَرِّفْنِي نَفْسَكَ فَإِنَّكَ إِنْ لَمْ تُعَرِّفْنِي نَفْسَكَ لَمْ
 أَعْرِفْ نَبِيَّكَ اللَّهُمَّ عَرِّفْنِي رَسُولَكَ فَإِنَّكَ إِنْ لَمْ
 تُعَرِّفْنِي رَسُولَكَ لَمْ أَعْرِفْ حُجَّتَكَ اللَّهُمَّ عَرِّفْنِي
 حُجَّتَكَ فَإِنَّكَ إِنْ لَمْ تُعَرِّفْنِي حُجَّتَكَ ضَلَّتُ عَنْ دِينِي
 اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَعَجِّلْ فَرَجَهُمْ

“Ee Allah! Nifanye mimi nikujue, kwani ikiwa mimi sikukujua sitoweza kumjua Mtume Wako. Ee Allah! Nifanye mimi nimjue Mtume Wako, kwani ikiwa sikumjua Mtume Wako sitoweza kumjua Hujjah Wako. Ee Allah! Nifanye mimi nimjue Hujjah Wako kwani kama sikumjua Hujjah Wako nitapotea kwenye dini yangu. Ewe Allah msalie Muhammad na Aali Muhammad na harakisha faraja yao.”

B. DUA YA MTU ANAYEZAMA MAJI:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ يَا اللَّهُ يَا رَحْمَانَ يَا رَحِيمَ
 يَا مُقَابِلَ الْقُلُوبِ ثَبَّتْ قَلْبِي عَلَى دِينِكَ. اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى
 مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَعَجِّلْ فَرَجَهُمْ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Ewe Allah, ewe Rahman, ewe Mrahimu, ewe Mwenye kuzigeuza nyoyo, uimarisha moyo wangu katika dini yangu. Ewe Allah msalie Muhammad na Aali Muhammad na harakisha faraja yao.”

15. Daima kumuomba Imam (a.t.f.)

16. Kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Alama za kudhihiri

Mtume (saww) na Maimamu wameelezea alama za kudhihiri ili kutowapa mwanya wadanganyifu na waongo watakaodai umahdi. Kwa hiyo kuzijua alama hizo ni kuwa na uhakika wa kumtambua Imam (a.t.f.). Umar Ibn Hanzala anasimulia kwamba Imam Sadiq (as) alisema: “Kuna alama tano thabiti kuhusu al-Qaim (a.t.f.): Sufyani, Yamani, mwito kutoka Mbinguni, kuuliwa kwa Nafsuz-Zakiyyah (Nafsi takatifu) na kutitia kwa ardhi hapo Baidah.”

17. Kufanya amali njema kwa ajili ya Imam (a.t.f.)

Hii ni ishara ya mapenzi na kumjali na kumpa kipaumbele kabla ya nafsi zetu. Kwa hiyo ni matendo yenye thawabu kufanya Hijja, Tawaf, Ziarah (ya Mtume na Maimamu), kutoa Sadaka kwa ajili ya usalama wa Imam,... Bila shaka kwa kumjali Imam yeye pia atatujali.

18. Kuwa na niya thabiti ya kumsaidia Imam wakati wa kudhihiri kwake.

19. Kula upya kiapo cha utii (Bay‘ah) kila siku na kila Ijumaa

Maana ya Bay‘ah ni mtu kula kiapo cha utii kwa ikhlaswi kwamba atatui na kumsaidia aliyempa kiapo kwa mali na nafsi yake.

Dua maarufu inayosomwa kila asubuhi kwa ajili ya kiapo ni Dua ul ‘Ahd (rej. Dua ‘Ahd.)

20. Kumsaidia Imam (a.t.f.) kwa mali yako

21. Kutoa msaada wa kifedha kwa Mashia wachamungu na marafiki wa Imam (a.t.f.)

22. Kuwafurahisha waumini

Hii ni kwa kuwasaidia kifedha, kihali, kuwatatulia matatizo yao, kuwaombea, kutowabana kulipa madeni yao... Kitendo hicho ni chenye kumridhisha sana Imam (a.t.f.), Mtume (saww) na Mwenyezi Mungu.

23. Ziyarah ya Imam (a.t.f.)

Ni wajibu wetu kumuelekea Imam na kumpelekea salaam. Zipo aina mbalimbali za Ziyarah na taratibu zake. Ziyarah ni njia madhubuti ya kujenga uhusiano na Maimamu wetu na kuhuisha utukufu wao ndani ya nyoyo zetu.

24. Kushikamana na ulamaa, mafaqihi wachamungu

Kumnusuru Imam ni kufuata wasia wake. Wakati wa Ghayba Kubwa alituusia kushikamana na ulamaa wachamungu. Ulamaa hawa ndio mawakili wake. Kuwafuata na kuwaenzi bila shaka ndiyo kumuenzi na kumfuata. Faida ya kuwafuata ulamaa wema imeonekana katika Mapinduzi ya Kiislamu huko Iran, ambapo kiongozi wa kiroho na kimwili, Ayatullah Khomeini aliwaunganisha watu na kutokomeza utawala wa Shah Pahlawi.

Ikiwa ni lazima kuwafuata ulamaa wema basi ni lazima kuwatambua wanazuoni waovu na kujiepusha nao. Wanazuoni waovu ambao wako nyuma ya dunia na uovu wao dhidi ya dini ni zaidi ya ule wa jeshi la Yazid (l.a).

Mazingatio:

- Makusudio ya Ghayba: Ni kwamba watu watamuona lakini hawatamtambua kama vile ilivyokuwa kwa ndugu zake Nabii Yusuf (as). Walizungumza naye bila ya kumtambua.
- Yeyote anayedai kuonana na Imam (as) kwa maana ya kwamba yeye ni wakili wake, huyo ni muongo.
- Wako wengi ambao wamekutana na Imam na kufaidika na Baraka zake.
- Imam amewasaidia ulamaa wengi kutatua matatizo mbalimbali ya dini.

MLANGO WA 3

ALAMA ZA KUDHIHIRI NA SERIKALI YA HAKI

1. ALAMA ZA KUDHIHIRI IMAM
2. MAPAMBANO DHIDI YA DHULMA
3. SERIKALI YA MUNGU YENYE HAKI NA UADILIFU
 - A. ALLAHKRASIA
 - B. ZAMA ZA AMANI NA HAKI

“Mmoja katika watoto wangu atamaliza magomvi yote. Ataondosha kila aina ya ufisadi na kuwafyeka waovu wote kwa upanga wake. Atapigana vita kwa miezi minane.”
- (Imam Ali (as))

1. ALAMA ZA KUDHIHIRI IMAM

“Yeyote anayekanusha kudhihiri Mahdi (a.t.f.), bila shaka amekufuru aliyoteremshiwa Muhammad (saww), na yeyote anayekadhibisha kuteremka Isa (as), bila shaka amekufuru, na yeyote anayekufuru kutokeza Dajjal, bila shaka amekufuru”.

Mtu alimuuliza Imam Baqir (as): Ewe mtoto wa Mtume ni lini atadhihiri Qaim (Mahdi) wenu? Imam Akajibu:

- “Pindi wanaume watakapowaiga wanawake na wanawake watakapowaiga wanaume,
- Pindi wanawake watakapopanda mapando,
- Watu watakapoacha swala na watu kufuata matamaniao yao,
- Watu watakapokuwa wala riba,
- Pindi kumwaga damu kutapokuwa jambo rahisi,
- Pindi riba itapokuwa ndiyo msingi wa biashara,
- Pindi watu watakapokuwa wanazini hadharani,
- Pindi watu watakapokuwa wanajenga majengo marefu,
- Pindi uongo utakapokuwa halali,
- Pindi watu watakapokubali rushwa,
- Pindi watu watakapokuwa nyuma ya ashiki na tamaa zao,
- Pindi watakapouza dini yao kwa ajili ya dunia,
- Pindi watakapokata uhusiano wa undugu,
- Pindi watakaposimanga kwa ajili ya chakula,
- Pindi watakapotazama ustahamilivu kuwa ni unyonge na dhulma kuwa ni fahari,

- Pindi watawala watakapokuwa ni waovu,
- Pindi mawaziri watakapokuwa ni waongo,
- Pindi wasimamizi watakapokuwa wasaliti,
- Pindi wasaidizi watakapokuwa madhalimu,
- Pindi wasomi watakapokuwa mafasiki,
- Pindi itakapodhihiri dhulma, jeuri,
- Pindi talaka zitakapozidi,
- Pindi utakapoenea ukahaba na uzinzi,
- Pindi ushahidi wa uongo utakapokubaliwa,
- Pindi pombe zitakaponywewa hadharani,
- Pindi wanaume watakapowapanda wanaume wenzao,
- Pindi wanawake watakaposhughulika na wanawake (katika uchafu),
- Pindi Zaka itakapochukuliwa kuwa ni ngawira,
- Pindi sadaka itakapoonekana kuwa ni gharama na kupoteza,
- Pindi waovu watakapoogopwa kwa sababu ya ndimi zao,
- Pindi Sufyani atakapotokeza kutoka Sham,
- Pindi Yamani atakapotokeza kutoka Yemen,

- Pindi ardhi itakapopasuka baina ya Makka na Madina mahala panapoitwa Baidaa,
- Pindi atakapouliwa kijana kutoka Aali Muhammad baina ya Rukni na Maqaam,
- Pindi itakaposikika sauti kutoka mbinguni kwamba haki ipo pamoja na Mahdi na wafuasi wake. Hapo ndipo atakapodhihiri Qaim wetu.”

Muda wa kudhihiri Imam Mahdi (as) ni katika mambo yaliyofichwa kiasi kwamba hata yeye Imam hajui ni wakati gani atadhihiri. Pekee Mwenyezi Mungu ndiye anayejua. Kwa hiyo mtu yeyote atakayedai kujua au kuainisha muda kuhusu kudhihiri Imam Mahdi (as) ni mwongo kadhabu na maluuni.⁵²

Pia suala la kudhihiri Imam (a.t.f.) ni muhimu sana na hoja ya Mwenyezi Mungu kwa walimwengu katika kusimamisha Tawhid. Kwa sababu hiyo Mtume (saww) alielezea kwa mapana na marefu alama kabla ya kudhihiri Imam ili kufunga mlango kwa watu waongo madajjali watakaodai umahdi kwa maslahi yao binafsi. Hadithi zimeeleza alama nyingi ambazo zimegawanyika katika mafungu mawili: Zipo alama ambazo ni ‘Mahtuum’ kwa maana ni thabiti, lazima zitatokea. Na zingine ni ‘Mushtaritwah’ sio thabiti, zinategemea baadhi ya masharti. Hapa tutataja tu zile ambazo ni ‘thabiti’.

⁵² **Mchezo wa ndoto.** Pamoja na indhari hii lakini bado tunashuhudia watu waongo wakidanganya watu kuhusu kudhihiri Imam. Mfano: kuna karatasi zinasambazwa kwamba: ‘Shaykh Ahmad Shamiy msimamizi wa msikiti wa Madina aliota ndoto kwamba yatatokea mambo kadha wa kadha, kwa hivyo watu tubuni kwa Mola wenu, Mahdi atadhihiri baada ya miaka sita...’ Ajabu kuna watu wengi wanaamini haya na kupiga photocopy ujumbe huo kama ilivyoagizwa na kuusambaza. Huu ni upuuzi, Waislamu tusome na kujua dini yetu.

ALAMA THABITI, LAZIMA ZITATOKEA

1. KUENEA DHULMA NA UKANDAMIZAJI

Miongoni mwa alama kubwa za kudhihiri Imam (a.t.f.) ni kuenea kwa dhulma, ukandamizaji na kutoweka kabisa kwa amani na usalama kiasi kwamba jamii itatawaliwa na ujahili, woga, uifisadi, maafa, majanga... Watu watashindana katika maasi na uovu na kuona kwamba hilo ni jambo jema. Uislamu utakuwa mgeni kama ulivyooanza, sheria za Mwenyezi Mungu zitapuuzwa. Tawala za madhalimu zitawakandamiza Waislamu...

Riwaya zinaonyesha kwamba karibu na kudhihiri Imam Mahdi (as) kutakuweko na:

Hali ya vurugu:

- Uchochezi, uasi, na fitna itakapotanda na kuenea.
- Hakuna mkubwa atakayemuonea huruma mdogo na hakuna mdogo atakayemheshimu mkubwa.

Mauwaji na vifo:

- Kudhiri ‘kifo cheupe’ na ‘kifo chekundu’. Kifo cheupe hii inaashiria watu kuangamia kwa tauni na kifo chekundu kwa upanga. Vita itazuka itakayoshamiri Magharibi na Mashariki. Mahdi hatodhihiri mpaka katika watu watatu, wawili waangamie na mmoja pekee ndiye abaki hai.

Maafa na misukosuko:

- Maafa makubwa na balaa ambazo hazijawahi kutokea zitawashukia watu na hawatapata kinga wala hifadhi.

- Matetemeko ya ardhi, tauni, mtafaruku katika dini, kukata tamaa na kuvunjika moyo.
- Vita na magomvi kushamiri.

2. KUJA KWA DAJJAL

Mojawapo ya alama za uhakika za kudhihiri Imam Mahdi (a.t.f.) ni kutokeza kwa Dajjal. Atapoteza fikra za watu na Mayahudi watamkubali na kumpenda sana. Dajjal atadanganya watu kwa utajiri na pesa. Atakuwa na nguvu sana kiasi kwamba atamiliki baadhi ya maeneo ya Ulimwengu wa Kiislamu. Baadhi ya mambo yanayohusiana naye ni kama yafuatayo.

Dajjal atatokeza kabla ya Imam Mahdi (a.t.f):

Miongoni mwa fitna zake ni kushirikiana na mashetani. Mathalan mtu ataambiwa ikiwa nikifufua wazazi wako utaamini kwamba mimi ni Mungu wako? Akikubali basi mashetani wawili watajigeuza na kuja kama wazazi wake na kumwambia ewe mwanetu, mtii kwa sababu yeye ni Mungu wako.

Majina yake:

Jina lake maarufu ni Dajjal (mdanganyifu, anayechanganya, uongo akauvika ukweli..). Mengine ni Chongo (mojawapo ya macho yake). Majina mengine ni Abu Yusuf, Dhidi Kristo (Anti-Christ), Amirus Salaam, Ilahkar. Ama Wakristo wanamuita: Rais, Dikteta (Mtawala wa kimabavu), Mtawala Mkuu.

Sifa za Dajjal:

Hadithi zinaashiria ya kwamba Dajjal ima ana jicho moja au kipofu wa jicho moja.

Hali ya Waumini zama za Dajjal :

Hakuna fitna kama ile ya Dajjal. Waumini watateswa na kukandamiwa zama zake. Dajjal atakuwa na maajabu na miujiza kama vile (kunyeshesha mvua nk.) ambayo yatamfanya aweze kuwapoteza wengi ila waumini ambao wataweza kufichua hila zake.

Atamiliki mito na matunda ya Ardhi na kwa wale watakaomfuata atawapa chakula na kuwageuza kuwa makafiri. Lengo lake hasa ni ufisadi, mabalaa na mitihani kwa watu. Wataepukana naye wale waumini ambao imani yao ni thabiti. Dajjal atawasakama waumini na adhabu kali.

Wafuasi wa Dajjal:

Ama wafuasi wake na wasaidizi, wengi wao watakuwa ni Mayahudi. Wao hasa ndiyo kiini cha ufisadi Duniani. Kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww):

- Wasaidizi wa Dajjal watakuwa Mayahudi elfu sabini wanaovaa hariri. Wachawi wa kiyahudi na watabiri wanaodanganya watu watakuwa pamoja naye.’
- ‘Mayahudi elfu sabini wa Isfahan wanaovaa hariri watakuwa wafuasi wa Dajjal.’
- ‘Watu wenye uchu (wa madaraka, utajiri,...) na tamaa ya Dunia. Wako watu watakaomfuata pamoja na kwamba wanajua Dajjal ni kafiri ilimuradi wapate chakula.

Imani ya Mayahudi kwa Dajjal:

Kwa Mayahudi, Dajjal atatizamwa kuwa ni kiongozi mkubwa. Watamuona kuwa yeye ndiye yule Masihi Mwokozi aliyetabiriwa katika Taurati na Zaburi...

Sababu hasa ya Mayahudi kumwamini Dajjal ni uadui wao dhidi ya Uislamu. Na bila shaka haitachukua muda Dajjal atapigana na Waisalamu, na hii ndiyo lengo la Mayahudi/mazayuni.

Dalili za kudhihiri Dajjal:

Miongoni mwa dalili za kudhihiri Dajjal ni: Kuenea kwa ukandamizaji, dhulma, rushwa, upotovu, unyang'anyi, uhasama, tabia mbaya, na maovu mengine mengi. Mtume (saww) anasema: 'Miaka mitano kabla ya kutokeza Dajjal, kutakuwepo ukame na hakuna chochote kitakachomea. Wanyama wote wenye kwato wataangamia.' Katika hali kama hiyo ambapo njaa itaangamiza watu na teknolojia haitafua dafu katika uzalishaji ndipo Dajjal atakuja na chakula ili awapotoshe watu.

Kudhihiri:

Siku ya kwanza atakapodhihiri, Dajjal atadai uungu. Wanaharamu elfu sabini Mayahudi, walevi, wanamuziki, waimbaji, mabedui na wanawake watamkubali na kumfuata.

Dajjal atahalalisha uzinifu na kulawiti na kila aina ya maovu na uchafu. Watu pia na watoto watafanya uzinzi na uchafu hadharani, barabarani. Wafuasi wa Dajjal watakula sana nyama ya nguruwe, kunywa pombe na kufanya kila aina ya haramu.

Hazina za Dunia chini ya Dajjal:

Kwa kuwa na uwezo mkubwa wa uchawi, Dajjal atamiliki hazina za ardhi. Ataamrisha sehemu yenye hazina itapike hazina yake na hazina hiyo itamwagwa juu ya ardhi mara moja. Ataaamrisha ardhi ioteshe mimea na mara moja ardhi hiyo itajaa mimea. Dajjal atatumia uchawi na mazingaombwe kuwapotosha watu wasio na elimu na imani.

Kuuliwa kwa Dajjal:

Dajjal atasimama kupambana na Mwenyezi Mungu. Atasimika nidhamu ya ufisadi na uharibifu. Pindi uharibifu utakapopindukia mipaka, Dajjal atauliwa na Baqiyatullah al-Aadham, Imam Mahdi (a.t.f.).

Mazingatio :

1. Nidhamu ya kidajjali inafanya kazi na kuandaa ujio wake.
2. Viongozi wa harakati za Dajjal ni Mayahudi.
3. Mbinu za kishetani: **Miujiza na maajabu.**

Sufyaniy

Huyu ndiye adui hatari dhidi ya Imam (as). Nyuma yake yatakuwa majeshi yote ya ukafiri dhidi ya haki. Kutokeza kwake ni jambo ambalo halina budi.

Nasaba yake:

Ameitwa Sufyaniy kwa sababu nasaba yake yatokana na Khalid bin Yazid bin Muawiya bin Abu Sufyan adui mkubwa wa Mtukufu Mtume (saww). Pia anaitwa mtoto wa mwanamke mla ini kwa kumnasibisha na Bibi yake mke wa Abu Sufyan, Hindi, aliyetafuna ini la Sayyidna Hamza katika vita vya Uhud. Atakuja akiwa na uadui wa jadi dhidi ya Mtume (saww) na Ahlul Bayt (as).

Hulka ya Sufyaniy:

Sufyaniy atakuwa ni mtu fatani⁵³ mwenye silika ya shari na ukandamizaji. Ni mtu muovu wa kupindukia, katili, khabithi kama yeye hakuna, adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Imam Mahdi (as). Mnafiki mkubwa atajidhihirisha mwenye dini na ibada wakati

⁵³ Mwenye kuhadaa, fitna kubwa, mdanganyifu,

yeye ni kibaraka wa Manasara na Mayahudi.⁵⁴ Ataua ulamaa na watu wema. Atamuua kila anayemhalifu, anawakata kwa misumeno, anawachemsha ndani ya masufuria, hata watoto wadogo, anapasua tumbo za wanawake. Atakuja hadharani na kumshika mwanamke na kuwatupia wafuasi wake wambake. Watambaka barabarani na kumchana tumbo lake na kumtoa kitoto chake...Ni mtu maluuni mbin-guni na ardhini na katili sana kuliko yeyote yule. Malezi yake na tabia zake ni za Kimagharibi. Mwelekeo wake na siasa yake itakuwa ni ya Kimagharibi kwa faida yao na Mayahudi.

Siasa yake:

Siasa yake itakuwa ni kujenga na kutilia nguvu fitna za kimadhehebu baina ya Waislamu na hasa kuwapiganisha Sunni na Shia chini ya bendera ya kuhifadhi na kulinda na kunusuru Usunni... wakati ambapo yeye yuko pamoja na maimamu wa makafiri wa Magharibi na Mayahudi na mbwa wao.⁵⁵

⁵⁴ Hii ndio hulka ya watawala wengi katika nchi za Kiislamu hivi sasa. Wamechota mali za Waislamu na kuzilundika katika mabenki Ulaya na Marekani. Wako tayari kutekeleza siasa ya Magharibi ya kuangamiza Uislamu kwa maslahi ya mayahudi. Ulimwengu ume-shuhudia kwa majonzi makubwa (29.12.2008), Israeli ikiandama Hamas kwa kuipiga Gaza kwa makombora na kufanya kila aina ya unyama dhidi ya Waislamu bila kujali haki za binadamu. Watawala wa nchi za kiislamu wamenyamaza... Bali viongozi wa Misri wameshirikiana na Israeli kuwakamata wanaharakati wa Hamas walioko Misri, na Misri imefunga mpaka wa Rafah kuzuwira kila msaada kuwafikia Hamas. La ajabu, Misri inajenga ukuta wa chuma kuzuia njia za chini ya ardhi zinazotumiwa na Hamas. Yote hayo ni kuwaridhisha mabwana wao mayahudi kwa kuwaangamiza Waislamu!?

⁵⁵ Haya ndiyo ambayo tunayashuhudia hivi sasa huko Iraq. Masunni na Mashia walikaa kwa amani na usalama, wameoana, wameshirikiana, kwa miaka yote. Lakini baada ya Shetani kuingia Iraq, mauaji ya kujitoa muhanga yasiochagua mtoto wala mzee, ugaidi, kubomoa misikiti,... yamekuwa mambo ya kawaida. Huu ni Uislamu aina gani au jihadi sampuli gani inayoruhusu mtu kuuu watoto na vikongwe pasi na hatia, kuvunja misikiti kwa sababu za kimadhehebu? Hizi ni itikadi za kiwahabbi na sera ambazo zinachochea na mashekhe wao za kuwakufurisha Waislamu kwa ujumla kwa sababu ya hitilafu katika itikadi kama vile kuzuru makaburi ya mawalii, kutawasali, kutabarruku...Kwa kutumia akili haya ni maswali yanahitaji majibu:

Atakapoingia Kufah Iraq atatoa amri: “Atakayekuja na kichwa cha Shia wa Ali atapewa Dirham elfu moja.” Jirani atamrukia jirani mwenzie na kusema huyu ni mmoja wao...

Mapambano yake na Utawala wake :

Atatokea jangwani baina ya Sham na Makka. Atapigana kwanza katika Syria kusimamisha utawala wake kwa miezi sita atateka

- 1 - Ni kwa ushahidi gani mawahabbi wanaweza kudai kwamba madhehebu yao ni sahihi? Je wana muhuri wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake? Bali ukweli, wao ni wafuasi wa Shekhe mmoja Muhammad Abdulwahhab () aliyefuata mtazamo wa Shaykh Ibn Taymiyyah () ambaye alikuwa anafuata madhehebu ya Ahmad bin Hambal. Muhammad Abdulwahhab alipozuka na itikadi zake za upotoshi, mashekhe na ulamaa wote, masunni kwa mashia walisimama kupinga upotofu wake kwa hoja za Qur’ani na Sunna. Vitabu vingi vimeandikwa kuelezea upotofu huo. Tukirudi nyuma je ni wapi Ahmad bin Hambal alitoa fatwa ya kuwakufurisha wasio mahambali? Hilo halipo kwa sababu yeye kama Aalim lazima aheshimu fatwa za ulamaa wengine. Vinginevyo atakuwa amejitangaza kuwa ni mtume mpya.
- 2 - Ikiwa mawahabbi wanadai wako sahihi, wengine pia wanadai wako sahihi kwa hoja na dalili. Sasa suluhisho ni nini? Je ni kulazimisha na kutumia nguvu hadi kuua? Kwa nini mawahabbi wasiweke makongamano ya kimataifa na wakawalingania watu kwa ustaarabu wa Qur’ani kwa kujadiliana vizuri kama vile Qur’ani inavyoelekeza () ?
- 3 - Ikiwa mawahabbi wataendelea na sera za kuwakufurisha Waislamu na hivyo kuwaua, je Waislamu wengine wakitoa fatwa ya kuwaua mawahabbi, hatima ya Uislamu itakuwaje? Hatima ni kuuana Waislamu na kupoteza nguvu na umoja kama wanavyotaka makafiri na mazayuni, na wala siyo uwahabbi kusimama na madhehebu zingine kutoweka. Je mawahabbi watafanikiwa kuwamaliza Waislamu wote wenye itikadi dhidi yao? Je historia inaonesha je ?
- 4 - Je hivi ni Uislamu au haki kumbukumu mtu bila ya kumpa dalili ambaye anayefuata madhehebu ya wazazi wake? Uislamu ni rehema na siyo nakma kuangamiza watu. Mtume aliishi na makafiri na kuwaheshimu na kuwastahamilia. Masahaba watukufu waliomfuata Mtume walikuwa wakiabudu masanamu. Mtume hakutuma majeshi ya kuwazimisha watu kufuata Uislamu na kuwaangamiza wasio Waislamu na kuua bila kujali wasio na hatia. Kwa hiyo, fatwa za ulamaa wa kiwahhabi za kuwakufurisha mashia na Waislamu wengine hazina misingi ya dini wala akili bali ni kutekeleza agenda ya maadui wa Uislamu ambayo lengo ni kumaliza nguvu za Uislamu kwa kuwapiganisha Waislamu. Waislamu tuamke na tuache ushabiki. Tusiwe watu ambao tunatumika kutekeleza agenda za madajjali kwa kupitia mawakala wao waliojificha ndani ya majoho ya dini. Ikiwa madhehebu yako ndiyo ya haki, basi wajibu wako kama inavyoagiza Qur’ani, jitokeze na uwalinganie waliopotea kwa hekima na mawaidha yalio mazuri, na sio kujilipua na kuua halaiki ya watoto, vikongwe, na wanawake wasio na hatia.

Demascus, Hims, Palestina, Jordan na Qansarayn. Baada ya kusimika utawala wake ataelekeza majeshi yake Iraq na Hijaz (kuelekea Madina na Makka).

Huko Iraq:

Sufyany ataishambulia Iraq na kuiteka. Hatapata upinzani wowote. Atawatesa na kuwadhiki na kuwaua watu wake hususan wapenzi wa Imam Mahdi (as) na Ahlul Bayt (as). Wataingia Baghdad na kufanya mauaji ya halaiki. Kisha wataelekea Kufa na Basra. Watazingira miji na kufanya mauaji na kila aina ya maasi. Kila haramu wataifanya halali. Kwa sababu ya chuki dhidi ya Mtume na Ahlul Bayt, watamuua kila aliye na jina la Ahmad, Muhammad, Ali, Ja'far, Hamza, Hasan, Husayn, Fatima, Zainab, Ruqaiyyah, Ummu Kulthum, Khadija au Aatika.

Majeshi yanayomfuata Imam (as) – majeshi ya Yamany na Kurasany - yakiwa na bendera nyeusi yataingia Iraq na majeshi ya Sufyany yataogopa na kuondoka.

Baada ya kushindwa huko, Sufyany atarudi nyuma Sham ambapo Imam Mahdi (as) atamfuata na kupambana naye katika vita vya ukombozi mkubwa wa Quds.

Huko Hijaz:

Jeshi la Sufyany litaingia Madina na kutekeleza muradi wake (nao ni mauwaji ya halaiki...). Baada ya hapo litaelekea Makka ili kumaliza Imam Mahdi (a.t.f.) na wafuasi wake. Litakapofika jangwani katikati, mnadi atawaita naye ni Jibril (as). Jeshi lote litaangamia kwa kutitia ndani ya ardhi. Watasalimika watu wawili ambao mmoja ataelekea Makka kumpa Imam Mahdi (as) bishara njema ya kuanga-

mia jeshi la Sufyaniy, na mwigine atarudi kumpasha habari Sufyaniy na kumuonya.

Muda wa utawala wa Sufyaniy:

Utawala wake utadumu kwa kipindi cha miezi minane/tisa. Katika kipindi hiki kifupi atafanya uovu na ukatili wa kupindukia mipaka, kama tulivyoelezea hapo juu. Kudhihiri kwake hadi kuangamia itachukua miezi kumi na tano. Miezi sita ataitumia kupigana kusimamisha utawala wake.

4. Bendera Nyeusi kutokea Khorasan:

Mojawapo ya alama thabiti kabla ya kudhihiri Imam (as) ni kuwepo kwa jeshi la Kiislamu kutoka Khorasan ambalo litaweka juu bendera nyeusi. Khorasan ni jimbo liko Mashariki Kaskazini mwa Iran. Jeshi hili litaelekea Kufa. Imam Mahdi (a.s.) atakapodhihiri Makka, jeshi hili litakwenda kumpa kiapo cha utii.

5. Sauti kutoka mbinguni:

Hii ni sauti ya malaika itakayosikika kutoka mbinguni ikitoa bishara njema ya kudhihiri Imam Mahdi (as) na kuwataka watu wamfuate na kumnusuru. Watu wote duniani wataisikia kwa lugha zao. Waliolala wataamka. Hii sauti itasikika mara tatu katika mwezi wa Rajab na mara nyingine usiku wa 23 wa mwezi wa Ramadhani. Ama Imam (as) atadhihiri siku ya Ashura. Ujumbe katika mwito huu ni: “Laana ipo juu ya madhalimu, Mahdi amedhihiri ili kuangamiza madhalimu...”

Hadithi zinasema:

- Imam Mahdi (as) atadhihiri na juu yake kutakuweko na wingu ndani yake yumo malaika ambaye atatangaza: ‘Huyu ndiye Khalifa wa Mwenyezi Mungu na Mahdi, basi mtiini.’

- Mtangazaji atatangaza kutoka mbinguni: ‘Jueni ya kwamba Hujjah wa Mwenyezi Mungu amedhihiri karibu na Nyumba ya Mwenyezi Mungu. Haki imo ndani yake na pamoja naye. Nyote mfuateni. Hakika haki ipo pamoja na kizazi cha Mtume (Ahlul Bayt).’

6. Kuteremka Nabii Isa (as) na kuswali nyuma ya Imam Mahdi (a.t.f.) :

Ni miongoni mwa alama thabiti, atateremka Nabii Isa (as) na kula kiapo cha utii kwa Imam (a.t.f.) na kuswali nyuma yake. Wakristo watakapoona hivyo wataamini Uislamu na kuacha imani ya kikristo. Atavunja msalaba na kuua nguruwe na kumwangamiza Dajjal, vijana wa pangoni watatembea nyuma. Atakuwa waziri na msaidizi na mlinzi wa Imam Mahdi (a.t.f.).

7. Al-Yamaniy :

Pia ni moja katika alama za kudhihiri Imam Mahdi (as). Sufyaniy, Yamaniy na Khurasaniy wote watatokeza katika mwaka mmoja, mwezi mmoja na siku moja. Bendera ya Yamaniy itakuwa ni ya uongovu na haki zaidi kuliko bendera yeyote ile.

8. Kupasuka ardhi hapo Baidaa:

9 Kuuliwa Nafsi Zakiyya:

Atauliwa siku 15 kabla ya kudhihiri Imam Mahdi (as). Imam atamwamuru awaite watu kwa niaba yake. Lakini watamuua katikati ya Masjidul Haraam pembezoni mwa Kaaba baina ya Rukni na Maqaam.

10. Sayyid Hasaniy:

Ni miongoni mwa masharifu (masayyid) wa kizazi cha Imam Hasan (as). Atatokea Qazwin na kuanza harakati zake ili kusimamisha Sheria ya Mwenyezi Mungu na kurekebisha hali ya Waislamu na kutokomeza dhulma. Watu wa Qazwin wataungana naye na pia hazina ya Twaliqaan (watu waumini wenye msimamo thabiti kama vipande vikubwa vya chuma). Wataongezeka wafuasi wake na kusimamisha dola adilifu hadi mipaka ya Iraq. Atakapopata habari ya jeshi la Imam kuelekea Kufa ataondoka na jeshi lake na kwenda kumlaki. Kwa ajili ya kutaka utulivu wa jeshi lake atamuomba Imam mirathi ya Mitume.

Mirathi ya Mitume:

Bila shaka Imam Mahdi (a.t.f.) kwa daraja yake adhimu ndiyo mwenye mirathi ya Mitume. Katika mirathi hiyo ni:

- Fimbo ya Nabii Musa (as),
- Pete ya Nabii Sulayman (as),
- Kilemba cha Mtume (saww), upanga wa Dhulfiqar, pete...

SERIKALI YA KIISLAMU ZAMA ZA GHAYBA, KABLA YA KUDHIHIRI IMAM MAHDI (A.T.F.)

Zipo riwaya zinazoashiria kwamba kabla ya kudhihiri Imam itasimama dola ya Kiislamu ambayo itaweka msingi wa serikali ya Imam Mahdi (a.t.f.). Mtume (saww) alisema: “Watatokeza watu kutoka Mashariki na watasawazisha njia ya utawala wa Imam Mahdi (as).” (Ibnu Maajah, *Kanzul Ummal*).

- Kutokeza bendera nyeusi Mashariki ili kunusuru haki na baadaye kukabidhi uongozi kwa Mahdi atakapodhihiri.
- Wafursi watapigana na Waarabu kwa ajili ya dini zama za mwisho.
- Mapinduzi ya Kiislamu yataanzia mji wa Qum zama za mwisho.

2. MAPAMBANO DHIDI YA DHULMA

Katika kipindi kifupi, wafuasi wa Imam Mahdi (a.t.f) watakusanyika chini ya bendera yake na kuwa tayari kung'oa kila aina ya utawala dhalimu. Askari wa Imam watakuwa na nguvu na mioyo madhubuti kuliko vipande vya chuma. Watapambana bila kurudi nyuma hadi watakapofyeka kila utawala dhalimu. Watawala mataghuti watakusanya nguvu zao za uovu na wafuasi wao, lakini askari wa haki watawafyeka. Woga na taharuki utawajaa wote watakaosalia na hivyo kusalimu amri...

VITA VYA DUNIA

Hadithi zinaashiria kwamba karibu na kutokeza Imam Mahdi (a.t.f.) kutakuwa na:

- Mauti nyeupe, kutokeza tauni,⁵⁶
- Mauti nyekundu, vita, kuwepo hali ya hofu kubwa, balaa, fitna na watu kumalizana. Watu wa Mashariki na Magharibi watahitilafiana na kufuatwa na Waislamu. Maafa haya yataangamiza theluthi mbili za watu duniani.

⁵⁶ Tauni: ugonjwa unaoambukiza unaosababishwa na aina ya bacteria. Katika historia ugonjwa huu umeua watu sana kwa kukosa kujua sababu na chanzo chake. Pia neno tauni linaweza kutumika kwa maana ya ugonjwa unaoambukiza na kuua watu wengi.

HALI YA HIJAZ KARIBU NA KUDHIHIRI IMAM

Vurugu za kisiasa na kuvunjika utawala wa miaka na kubadilika kuwa utawala wa miezi na siku:

Litatokea hili baada ya kuuliwa mfalme ambaye jina lake ni Abdullah. Baada yake kila watakapochagua mfalme basi, hatofikisha mwaka. Baada ya miezi watachagua mwingine. Hali itaendelea hadi atakapodihiri Imam Mahdi (as). Sababu ya mgogoro huo wa utawala utakuwa ni ukabila katika familia ya kifalme. Mgogoro huo utasababisha vita baina ya Magharibi na Mashariki....

Kisha atatokeza Sufyaniy:

Kisha ni Sauti kutoka mbinguni. Tangazo hili litawapa faraja Waumini na watu watajenga mahaba wakimtarajia Imam Mahdi (a.t.f.). Hili litasababisha taharuki katika kambi ya ukafiri. Kwa sababu hiyo jeshi la Sufyaniy litaingia Hijaz na kumsaka Imam katika mji wa Madina. Kila aliye Hashimiy, kizazi cha Mtume (saww) (sharifu, sayyid,) atashikwa pamoja na Mashia wao. Watauliwa wengi na wengine kuwekwa kizuwizini. Imam ataondoka Madina na kukimbilia Makka. Akiwa Makka, Imam ataendelea kuwasiliana na baadhi ya wafuasi wake mpaka pale atakapotangaza kudhihiri. Kabla ya hilo kutadhihiri moto mkubwa wa njano na mwekundu utakaotokeza Hijaz (au Mashariki) na kubakia kwa siku kadhaa.

Muda na Mahala pa Kudhihiri Imam wa Zama (a.t.f.): Wapi?

Atadhihiri Makka. Ataingia ndani ya Masjidul Haraam na kuswali raka nne hapo Maqaam Ibrahim. Atasimama baina ya Rukn na

Maqam ambapo ni mahala patakatifu, na mtu mmoja atasimama mbele yake akinadi: ‘Kiapo cha utii! Kiapo cha utii!’ Wasaidizi wa Imam kutoka kote ulimwenguni wataelekea huko aliko na kula kiapo cha utii kwake. Jibril (as) ndiye wa kwanza atakayempa kiapo cha utii. Wakati watakapokuwa wanakula kiapo cha utii, sauti itasikika kutoka ghaibuni ikitangaza: **“Huyu ni Khalifa wa Allah, Mahdi, msikilizeni na mtiini.”**

Wakati wa kudhihiri:

Itakuwa ni siku ya Jumamosi, katika mwezi wa Muharram. Itakuwa ni siku ya Ashura, siku aliyouliwa Imam Husayn (as). Atadhihiri wakati wa Swala ya Isha akiwa na bendera ya Mtume (saww), kanzu yake, upanga wake, alama, nuru na bayana. Baada ya kuswali Isha atawaita watu na kuwahutubia...

Atakapomaliza kuswali Swala ya Isha, atapaza sauti yake na kusema:

“Enyi watu: Ninawakumbusheni pindi mtakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu wakati amewakamilishieni hoja juu yenu: Mitume walitumwa na vitabu vilikwisha teremshwa na walikuamuruni kamwe msimshirikishe Mwenyezi Mungu na chochote na mumtii Allah na Mtume Wake. Chochote ambacho Qur’ani imekiweka hai basi nanyi kiwekeni hai, na chochote ambacho Qur’ani imekibomoa, basi nanyi mkibomoe. Basi muwe wasaidizi wa uongofu na daima mjiipambe kwa uchamungu kwa sababu karibu dunia itamalizika. Ninawaiteni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na kutenda kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kuangamiza batili na kuhuisha Sunnah ya Mtume (saww)...” – Maadui watajaribu kumuua, lakini wafuasi wa Imam (a.t.f.) watadhibiti hali hiyo na kuiweka Makka yote chini ya mamlaka yao.

KUHUTUBIA MATAIFA YOTE

Siku ya Ashura, Jumamosi, Imam (a.t.f.) ataingia Masjidul Haraam na kutilia mkazo utandawazi wa harakati zake. Atayahutubia mataifa yote ulimwenguni - ya Kiislamu na yasio ya Kiislamu - kwa lugha zao tofauti . Atawaomba wote wamnusuru dhidi ya makafiri na madhalimu. Maimamu wa ukafiri – kote waliko, Mashariki na Magharibi - watatahayari na kulaani harakati hizo.

Sufyaniy atatuma jeshi lake kutoka Madina liende Makka kumaliza harakati za Imam Mahdi (as). Lakini muujiza mkubwa al-ioutabiri Mtume (saww) utatokea nao ni kwamba Mwenyezi Mungu ataliangamiza jeshi hilo baina ya Makka na Madina, mahala panapoitwa Bidaa. Imam (a.t.f.) ataondoka Makka baada ya kumtawaza gavana na kuelekea Madina akiwa na jeshi la takriban watu 10,000. Atarejea kwa kuuliwa gavana wake Makka. Na baada ya kuwaua wauaji ataelekea Madina. Atapita mahala ambapo jeshi la Sufyaniy litamezwa na ardhi.

KUIKOMBOA MADINA NA HIJAZ

Ndani ya Madina atasafisha upinzani na Madina itasalimu amri. Baada ya hapo utawala dhaifu wa Hijaz utaporomoka na kufanya utawala wake kuenea bara Arabu yote hadi Iran. Tukio hili litasababisha mtikisiko mkubwa kwa dola zenye nguvu za Mashariki, Magharibi, Mayahudi na makafiri wote ambao Uislamu ndio tishio kwao.

IRAQ NA IRAN

Vita vya Qirqiisia:

Vita vitajumlisha mapambano baina ya majeshi ya kikafiri ambayo yatakuwa yanapigania hazina ya mali itakayokuwa imepatikana mahala hapo. Matokeo ya vita hivyo itakuwa ni kudhoofika nguvu za kikafiri.

Mapambano ya Ahwaaz, Khurasani, Shuayb bin Saleh, watokea Iran:

Imam Mahdi baada ya kuikomboa Hijaz ataelekea 'BAIDHAA ISWTWAKHARA na kukutana na jeshi la Khurasani, na kuelekeza mapambano dhidi ya Sufyaniy na jeshi lake likisaidiwa na Urumi (dola za Magharibi). Baada ya vita kali, majeshi ya Sufyaniy yatashindwa. Hili litakuwa na taathira kubwa kwa kusukuma mkondo wa wapenzi wa Imam Mahdi (as) baina ya Waislamu kote walipo na kuwafanya kuharakisha kujiunga na jeshi lake. Kuanzia hapo Khurasani na Shuayb watakuwa miongoni mwa wafuasi maalumu (muhtasi) wa Imam Mahdi, na Shuayb atakuwa Kamanda Mkuu wa majeshi ya Imam Mahdi. Jeshi la Khurasani ndilo litakuwa la kutegemewa katika kusafisha upinzani Irak na kupambana na Turk (Urusi) na kisha kuelekeza mashambulizi makubwa kuiteka Quds na Palestina.

Imam ataingia Kufa, Najaf na Karbala na kuifanya Kufa kuwa mji mkuu na kitovu cha harakati zake. Ndani ya Kufa atajenga msikiti wa Ijumaa wa dunia ambao utakuwa na milango elfu moja. Huu ni msikiti ambao wataswali watu kutoka sehemu mbalimbali kutoka kote duniani ili kupata swala nyuma ya Mtakaswa, Mbarikiwa mtoto wa Mtume (saww). Akiwa Iraq, atatuma majeshi yake kwanza dhidi

ya Urusi na kuwashinda. Pia atatuma majeshi yake China, Uturuki... ili kusimika utawala wake na kuweka usalama upande wa Mashariki.

KUIVAMIA SYRIA NA KUIKOMBOA QUDS

Kiyama hakitasimama mpaka Waislamu wapigane na Mayahudi. Waislamu watawaua mpaka Yahudi atajificha nyuma ya jiwe na mti! Lakini pia jiwe na mti vitanena: ‘Ewe Mwislamu! Huyu hapa Yahudi nyuma yangu, njoo haraka umuue!...’⁵⁷

Baada ya kuweka mambo sawa ataelekea yeye mwenyewe na jeshi lake Sham na kuweka kambi **Marja ‘Adhraa**, eneo lililo umbali wa takriban km 30 na Damascus kujiandaa kupambana na Sufyaniy, Mayahudi na Urumi.

Watu wa Sham wakiwa ni Waislamu, wengi watamuunga mko-no Imam Mahdi (as) na hivyo Sufyaniy kujikuta hana usaidizi wa umma. Atarejea nyuma na kupiga kambi yake mahala panapoitwa **Waadi Ramlah**, ambapo majeshi ya Magharibi yatateremkia kum-saidia. Kabla ya mapambano, Imam atamtaka Sufyaniy wakutane. Imam atamwathiri na kumfanya Sufyaniy ale kiapo cha utii kwake.

⁵⁷ Musnad Ahmad b. Hambal, Muslim, Tirmidhiy, Bukhariy. Hadithi hii ni kioo cha ukweli kuhusu itikadi, hulka ya mayahudi na mwisho wao. Hivi sasa sote tunashuhudia unyama, ukatili na ushenzi unaofanywa na watu hawa dhidi ya Wapalestina na ubinadamu kwa ujumla. Uovu na ushetani wa watu hawa hauna mithili katika historia ya binadamu. Ajabu wanadai kupepea bendera ya Nabi Daudi (a.s.) wakisahau kwamba katika Zaburi anasema: *“Mwisho wa waovu ni kuangamia, na wema watarithi dunia”*. Pamoja na kutawala dunia na kuwa na uwezo na hazina zote za fedha, sayansi na teknolojia, na kufikia daraja ya kutangaza uungu wa dunia, siku ipo karibu ambapo watashindwa na dunia kuwakataa kwa uovu wao na hivyo miti yote kuteleza na kujikuta ni madhalili, duni hawana hata pakujificha isipokua nyuma ya jiwe na mti!!! Pia miti na mawe it-awakana waovu hawa. Itawafichua ili waangamizwe makafiri hawa. Mwenyezi Mungu si Athumani, kwake hakuna ‘mtoto’ wala ‘kabila teule’. Huu ni uzushi na uzindiqi. Wote mitume waliotumwa kwa mayahudi, Nabi Musa, Daudi, Isa (wote juu yao amani), wamefundisha kwamba *‘utoto’ na ‘uteule’ ni kwa matendo mema na kumcha Mola, ama waovu lazima wataangamia.*

Lakini baada ya kurejea kambini kwake, jamaa zake na nguvu zilizo nyuma yake – Mayahudi na Urumi - watamkemea na kumrejsha kwenye azma yake ya kupigana.

Sufyaniy ataandaa majeshi yake tayari kupambana na Imam Mahdi (as). Uwanja wa Mapambano haya makubwa utajumlisha ukanda kuanzia Akka, Sur hadi Antokia. Kwa ndani utaanzia Damascus, Tiberia hadi Jerusalem.

Imam Mahdi (a.t.f) akiwa na msaada wa Mwenyezi Mungu, malaika Jibril (as) akiwa kuliani na malaika Mikail (as) akiwa kushotoni na halaiki ya watu wakijiunga naye kutoka kila sehemu, atapambana na maluumi Sufyaniy hapo Tiberia. Gadhabu (laana) ya Mwenyezi Mungu itamtermkia Sufyaniy na jeshi lake, jeshi lake lote litaangamia. Sufyaniy atakimbia lakini atashikwa na Sabbah mmoja kati ya wafuasi wa Imam. Akiwa mbele ya Imam, Sufyaniy atamuomba Imam Mahdi (a.t.f) amuonee huruma asimuu na kuahidi kwamba atakuwa mfuasi wake na kupigana na maadui wake. Lakini kwa maombi ya masahaba wa Imam, ombi hilo la mtu huyo muovu adui wa Mtume (saww) na kizazi chake, aliyewa kwa ukatili mkubwa waja wema, litakataliwa. Sabbah na wenzake watampeleka Sufyaniy chini ya mti na kumkata kichwa chake... Allahu Akbar!

Jamaa zake na makada wake baada ya kuuliwa Sufyaniy watakimbia Rum (Magharibi). Imam Mahdi (as) ataitaka Rum iwarejeshwe. Watarejeshwa na watauliwa.

Hivyo ndivyo Quds (Jerusalem) itakavyokombolewa... Kwa kuangamia Sufyaniy na jeshi lake, nguvu za Uyahudi na Urumi zitakuwa zimeshindwa, na hivyo kufungua milango ya ulimwengu wa Magharibi...

KUTEREMKA NABII ISA (AS) KUTOKA MBINGUNI

Waislamu wamekubaliana kwamba Akhirizaman Nabii Isa (as) atateremka kutoka mbinguni. Wengi katika wanatafsiri kwa madhumuni hayo wamefasiri aya 4:159:

وَإِن مِّنْ أَهْلٍ أَلَكْتَبِ إِلَّا لِيُؤْمِنَنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ ۗ وَيَوْمَ
الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِدًا

“Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.”

Kwa hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Imam Baqir (as), yeye alisema: “Atateremka duniani kabla ya siku ya Kiyama. Hatobakia yeyote mfuasi wa mila (dini fulani), yahudi wala mkristo ila atamuamini kabla ya kufa kwake. Nabii Isa (as) atarekebisha kila uzushi ulioingizwa ndani ya dini. Ataswali nyuma ya Mahdi na kufuata Uislamu.

KUULIWA DAJJAL

Baada ya kusimama dola moja chini ya Imam Mahdi (as) hapo ndipo atasimama Dajjal na fitna yake kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu ya zama hizo. Watamfuata Mayahudi ambao kwa uhakika ndiyo walio nyuma yake. Zipo riwaya zinasema Dajjal atauliwa na Isa (as) na kauli nyingine ni kwamba atauliwa na Waislamu chini ya uongozi wa Imam Mahdi (as).

MWAFKA (SULUHU) NA NCHI ZA MAGHARIBI NA VITA KUU

Imam atawekeana mkataba wa amani na dola za Magharibi na hivyo kuchukua mkondo wa kawaida katika kubadilisha mtazamo wa ki-siasa na kiakida wa watu. Baada ya muda mfupi watavunja mwafaka huo na hivyo kusimamisha jeshi kubwa na vita kubwa zaidi kuliko ile ya Quds. Tukio hili linafanana na lile la Hundaybiyah ambalo Mwenyezi Mungu aliliita Ushindi Ulio Wazi.

WATU WA MAGHARIBI WAINGIA NDANI YA UISLAMU

Ushindi wa majeshi ya Kiislamu chini ya uongozi wa Imam Mahdi (as) hapo Palestina na Sham utakuwa na athari kubwa sana kwa watu wa Magharibi. Wengi wataathirika na Nabii Isa (as) na Imam Mahdi (as) na kuwapa nguvu wafuasi wao na mkondo huo ndiyo utaka-oangusha serikali za kidhalimu na kikafiri na kutangaza kujiunga na dola ya Imam Mahdi (as).

KUENEA UISLAMU KOTE DUNIANI

Aya ifuatao inaashiria kwamba Uislamu utakuja kuenea ulimwengu kote:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى
الدِّينِ كُلِّهِ ۗ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٩٣﴾

“Yeye ndiye aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na dini ya haki ili ipate kushinda dini zote, ijapokwa washirikina wamechukia.”

(9:33).

Hadithi zinaonyesha kwamba hili litakamilika zama za Imam Mahdi (as). “Wote, awe myahudi, mnasara (mkristo) na mwenye dini, wataingia ndani ya Uislamu. Jizya itaondolewa (hatokubaliwa yeyote kulipa jizya), atavunja msalaba na kuua nguruwe.” “Hata kama kafiri au mushrik atajificha ndani ya jabali, litamuita muumini na kumuambia: ‘Ewe muumini huyu hapa kafiri ndani yangu, muue.’ Atakuja na atamuua.” Kwa hiyo hatobakia yeyote juu ya ardhi ila atakiri ushindi wa Uislamu na Mtume (saww).

Uislamu kuenea Dunia nzima ni jambo ambalo lazima litatokea kwa sababu nyingi za kiitikadi, kiuchumi, kisiasa kama ilivyoielezwa hapo kabla:

1. Uislamu ni dini inayokubaliana na maumbile ya mwanadamu na kukidhi mahitaji yake yote ya kiroho na kimwili. Wanadamu hivi sasa wanasumbuliwa na mfumo wa kibepari na ukanamungu ambao umeleta maafa makubwa. Kwa kuwa mfumo huo umeshindwa kuleta amani na utulivu, na utaendelea kusababisha maafa makubwa, wanadamu watajikuta wanatahayari wakitafuta njia ya uokovu... Baada ya mifumo yote batili kushindwa, wanadamu watakuwa hawana budi ila kurejea kwenye *Allahkrasia* (mfumo wa serikali ya Mwenyezi Mungu).
2. Uislamu aliousimamisha Mtume (saww), ulithibitisha kwamba unaweza kujenga jamii yenye maendeleo na amani. Uislamu baada ya muda mchache uliweza kuongoza maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia ulimwenguni.
3. Hivi sasa Mapinduzi ya Kiislamu huko Iran yameonyesha maajabu ya nguvu zake. Baada ya miaka 30 yamebadilisha nchi hiyo kutoka chini ya utawala wa kibeberu na kuwa nchi huru yenye maendeleo makubwa kisayansi na kiteknolojia kiasi cha

kuwa tishio kubwa kwa nchi za Magharibi ambazo lengo ni unyonyaji na ukoloni mamboleo. Mafanikio yote haya yamefikiwa pamoja na kuwepo vita ya miaka minane dhidi ya Iraq, upinzani wa ndani, na juu ya yote vikwazo vya kimataifa. Hii ni nguvu ya Uislamu ambayo wanaishuhudia Waislamu na wasio Waislamu.

4. Atakapodhihiri Mahdi (a.t.f), atakuja na maajabu, ushindi na hoja ambazo zitawakinaisha watu wote kwamba yeye ndiye Khalifa wa Allah. Kwa Mayahudi na Wakrisro, atawaletea Tabuti, Taurati, Zaburi, Injili na vitabu vingine. Wengi watasalimu amri. Atakapoteremka Isa bin Maryam (as), miujiza atakayoifanya, wengi kati ya Wakristo watamkubali na kusalimu amri. Ushindi wa nguvu katika kila medani, kuuliwa Dajjal, Sufyaniy na makafiri wengine yatafanya watu wamkubali Mahdi (a.t.f.) na Uislamu.
5. Ulimwengu wa Kiislamu utakuwa na maendeleo ya kiuchumi, elimu, sayansi na teknolojia na kijamii kwa sababu ya uongozi bora na uadilifu na baraka za Imam na mawalii wake.

3. SERIKALI MOJA YA MUNGU DUNIANI YENYE HAKI NA UADILIFU

“Mahdi wetu atasaidiwa na haiba (inayotia woga) na kutiwa nguvu kwa ushindi. Ardhi itapasuka ili kumlaki na hazina za dunia zitadhihiri ili kumridhisha. Utawala wake utaenea Mashariki na Magharibi. Chini ya uongozi wake Uislamu utashinda kila dini, hata kama makafiri watachukia.” (3:150, 8:12, 9:26, 59:21) - **Imam Muhammad Baqir**

A. ALLAHKRASIA

Nidhamu ya Utawala wa Imam:

Utawala wake utaenea Dunia nzima, Mashariki na Magharibi. Hakuna amri itakayotekelezwa bila amri yake. Huu ni *utandawazi* wa nidhamu ya Mwenyezi Mungu. Imam atasimamisha Uislamu halisi na utamaduni wa tawhidi.

Allahkrasia: Uislamu unaainisha aina mbili za utawala: Allahkrasia na utaghuti. Ikiwa Demokrasia ni serikali ya watu kwa watu kwa ajili ya watu,⁵⁸ Allahkrasia ni serikali ya Allah, iliyowekwa na Allah, kwa ajili ya Allah.

Serikali ya Allah: Allah ndiye Mtawala na Mfalme. Yeye ndiye anayemchagua Khalifa Wake ili awahukumu watu kama anavyoridhia. Kiongozi kama huyu lazima awepo katika kila zama. Kiongozi huyu lazima awe na sifa za ukamilifu katika elimu, imani na maumbile. Kukosekana kwake ni kukanusha uadilifu wa Mwenyezi Mungu kwani ni sawa na kusema Mwenyezi Mungu anataka tusi-mamishe Tawhid, wakati nguzo ya Tawhid haipo nayo ni kiongozi mwadilifu.

Iliyowekwa Allah: Serikali inaongozwa kwa sheria Zake Allah kama alivyoziteremsha ndani ya Kitabu Chake. Serikali yoyote inayohukumu kwa sheria zisizo za Mwenyezi Mungu bila shaka ni serikali ya kitaghuti na kidhalimu.

Kwa ajili ya Allah: Mwenyezi Mungu ndiye Muumbaji na Mfalme pekee. Kwa hiyo lengo la serikali ni kusimamisha utawala wa Mwenyezi Mungu na siyo utawala wa watu au mtu binafsi. Nidhamu hii ndiyo aliyoiasisi Mtukufu Mtume (saww) na kutowe-

⁵⁸ Abraham Lincoln (1809-1865), rais wa 16 wa Marekani. Alisema '*Democracy is the government of the people, by the people, for the people*'. (Demokrasia ni serikali ya watu, iliyowekwa na watu, kwa ajili ya watu)

ka baada ya Uislamu kugeuzwa kuwa utawala wa kiukoo. Uislamu utarudi katika mfumo wake halisi wa awali.

Lengo la serikali na sera zake ni kueneza ukweli na haki na kueneza usalama na amani kwa watu wote. Sera zote zinasimama kwenye misingi miwili mikuu; Qur’ani na Sunnah. Utawala huu na aina hii ya uongozi ndio Mitume wote waliokuja kuwafundisha walimwengu katika kila zama za historia ya mwanadamu. Baadhi yao walifanikiwa kusimamisha serikali na kuhukumu kama vile: Nabii Yusuf (as), Talut (as), Nabii Dawud (as), Sulayman (as), DhulQarnayn (as), na pia Mtume (saww). Mfano wa utawala wa Allahkrasia hivi sasa katika zama zetu ni Serikali ya Kiislamu ya Iran.

Imam na msaada wa Malaika:

Atakapodhihiri, Imam atapata msaada wa Malaika; Malaika Jibrail (as) atatembea kuliani kwake, Mikail (as) kushotoni kwake, Israfil (as) mbele yake, na Izrail (as) nyuma yake, na Malaika wengine watamsaidia.

Sifa za masahaba wa Imam Mahdi (as):

Hawa ni hazina ya Mwenyezi Mungu ardhini, sio ya dhahabu wala fedha, bali ya imani, watu ambao ndio mfano halisi wa *Hizbullah* (kundi la Allah).

- Wenye upendo baina yao, nyoyo zao zimeungana.
- Hawana woga na chochote kile, mioyo yao itakuwa na nguvu kama chuma.
- Hawajioni kwamba ni wenye daraja pamoja na kujitoa muhanga katika njia ya Allah.
- Wapiganaji katika njia ya Allah. Thamani yao haijulikani duniani lakini inafahamika vizuri mbinguni.

- Usiku ni wenye kushughulika na ibada, na mchana ni wenye kupambana kama simba.
- Kila sahaba atakuwa na nguvu sawa na watu arobaini.
- Idadi yao ni 313 sawa na idadi ya wapiganaji wa vita vya Badr. Mwenyezi Mungu atawakusanya kutoka sehemu mbalimbali na watajumuika na kumpa kiapo cha utii Imam (as). Hii ndiyo maana ya Aya:

وَلِكُلِّ وِجْهَةٍ هُوَ مُوَلِّيهَا ۖ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ ۗ أَيْنَ مَا تَكُونُوا
يَأْتِ بِكُمْ اللَّهُ جَمِيعًا ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٤٨﴾

“Na kila mmoja ana mwelekeo anaouelekea. Basi shindaneni kufanya mema. Popote mtakapokuwa, Mwenyezi Mungu atawaleta nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mweza wa kila kitu.”

Masharti ya Imam wa Zama (as) wakati wa kiapo cha utii:

Kiapo cha utii kitatolewa kwa Imam baina ya Rukn na Maqam. Haya ni baadhi ya masharti ya Imam wakati wa kuchukua kiapo cha utii kutoka kwa wafuasi wake:

- Kamwe hawatakimbia,
- Kamwe hawataiba wala kufanya zinaa,
- Hawataua wala kuvunja hadhi ya mtu,
- Hawatasema kauli mbaya kwa Waislamu,
- Kamwe hawatashambulia nyumba yeyote wala kuua ila kwa sababu,
- Usivae dhahabu wala Hariri,

- Usivunje heshima ya msikiti wala kuzuia njia,
- Usiwadhulumu yatima wala kufanya njia kuwa si salama,
- Msitumie vitimbi na udanganyifu,
- Msinyang’anye mali ya yatima,
- Msilawiti, wala kunywa pombe, wala kunyang’anya haki,
- Msivunje ahadi na viapo,
- Msilundike ngano na shairi, dhahabu na fedha,
- Usimuue aliyeomba hifadhi kwako,
- Usimfuate aliyekimbia,
- Usimwage damu na kumshambulia aliyeumia,
- Vaa nguo ngumu na kusujudu juu ya udongo,
- Kula mkate mkavu na pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu,
- Weka manukato na kujiepusha na vitu vichafu, najisi,
- Msimuache mnafiki na kafiri,
- Amrisheni mema na katazeni mabaya,
- Fanyeni jihadi kwa kufuata amri za Mwenyezi Mungu.
- Mshika bendera wa Imam (as):

Mshika bendera wa Imam (as) atakuwa Shuayb bin Salih ambaye atakuja kutoka Khorasan akiwa ni kamanda wa jeshi la Khorasaniy. Bendera ya Imam Mahdi (a.t.f.) itaandikwa: Kiapo cha utii ni kwa Allah peke Yake. Kiapo cha utii ni kwa Imam Mahdi (a.t.f.), ambaye ndiye Khalifa wa Allah, bila shaka ni kiapo cha utii kwa Allah.

B. ZAMA ZA AMANI NA HAKI

أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ تَحِيَّ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ الْآيَاتِ
لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumewabainishia Ishara ili mpate kutia akili.”
(Suratul Hadid, 57:17).

“Ataijaza ardhi uadilifu na haki kama itakavyokuwa imejaa dhulma na jeuri.” – (Mtukufu Mtume (saww))

Kipindi cha utawala wa Imam Mahdi (a.t.f.):

Kushamiri Haki na Uadilifu:

Uadilifu na haki vitashamiri dunia nzima kiasi kwamba mwanamke mrembo kijana akiwa na mapambo yake ya thamani atatoka Sham na kufika Baghdad peke yake bila kubughudhiwa na yeyote. Watu watafikia daraja ya juu ya uadilifu kiasi kwamba wizi utatoweka na mtu hatomtizama mwanamke kwa jicho la haramu. Picha hii ya usalama inashabihishwa na ‘mbwamwitu ataishi na mbuzi na kuwachunga.’

KUTOKOMEZA MIZIZI YA DHULMA NA KUSIMIKA UADILIFU

Imam atahuisha Sunnah sahihi ya Mtume (saww) na kuhukumu kwa Qur’ani na Sunnah. Ataondosha kila aina ya uzushi na kudhihirisha Uislamu katika ukweli wake kama vile Mtume (saww) alivyokamilisha.

Ni dhahiri kabisa kwa mtazamo huo hali ya Dunia itabadilika na kufikia maendeleo ya kisayansi na teknolojia ambayo haijawahi kufikiwa na mwanadamu. Hii ni dalili kwamba matatizo, migogoro, vita, njaa na misukosuko, chanzo chake ni utawala mbovu na sera za kikafiri. Imam (as) hatawaonea huruma waovu, atawatambua kwa kudra aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Atawaua mpaka watu watakuwa na shaka kuhusu kwamba yeye ni khalifa kweli wa Mtume (saww), kwani Mtume (saww) alikuwa ni mwenye huruma na msa-maha.

Uwingi wa Neema na Utajiri zama za Serikali ya Imam Mahdi (a.t.f.)

Muhimili wa Neema:

Hadithi nyingi zinaonyesha kwamba zama za utawala wa Imam Mahdi (a.t.f.) ulimwengu utabarikiwa na neema nyingi, mali, baraka, nk. Hayo siyo muujiza, bali ni matokeo ya:

- Uongozi adilifu na wenye kuhukumu kwa haki,
- Watu kupenda haki, kuifuata na kuinusuru.

Mwenyezi Mungu ameahidi ikiwa watu wataamini na kumcha atawafungulia baraka za ardhini na mbinguni:

وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أَنْزَلْنَا إِلَيْهِمْ مِنَ الرَّسْمِ
 لَأَكَلُوا مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِن تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ مِّنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ
 وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ سَاءَ مَا يَعْمَلُونَ ﴿١١﴾

“Na lau wangelisimamisha Tawrat na Injil na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola Wao kwa hakika wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Miongoni mwao wako watu walio sawa na wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.” (Sura Maidah: 66).

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ
السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا
يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾

“Na lau kama watu wa mji wangeliamini na kuogopa, kwa hakika tungewafungulia baraka za mbingu na ardhi. Lakini walikadhibisha, kwa hiyo tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.” (Sura Aarfa: 96).

Hata hivi sasa matajiri mabeberu wakiamua kuacha dhulma, dunia ina utajiri wa kutosha kila mwanadamu kuishi kwa neema bila ufukara. *Taghutikrasia*, mfumo unaoongozwa na Ukafiri na Udhaliimu ndiyo sababu ya maafa yote tunayoshuhudia hivi leo. Kwa kusimama kiongozi wa haki na mwadilifu kama Mahdi (a.t.f.) na watu kumnusuru kama vile nyuki wanavyoshikamana na kiongozi wao, ni haki ardhi na mbingu zitapike neema zake.

Neema na Baraka kwa wingi:

Neema zitakithiri kiwango ambacho ulimwengu haujawahi kushuhudia. Mbingu zitateremsha mvua na ardhi itaotesha kila aina ya mimea, majani na matunda. Kila kitu kitapatikana na kugawiwa bure. Mali na utajiri utazidi na mtu atajichukulia kadri anavyoweza. Ardhi itatoa baraka zake. Baraka itazidi. Mazao yatatoka kwa wingi. Miti ya matunda itazaa matunda maradufu. Ardhi itatapika hazina zake (madini yatatoka kwa wingi...)

Amri ya Imam Mahdi (as) kwa wawakilishi wake kote duniani:

Kuwafanya watu kuwa wema na wafuata haki kiasi kwamba hata mbwa mwitu na kondoo wataishi pamoja bila madhara. Uovu wote utapigwa marufuku. Zinaa, ulevi, riba... yote yatatoweka na watu wataelekea kwenye mambo ya dini, ibada, Sheria, na kazi za ku-saidiana. Watu watafanya ibada pamoja. Amana zitarejeshwa kwa wenyewe. Undugu wa kiimani utashamiri. Uovu utatoweka na kila mwenye uadui na Ahlul Bayt (as) ataangamia. Neema itakithiri kiasi kwamba hakuna mtu atakayeomba wala kuhitaji zaka wala sadaka. Mwenye kutoa zaka atatafuta mtu wa kumpa na hatampata yeyote. Kwa sababu ya nuru ya elimu na Wilayah, watu watatosheka na kui-shi maisha ya amani na furaha.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia:

Uislamu ni dini inayotilia mkazo elimu, sayansi na teknolojia. Maisha ya hapa duniani na kesho akhera msingi wake ni elimu. Ndiyo maana neno la kwanza Mwenyezi Mungu alilomteremshia Mtume wake ni *'Iqra-a'* yaani 'soma'. Wengi wa Waislamu kwa kukosa mwongozo sahihi, hatuelewi nini maana ya kusoma. Wengi tunadhani ya kwamba kusoma ni kusoma Qur'ani na kwamba Qur'ani inahusika na mambo ya kiimani tu. Haya siyo mafunzo ya Qur'ani. Qur'ani inatutaka tusome Kitabu cha Mwenyezi Mungu 'aliyeumba'. Kwa hivyo kitabu hapa ni kitabu cha uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Kila kiumbe ni karatasi au mlango wa elimu ndani ya kitabu hicho cha uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hili linatuwekea wazi kwamba elimu zote wanadamu tunazosoma leo ni za Mwenyezi Mungu. Kule kufanya utafiti katika uumbaji na kuona maajabu yake ndiyo kumjua Mwenyezi Mungu na kuelewa kudra na uwezo Wake. Ikiwa Mwenyezi Mungu ni Aalimu na elimu yake ameidhihirisha

katika uumbaji, basi muumini ni yule anayesoma viumbe vya Mwenyezi Mungu.

Hivi ndivyo Qur’ani inavyoelekeza katika aya nyingi. Ni wazi kwamba Waislamu waliofuzu kutoka madrasah ya Mtume wali-poelewa mwongozo wa Qur’ani kuhusu elimu, waliitafuta elimu, sayansi na teknolojia popote ilipo. Baada ya karne moja, Uislamu tayari ulikuwa unashika mwenge wa elimu duniani. Baada ya kuelewa haya, hebu fikiria maendeleo ya elimu, sayansi na teknolojia yatafikia kiwango gani zama za Imam Mahdi (a.t.f.)? Ili kupata taswira kamili, hebu fikiria yafuatayo:

- Leo ulimwengu umefikia maendeleo ya ajabu katika kila uwanja wa elimu. Maajabu ya sayansi na teknolojia kila mtu leo anayashuhudia. Ulimwengu wa elektronika na kompyuta kila siku unafanya miujiza. Kwa hiyo atakapodhihiri Imam Mahdi (as) atakuwa ameshuhudia maajabu haya yote na kuyapokea ili kuyaendeleza na siyo kuyadidimiza. Maendeleo ya sayansi na teknolojia ni neema na baraka ya Mwenyezi Mungu. Ni hoja ya Tawhid, Nubuwwah na Ma’ad.
- Kama kiongozi na Khalifa wa Mwenyezi Mungu, na mrithi wa Kitabu na elimu ya Mtume (saww), Imam Mahdi (a.t.f.), ndiye mwenye siri zote za sayansi na teknolojia. Hakuna katika zama hizi hadi Kiyama mjuzi kuliko yeye katika fani yeyote ile. Kwa kuwa na madaraka yote na hazina zote za ardhi, bila shaka ataendeleza sayansi na teknolojia kwa kiwango cha juu ambacho hakijawahi kufikiwa.
- Kwa kutoweka ukafiri, dhulma na maasi na kushamiri tawhid, amani, na neema, bila shaka watu watakuwa na hamasa ya kusoma na kutafiti kama vile Qur’ani na Sunnah inavyoagiza. Matokeo yake itakuwa ni maendeleo ya ajabu katika sayansi

na teknolojia. Baadhi ya riwaya zinaashiria kwamba Imam atazungumza na watu wote duniani watamuona na kumsikia. Pia zipo zinazoelezea kwamba watu watakuwa na uwezo mkubwa wa kuona na kusikia. Mtu atakuwa na uwezo wa watu arobaini, bali watu watakuwa na nguvu kiasi cha kuondosha mlima kwa mkono. Haya yanaonekana kama alinacha au ngano za kale. Lakini kwa mwanasayansi haya yanawezekana na hata ya ajabu kuliko hayo. Wanasayansi kugundua lishe au virutubisho ambavyo vinaweza kujenga mwili na kuupa uwezo mkubwa si jambo muhali. Pia inawezekana maana halisi ni uwezo wa kiteknolojia watakaoumiliki watu zama hizo.⁵⁹ Kwa kuvaa mawani maalum na kuweka kifaa kidogo sikioni mtu ataweza kuona na kusikia yalio mbali maelfu ya kilomita.

Safari katika anga na sayari za mbali:

Hadithi zinaashiria kwamba Imam (as) atatumia vyombo mahsusi kwenda kwenye anga za juu na sayari zake. Hili siyo kwake tu bin-afsi, bali ni ishara ya maendeleo ya kisayansi na teknolojia kuhusu anga za mbali. Watu zama hizo, watasafiri kwenda anga za juu kama vile sisi tunavyosafiri kutoka bara moja kwenda jingine. Hadithi zinathibitisha kwamba kuna sayari nyingi na zina viumbe wasio binadamu wala malaika wala majini. Hili limethibiti ndani ya Qurani kwa kauli ya Mwenyezi Mungu (swt) katika Surah Rahman:

يَا مَعْشَرَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ إِنِ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُذُوا مِنْ
أَقْطَارِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفُذُوا لَا تَنْفُذُونَ إِلَّا
بِسُلْطَانٍ

⁵⁹ Dastaghayb, Sayyid Abdulhusayn: *Al Mahdi al Maw'ud'*, uk.68

**“ Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa madaraka.”
(Sura Rahman: 33).**

MLANGO WA 4

HAZINA/URITHI ALİYOTUPA IMAM MAHDI (AS)

1. Mwongozo na mafunzo kupitia wawakilishi wake zama za Ghayba Ndogo:

Ni wajibu wa Imam kuwaongoza watu wake zama za Uimamu wake. Mantiki ya kuwepo Imam ni kuongoza umma wake. Zama za Ghayba Ndogo waumini walifaidika na Imam kwa kupitia wawakilishi wake. Walifaidika moja kwa moja na mwongozo wake kwa kupitia wawakilishi wake wanne.

2. Ghayba Kubwa:

Kama ilivyotangulia, baada ya Ghayba Ndogo, Imam alielekeza kwamba waumini washikamane na Ulamaa wenye elimu na dini, walioipa dunia nyongo ili kuwaongoza. Hii ni dhahiri kwamba ulamaa wachamungu, wanapata msaada wake. Katika visa vilivyotangulia (rejea visa) tumeona msaada wa Imam kwa ulamaa kama Al Muqaddas Ardabiliy na Sayyid Bahrul Uluum. Msaada huu utaendelea hadi atakapodhihiri.

3. Baadhi ya dua, Ziyarah na mafunzo:

Dua, katika madrasah ya Ahlul Bayt (as) ni hazina ya mafunzo ya Qur'ani na Sunnah. Ni njia waliyoitumia Maimamu wa Ahlul Bayt (as) kubainisha mafunzo sahihi ya Qur'ani na Sunnah

na pia kudhihirisha haki yao kwa umma wa Kiislamu. *Sahifah as-Sajjadiyah* ni mfano mzuri, Imam Ali Zaynul-Abidin pamoja na kuishi zama za vikwazo na shida alifanikiwa kufikisha ujumbe kwa kupitia dua ambazo zimekusanywa katika kitabu *Sahifah as-Sajjadiyah*. Hazina hizi kutoka kwa Mtume (saww) na Maimamu bila shaka zimo ndani ya mikono ya Imam Mahdi (a.t.f.). Kwa hiyo dua nyingi zimepokelewa kutoka kwa Imam Mahdi (a.t.f.) na pia Ziyarah.

Hizi ni baadhi ya dua. Ni vyema tukachunguza maana na faida zake ili kuwa na fikra ya hazina tuliyopewa na Imam wetu wa Zama.

DUA ‘AHD

اللَّهُمَّ بَلِّغْ مَوْلَايَ صَاحِبَ الزَّمَانِ صَلَوَاتِ اللَّهِ
عَلَيْهِ عَنْ جَمِيعِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ فِي مَشَارِقِ
الْأَرْضِ وَمَغَارِبِهَا، وَبَرِّهَا وَبَحْرِهَا وَسَهْلِهَا
وَجَبَلِهَا، حَيْثُمْ وَمَيْتِهِمْ، وَعَنْ وَالِدِيَّ وَوَلَدِي
وَعَنِّي مِنَ الصَّلَوَاتِ وَالتَّحِيَّاتِ زِنَةَ عَرْشِ اللَّهِ
وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ، وَمُنْتَهَى رِضَاهُ وَعَدَدَ مَا أَحْصَاهُ
كِتَابُهُ وَأَحَاطَ بِهِ عِلْمُهُ، اللَّهُمَّ إِنِّي أُجَدِّدُ لَهُ فِي هَذَا
الْيَوْمِ وَفِي كُلِّ يَوْمٍ عَهْدًا وَعَقْدًا وَبَيْعَةً فِي رَقَبَتِي
اللَّهُمَّ كَمَا شَرَفْتَنِي بِهَذَا التَّشْرِيفِ وَفَضَّلْتَنِي

بِهَذِهِ الْفَضِيلَةِ وَخَصَّصْتَنِي بِهَذِهِ النِّعْمَةِ، فَصَلِّ
 عَلَيَّ مَوْلَايَ وَسَيِّدِي صَاحِبِ الزَّمَانِ، وَاجْعَلْنِي
 مِنْ أَنْصَارِهِ وَأَتَّيَاعِهِ وَالذَّابِّينَ عَنْهُ، وَاجْعَلْنِي
 مِنَ الْمُسْتَشْهِدِينَ بَيْنَ يَدَيْهِ طَائِعًا غَيْرَ مُكْرَهٍ فِي
 الصِّفِّ الَّذِي نَعَتَ أَهْلَهُ فِي كِتَابِكَ فَقُلْتَ: (صَفَا
 كَانَهُمْ بُنْيَانٌ مَرْصُوصٌ) عَلَيَّ طَاعَتِكَ وَطَاعَةِ
 رَسُولِكَ وَآلِهِ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ، اللَّهُمَّ هَذِهِ بَيْعَةٌ لَهُ فِي
 عُنُقِي إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ .

“Ewe Mola mfikishie bwana wangu, Kiongozi wa zama hizi, rehema na amani za Mwenyezi Mungu kutoka kwa waumini wote – waume kwa wake - walioko Mashariki na Magharibi ya ardhi, (wanaoishi) nchi kavu na majini, kwenye tambarare na milimani, walio hai na walio wafu, na kutoka kwa wazazi wangu na watoto wangu, na kuto- ka kwangu - rehema na amani na salamu ambazo - (kiwango chake ni sawa na) uzito wa arshi ya Mwenyezi Mungu na wino wa maneno yake na ukomo wa ridha yake na idadi ya yale ambayo kitabu Chake kimekusanya na elimu yake kuyaenea. Ewe Mola mimi kwa siku hii ya leo na kila siku ninathibitisha upya ahadi kwake, mkataba na bay’a iliyopo shingoni mwangu.

“Ewe Mola, kama ulivyonitukuza kwa jambo hili tukufu, na ukani- fadhilisha kwa fadhila hii, na ukanitunuku neema hii, basi mfikishie kiongozi wangu na bwana wangu, Kiongozi wa zama hizi, rehema na amani na unijalie kuwa miongoni mwa wasaidizi wake, wafuasi wake na watetezi wake. Pia nijalie niwe miongoni mwa wenye kujitoa muhanga mbele yake, nikiwa mtiifu bila kushurutishwa, (nijalie)

kuwa miongoni mwa safu uliyosifu watu wake katika Kitabu chako ukasema : ‘Safu kana kwamba ni jengo madhubuti. ’Surah Swaff: 4) kwenye utiifu wako na utiifu wa Mtume wako na Aali zake (as). Ewe Mwenyezi Mungu hii ni bay’a yangu kwake shingoni mwangu hadi siku ya Kiyama.”

DUA FARAJ

إِلٰهِي عَظُمَ الْبَلَاءُ، وَبَرَحَ الْخَفَاءُ، وَانْكَشَفَ
 الْغَطَاءُ، وَانْقَطَعَ الرَّجَاءُ، وَضَاقَتِ الْأَرْضُ،
 وَمُنِعَتِ السَّمَاءُ، وَأَنْتَ الْمُسْتَعَانُ، وَالْإِيكَ
 الْمُشْتَكِي، وَعَلَيْكَ الْمُعْوَلُ فِي الشَّدَّةِ وَالرَّخَاءِ،
 اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، أَوْلِي الْأَمْرِ
 الَّذِينَ فَرَضْتَ عَلَيْنَا طَاعَتَهُمْ، وَعَرَّفْتَنَا بِذَلِكَ
 مَنْزِلَتَهُمْ، فَفَرِّجْ عَنَا بِحَقِّهِمْ فَرَجًا عَاجِلًا قَرِيبًا
 كَلِمَحَ الْبَصْرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ، يَا مُحَمَّدُ يَا عَلِيُّ يَا
 عَلِيُّ يَا مُحَمَّدُ اكْفِيَانِي فَإِنِّكُمَا كَافِيَانِ، وَأَنْصُرَانِي
 فَإِنِّكُمَا نَاصِرَانِ، يَا مَوْلَانَا يَا صَاحِبَ الزَّمَانِ،
 الْغَوْثَ الْغَوْثَ الْغَوْثَ، ادْرِكْنِي ادْرِكْنِي ادْرِكْنِي،
 السَّاعَةَ السَّاعَةَ السَّاعَةَ، الْعَجَلَ الْعَجَلَ الْعَجَلَ، يَا

أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ، بِحَقِّ مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ .

“Ewe Mola wangu, balaa imekuwa kubwa, na jambo limekuwa wazi, na pazia imeondoka, na matumaini yamekatika na ardhi imekuwa finyu, na mbingu imezuiwa, na Wewe ndiye unayeombwa msaada na ni kwako ndiko yanaelekezwa mashtaka. Na ni Wewe ndiye unayeliliwa katika shida na raha. Ewe Mola, mfikishie rehema na amani Mtume Muhammad na Aali zake – ulil amri (wenye mamlaka)- ambao umetufaradhishia sisi kuwatii na ukatufahamisha kwa hilo daraja yao, basi kwa haki walio nayo utufariji faraja iliyo ya haraka, tena karibu kama vile pepeso la macho au iliyo karibu zaidi. Ewe Muhammad, ewe Ali, ewe Ali, ewe Muhammad, nitoshelezeni hakika nyinyi ni wenye kutosheleza, na mminusuru hakika nyinyi ni wenye kunusuru. Ewe bwana wetu ewe Kiongozi wa zama hizi, msaada, msaada, msaada, niwahi (uniokoe), niwahi (uniokoe), niwahi (uniokoe), muda huu, muda huu, muda huu, haraka, haraka, haraka, ewe mwingi wa kurehemu, kwa haki ya Muhammad na Aali zake waliotakaswa.

ZIYARAH YA IMAM MAHDI (AS)

<p>Amani iwe juu yako, ewe Khalifa wa Mwenyezi Mungu na Khalifa wa baba zake walioongoka,</p>	<p>Assalamu a'layka ya khaliifatal-lahi wa khaliifata aabaa ihil mahdiyyina</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا خَلِيفَةَ اللَّهِ وَخَلِيفَةَ آبَائِهِ الْمُهَدِّيِّينَ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe Wasii wa Mawasii waliotangulia,</p>	<p>Assalamu a'layka ya wasiyy al-awsya 'ilmaadhiiina</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَصِيَّ الْأَوْصِيَاءِ الْمَاضِيْنَ،</p>

<p>Amani iwe juu yako, ewe mwenye kuhifadhi siri za Mola wa walimwengu,</p>	<p>Assalamu a'layka ya haafidha asraari rabbil aa'lamiina</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حَافِظَ أَسْرَارِ رَبِّ الْعَالَمِينَ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe Bakisho la Mwenyezi Mungu kutokana na wabora walioteuliwa,</p>	<p>Assalamu a'layka ya baqiyyatallahi mina sswaf-watil muntajabiina</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَقِيَّةَ اللَّهِ مِنَ الصَّفْوَةِ الْمُنْتَجَبِينَ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe mtoto wa Nuru zing'arazo,</p>	<p>Assalamu 'alayka yaabnal anwaariz zaahirah</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنَّ الْأَنْوَارِ الزَّاهِرَةِ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe mtoto wa ma-bwana watukufu wenye nuru,</p>	<p>Assalamu 'alayka yabnal a-a'laa-milbaahirah</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنَّ الْأَعْلَامِ الْبَاهِرَةِ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe mtoto wa kizazi kilichotakaswa,</p>	<p>Assalamu 'alayka yaabnal 'itratit twaahirah</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنَّ الْعُرْتَةِ الطَّاهِرَةِ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe machimbo ya elimu ya Mtume (saww),</p>	<p>Assalamu 'alayka ya ma'dinal 'uluumi nnabawiyah</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَعْدِنَ الْعُلُومِ النَّبَوِيَّةِ،</p>

<p>Amani iwe juu yako, ewe mlango wa Mwenyezi Mungu, (mlango) wa pekee wa kuingilia Kwake,</p>	<p>Assalamu ‘alayka ya baaba llahi lladhy laa yu-‘ta illa minhu</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَابَ اللَّهِ الَّذِي لَا يُؤْتِي إِلَّا مِنْهُ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe njia ya Mwenyezi Mungu ambayo asiyeipita lazima ataangamia,</p>	<p>Assalamu ‘alayka ya sabiila llahi lladhy man salaka ghayrahu halaka</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَبِيلَ اللَّهِ الَّذِي مَنْ سَلَكَ غَيْرَهُ هَلَكَ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe nuru ya Mwenyezi Mungu isiyozimwa,</p>	<p>Assalamu ‘alayka ya nuura allahi lladhy la yutfaa</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نُورَ اللَّهِ الَّذِي لَا يُطْفِئُ،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe Hoja ya Mwenyezi Mungu isiyofichwa,</p>	<p>assalamu `alayka ya hujjata allahi allaty la takhfa</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حُجَّةَ اللَّهِ الَّتِي لَا تَخْفَى،</p>
<p>Amani iwe juu yako, ewe Hoja wa Mwenyezi Mungu kwa wote walio ardhini na mbinguni,</p>	<p>assalamu `alayka ya hujjata allahi `ala man fi al-ardhi walssama ‘i</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حُجَّةَ اللَّهِ عَلَى مَنْ فِي الْأَرْضِ وَالسَّمَاءِ،</p>

<p>Amani iwe juu yako, amani kutoka kwa yule anayekutambua kwa vile alivyokutambulisha Mwenyezi Mungu,</p>	<p>assalamu `alayka salama man `ara-faka bima `arra-faka bihi allahu</p>	<p>السَّلَامُ عَلَيْكَ سَلَامٌ مَنْ عَرَفَكَ بِمَا عَرَفَكَ بِهِ اللَّهُ،</p>
<p>Na akakusifu kwa baadhi ya sifa zako unazostahili na juu ya hizo,</p>	<p>wa na`ataka biba`di nu`utika allaty anta ahluha wa fawqaha</p>	<p>وَنَعْنَتُكَ بِبَعْضِ نِعْوَتِكَ الَّتِي أَنْتَ أَهْلُهَا وَفَوْقُهَا،</p>
<p>Nashuhudia ya kwamba wewe ni Hoja juu ya waliotangulia na kwa watako-okuja,</p>	<p>ash-hadu annaka alhujjatu `ala man mada wa man baqiya</p>	<p>أَشْهَدُ أَنَّكَ الْحُجَّةُ عَلَى مَنْ مَضَى وَمَنْ بَقِيَ،</p>
<p>Na maadui zako ndiyo wenye hasara,</p>	<p>wa a`da`aka humu alkhasiruna</p>	<p>وَأَعْدَاؤُكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ،</p>
<p>Na hakika wewe ni hazina ya kila elimu,</p>	<p>wa annaka khazinu kulli `ilmin</p>	<p>وَأَنَّكَ خَازِنُ كُلِّ عِلْمٍ،</p>
<p>Na mfunguaji (mpasuaji) wa kila kilicho fungwa,</p>	<p>wa fatiqu kulli ratqin</p>	<p>وَفَاتِقُ كُلِّ رَتْقٍ،</p>
<p>Na msimamishaji wa kila haki,</p>	<p>wa muhaqqiqu kulli haqqi</p>	<p>وَمُحَقِّقُ كُلِّ حَقٍّ</p>

<p>Na mwondoshaji wa kila upotofu,</p>	<p>wa mubtilu kulli batilin</p>	<p>وَمُبْتَلٍ كُلِّ بَاطِلٍ،</p>
<p>Ewe bwana wangu! Nimekuridhia wewe kuwa ndio Imamu wangu, kiongozi, msimamizi na mwelekezaji,</p>	<p>radhwituka ya mawlaya im-aaman wa haadi-yan wa waliyyan wa murshidan</p>	<p>رَضِيْتِكَ يَا مَوْلَايَ إِمَامًا وَهَادِيًا وَوَلِيًّا وَمُرْشِدًا</p>
<p>Kamwe, simtaki yeyote badili yako na wala sitamchukua bwana mwingine zaidi yako,</p>	<p>laa abtaghii bika badalan wa la attakhidhu min dunika waliyyan</p>	<p>لَا أَبْتَغِي بِكَ بَدَلًا وَلَا أَتَّخِذُ مِنْ دُونِكَ وَلِيًّا،</p>
<p>Nashuhudia ya kwamba wewe ndiyo haki iliyo thabiti na isiyo na kasoro yeyote,</p>	<p>ash-hadu annaka alhaqqu alththabitu alladhii la `ayba fih</p>	<p>أَشْهَدُ أَنَّكَ الْحَقُّ الْثَّابِتُ الَّذِي لَا عَيْبَ فِيهِ،</p>
<p>Na kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu kuhusu wewe ni haki, mimi sina shaka kwa sababu ya urefu wa ghayba na umbali wa zama,</p>	<p>wa anna wa `dallahi fiika haqun la artaabu litulil ghaybati wa bu `dil amadi</p>	<p>وَأَنَّ وَعَدَ اللَّهُ فِيكَ حَقًّا لَا أَرْتَابُ لِطَوْلِ الْغَيْبَةِ وَبَعْدِ الْأَمَدِ،</p>

<p>Na kamwe sitochanganyikiwa kama wale ambao waliokupuuza na wakapuuza haki yako,</p>	<p>wa la atahayyru ma`a man jahilaka wa jahila bika</p>	<p>وَلَا أَتَحِيرُ مَعَ مَنْ جَهْلِكَ وَجَهْلِكَ بِكَ،</p>
<p>Nasubiri na kutegemea siku (za kudhiri) zako,</p>	<p>munta`irun mutawaqqi`un li-ayyamika</p>	<p>مُنْتَظِرٌ مُتَوَقِّعٌ لِأَيَّامِكَ،</p>
<p>Na wewe ni mwombezi usiye na upinzani</p>	<p>wa anta shshafi`ul ladhii la tunaza`u</p>	<p>وَأَنْتَ الشَّافِعُ الَّذِي لَا تُنْزَعُ،</p>
<p>Na mpenzi (wa Mwenyezi Mungu) usiyerudishwa nyuma,</p>	<p>walwaliyyu lladhy la tudaafa`u</p>	<p>وَالْوَلِيُّ الَّذِي لَا تُدْفَعُ</p>
<p>Allah amekuweka akiba kwa ajili ya kunusuru Dini na kuwapa nguvu waumini,</p>	<p>dhakharaka llahu linusrati ddini wa i`zaazil mu`miniina</p>	<p>ذَخَّرَكَ اللَّهُ نُصْرَةَ الدِّينِ وَإِعْزَازِ الْمُؤْمِنِينَ،</p>

Na kulipiza kisasi dhidi ya wanaokanusha haki na kuritadi,	wal-intiqami minal jaahidiinal maariqiina	وَالْإِنْتِقَامِ مِنَ الْجَاحِدِينَ الْمَارِقِينَ،
Ninashuhudia ya kwamba kwa kuku-fuata (na kukunusu-ru) ndiyo amali (kazi) zinakubaliwa,	Ashhadu anna biwilaayatika tuqbalu al-a`maalu	أَشْهَدُ أَنَّ بَوْلَايَتِكَ تَقْبَلُ الْأَعْمَالُ،
Na matendo yana-takaswa,	wa tuzakka al-af`aalu	وَتُزَكَّى الْأَفْعَالُ
Na mema yanaongezwa maradufu,	wa tudha `aful hasanatu	وَتُضَاعَفُ الْحَسَنَاتُ،
Na maovu hufutwa,	wa tumha ssayy-iaatu	وَتُمَحَى السَّيِّئَاتُ
Kwa hivyo huyo anaekuja na ameshi-kamana na wilayah yako,	faman jaa-a biwilaayatika	فَمَنْ جَاءَ بَوْلَايَتِكَ
Na akatambua uimamu wako Amali zake huku-baliwa,	Wa`tarafa bi-imaamatika qubilat a `maalu	وَاعْتَرَفَ بِإِمَامَتِكَ قُبِلَتْ أَعْمَالُهُ

Na anenayo huthibitika kuwa kweli,	wa suddiqat aqwaaluhu	وَصَدَّقْتَ أَقْوَالَهُ
Na mema yake huzidi maradufu,	wa tadhaa 'afat hasanaatuhu	وَتَضَاعَفَتْ حَسَنَاتُهُ
Na maovu yake hufutwa,	wa muhiyat sayyi aatuhu	وَمُحِبَّتِ سَيِّئَاتُهُ،
Ama yeyote anaekengeuka na usimamizi wako,	wa man 'adala 'an wilaayatika	وَمَنْ عَدَلَ عَنِ وِلَايَتِكَ
Na kupuuza maarifa (kukujua) yako,	wa jahila ma 'rifataka	وَجَهَلَ مَعْرِفَتَكَ
Na akamtambua mwingine badala yako,	wastabdala bika ghayraka	وَأَسْتَبَدَّلَ بِكَ غَيْرَكَ
Allah atamtupa Motoni akiangukia pua lake,	kabbahu -Ilaahu 'ala mankharihi fin nari	كَبَّهُ اللَّهُ عَلَى مَنْخَرِهِ فِي النَّارِ،
Na Allah hatamkubalia amali yeyote ile,	wa lam yaq-bali -Ilaahu lahu 'amalan	وَلَمْ يَقْبَلِ اللَّهُ لَهُ عَمَلًا
Na siku ya Kiyama hatopimiwa chochote,	wa lam yuqim lahu yawmal qiyaamati waznan	وَلَمْ يُعِمَّ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَزَنًا،

<p>Namshuhudisha Allah na malaika wake na wewe pia ewe bwana wangu na-kushuhudisha na hili,</p>	<p>ushhidu -Ilaaha wa ushidu malaaikatahu wa ushiduka ya mawlaaya bihad-haa</p>	<p>أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُ مَلَائِكَتَهُ وَأَشْهَدُكَ يَا مَوْلَايَ بِهَذَا،</p>
<p>(shahada) ambayo dhahiri yake ni sawa na batini yake,</p>	<p>dhwaahiruhu kabaatinihi</p>	<p>ظَاهِرُهُ كَبَاطِنِهِ</p>
<p>Na siri yake ni sawa na uwazi wake,</p>	<p>wa sirruhu ka'alaaniyatih</p>	<p>وَسِرُّهُ كَعَلَانِيَّتِهِ،</p>
<p>Na wewe ni shahidi juu ya hilo (shahada hii),</p>	<p>wa antash shaahidu 'ala dhaalika</p>	<p>وَأَنْتَ الشَّاهِدُ عَلَى ذَلِكَ،</p>
<p>Na hii ni ahadi yangu kwako na agano langu na wewe,</p>	<p>wa huwa 'ahdy ilayka wa miitha-qiy ladayka,</p>	<p>وَهُوَ عَهْدِي إِلَيْكَ وَمِيثَاقِي لَدَيْكَ،</p>
<p>Kwa sababu wewe ni nidhamu ya dini,</p>	<p>idh anta nidhaamud dini</p>	<p>إِذْ أَنْتَ نِظَامُ الدِّينِ،</p>
<p>Na kiongozi wa wachamungu,</p>	<p>wa ya'subul mut-taqiina</p>	<p>وَيَعْسُوبُ الْمُتَّقِينَ،</p>

Na heshima ya wana-tawhidi,	wa `izzul muwah-hidiina	وَعِزُّ الْمُؤَحِّدِينَ
Na Mola wa walim-wengu ameniamrisha hilo.	wa bidhaalika amaranii rabbul `alamiina	وَبِذَلِكَ أَمَرَنِي رَبُّ الْعَالَمِينَ
Hata kama zama zitakuwa ndefu,	falaw tatwaawa-latid duhuuru	فَلَوْ تَطَاوَلَتِ الدُّهُورُ،
Na hata kama miaka ya kuishi itakuwa mirefu,	wa tamaadatil-a`amaaru	وَتَمَادَتِ الْأَعْمَارُ
Hayo hayata-nizidishia ila kuwa na yakini kuhusu wewe,	lam azdad fiika illa yaqiinan	لَمْ أَزِدْ فِيكَ إِلَّا يَقِينًا
Na mapenzi kwako,	wa laka illa hub-ban	وَلَكَ إِلَّا حُبٌّ
Na kuwa na imani nawe na kukutege-me,	wa `alayka illa muttakilan wa mu`tamidan	وَعَلَيْكَ إِلَّا مُتَّكِلًا وَمُعْتَمِدًا

<p>Na kuhusu kudhihiri kwako, kutazamia na kungojea,</p>	<p>wa lidhuhu-urika illa mutawaqqi`an wa muntadhiran</p>	<p>وَلِظُهُورِكَ إِلَّا مُتَوَقِّعًا وَمُنْتَظِرًا</p>
<p>Na kutazamia mimi kufanya jihadi katika hadhara yako,</p>	<p>wa lijahaady bayna yadayka mutaraqqiban</p>	<p>وَلِجِهَادِي بَيْنَ يَدَيْكَ مُتَرَقِّبًا</p>
<p>Na hivyo, mimi kutoa nafsi yangu, mali yangu, watoto wangu, familia yangu, na kila kitu alichoni-bariki Mwenyezi Mungu mbele yako na kutekeleza kama unavyoamrisha na kukataza,</p>	<p>Fa-abdhul nafsy wa maaly wa walady wa ahly wa jami`a ma khaawwalaniya rabby bayna yadayka watasarrufa bayna amrika wa nahyika</p>	<p>فَأَبْدُلْ نَفْسِي وَمَالِي وَوَلَدِي وَأَهْلِي وَجَمِيعَ مَا خَوْلَنِي رَبِّي بَيْنَ يَدَيْكَ وَالتَّصَرُّفِ بَيْنَ أَمْرِكَ وَنَهْيِكَ</p>
<p>Ewe bwana wangu, ikiwa nitadiriki zama zako tukufu,</p>	<p>mawlaya fa-in adraktu ayyaam-akaz zaahirah</p>	<p>مَوْلَايَ فَإِنْ أَدْرَكْتُ أَيَّامَكَ الزَّاهِرَةَ</p>
<p>Na alama (bendera) zako zenye kung'ara,</p>	<p>wa a`laamakal baahirah</p>	<p>وَأَعْلَامَكَ الْبَاهِرَةَ</p>

<p>Basi, mimi ndiye huyu hapa, mtumwa wako mwenye kutekeleza amri yako na kujiepusha na unayokataza,</p>	<p>fahaa anaa dhaa `abdukal mutasarriifu bayna amrika wa nahyika</p>	<p>فَهَا أَنَا ذَا عَبْدُكَ الْمُتَّصِرُفُ بَيْنَ أَمْرِكَ وَنَهْيِكَ</p>
<p>Nataraji kwa hayo, kufa shahidi mbele yako na kufuzu ni kiwa pamoja nawe,</p>	<p>arjuu bihish shahaadata bayna yadayka wal-fawza ladayka</p>	<p>أَرْجُو بِهِ الشَّهَادَةَ بَيْنَ يَدَيْكَ وَالْفَوْزَ لَدَيْكَ</p>
<p>Ewe bwana wangu, ikiwa yatanifika mauti kabla ya kudhiri kwako,</p>	<p>mawlaaya fa-in adrakanyal mawtu qabla dhuhuurika</p>	<p>مَوْلَايَ فَإِنِ أَدْرَكَنِي الْمَوْتُ قَبْلَ ظُهُورِكَ</p>
<p>Basi mimi namlilia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kupitia kwako na baba zako waliotoharika,</p>	<p>fa'inny atawas-salu bika wa bi-aabaa'ikat twaahiriina ila allahi ta`ala</p>	<p>فَأِنِّي أَتَوَسَّلُ بِكَ وَبِآبَائِكَ الطَّاهِرِينَ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى</p>
<p>Na ninamuomba aziteremshe rehema na amani kwa Muhammad (saww) na Aali zake Muhammad (saww),</p>	<p>wa as'aluhu an yusalliya `ala Muhammadin wa aali Muhammadin</p>	<p>وَأَسْأَلُهُ أَنْ يُصَلِّيَ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ،</p>

Na anijalie (kurejea) mara nyingine zama za kudhihiri kwako,	wa an yaj`ala lii karratan fii dhuhuurika	وَأَنْ يَجْعَلَ لِي كَرَّةً فِي ظُهُورِكَ
Na maisha mara nyingine katika zama zako,	wa raj`atan fii ayyaamika	وَرَجْعَةً فِي أَيَّامِكَ،
Ili kwa kukutii wewe nifikie muradi wangu,	li-ablugha min taa`atika muraadii	لِإِبْلَغٍ مِنْ طَاعَتِكَ مُرَادِي
Na niponye moyo wangu (kwa kulipiza kisasi) dhidi ya maadui wako,	wa ashfiya min a`da`ika fu aadii	وَأَشْفِيَّ مِنْ أَعْدَائِكَ فُؤَادِي،
Ewe Bwana wangu, nimesimama kuku-zuru nikiwa na msimamo wa wenye makosa wenye kujutia,	mawlaaya waqaf-tu fi ziyaaratika mawqifal khaatwi-iinan naadimiina	مَوْلَايَ وَقَفْتُ فِي زِيَارَتِكَ مَوْقِفَ الْخَاطِئِينَ النَّادِمِينَ
Wenye kuogopa adhabu ya Mola wa walimwengu,	Alkhaa-ifina min `iqaabi rabbil`aalamiina	الْخَائِفِينَ مِنْ عِقَابِ رَبِّ الْعَالَمِينَ،
na nimekwisha tegemea juu ya shafaa (uombezi) yako,	wa qadit takaltu `alaa shafaa`atika	وَقَدِ اتَّكَلْتُ عَلَى شَفَاعَتِكَ،

na kutarajia, kwa kukunusuru kwangu na shafaa yako, kufutiwa madhambi yangu,	Warajawtu imuwaalaatika wa shafaa`atika mahwa dhunuubii	وَرَجَوْتُ بِمُؤَلَاتِكَ وَشَفَاعَتِكَ مَحَوَّ ذُنُوبِي،
na kusitiriwa aibu zangu,	wa satra`uyubi	وَسَتَّرَ عُيُوبِي،
na msamaha wa kasoro zangu,	wa maghfirata zalalii	وَمَغْفِرَةَ زَلَّيْ،
(Kwa hivyo basi), ewe Bwana wangu uwe pamoja na mtumwa wako hadi kutimiza matumaini yake,	fakun liwaliyyika ya mawlaaya `inda tahqiqi amalihi	فَكُنْ لَوْلِيَّكَ يَا مَوْلَايَ عِنْدَ تَحْقِيقِ أَمَلِيهِ
na umuombe Mwenyezi Mungu amsamehe kasoro zake,	was-ali llaha ghufraana zalalihi	وَاسْأَلِ اللَّهَ غُفْرَانَ زَلَّيْ،
hakika, amening`inia kwenye kamba yako,	faqad ta`allaqa bihablika	فَقَدْ تَعَلَّقَ بِحَبْلِكَ
na kushikamana na wilaya (kukunusuru) yako,	wa tamassaka biwilaayatika	وَتَمَسَّكَ بِوِلَايَتِكَ،

na kujivua (ku-wakataa) na maadui zako,	wa tabarra-a min a- a'daaika	وَتَبَرَّأَ مِنْ أَعْدَائِكَ
Ewe Allah, ziteremshe rehema na amani kwa Muhammad (saww) na Aali zake na umtimizie walii (mpenzi) Wako uli-omuahidi,	Allahumma swalli a'laa Muhammadin wa aalihi wa anjiz liwaliyyika maa wa a'dtahu	اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَالِهِ وَأَنْجِزْ لَوْلِيِّكَ مَا وَعَدْتَهُ،
Ewe Allah, lidhi-hirishe neno lake,	Allahumma adh'hir kalima-tahu	اللَّهُمَّ أَظْهِرْ كَلِمَتَهُ،
na uweke juu mwito wake,	wa a-a'li da-'watahu	وَأَعْلِ دَعْوَتَهُ،
na umnusu juu ya adui yake na adui Yako, Ewe Mola wa walimwengu,	wansurhu a'laa a'duwwihi wa a'duwwika ya rabbal aa'lamiina	وَأَنْصُرْهُ عَلَى عَدُوِّهِ وَعَدُوِّكَ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ،
Ewe Allah, ziteremshe rehema na amani kwa Muhammad (saww) na Aali zake,	Allahumma swalli a'laa Muhammadin wa aali Muhammadin	اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَالِ مُحَمَّدٍ

na ulidhihirishe Neno Lako Kamili na Mfichwa wako ndani ya ardhi Yako,	wa adh-hir kalimatakat taammatata wa mughayyabaka fi ardhwika	وَأَظْهَرُ كَلِمَتِكَ التَّامَّةَ وَمُغَيَّبِكَ فِي أَرْضِكَ
mwenye hofu (wasiwasi), mwenye kutazamia,	alkha-ifa almutaraqqiba	الْخَائِفَ الْمُتَرَقِّبَ،
Ewe Allah, mnu-suru kwa nusra yenye nguvu,	Allahumma nsurhu nasran a'ziizan	اللَّهُمَّ أَنْصُرْهُ نَصْرًا عَزِيزًا
na umpe ushindi ulio mwepesi,	waftah lahu fathan yasiiran	وَأَفْتَحْ لَهُ فَتْحًا يَسِيرًا
Ewe Allah, kwa mkono wake, itukuze dini Yako, baada ya kuzorota,	Allahumma wa-i'zza bihi ddiina ba-a'dal khu-muuli	اللَّهُمَّ وَأَعِزِّ بِهِ الدِّينَ بَعْدَ الْخُسُوفِ،
na ifanye haki ichomoze tena baada ya kupotea,	wa atwli` bihil haqqa ba-a'dal-ufuuli	وَأَطْلِعْ بِهِ الْحَقَّ بَعْدَ الْأَفْوَالِ

na litoweshe giza,	wa ajli bihi dh-dhulmah	وَأَجَلٍ بِهِ الظُّلْمَةَ
na uondoshe ghamu (yote ya huzuni),	wakshif bihil ghummah	وَكَشِفَ بِهِ العُمَّةَ
Ewe Allah, kwa kupitia yeye, eneza amani katika nchi,	Allahumma wa amin bihil bilaada	اللَّهُمَّ وَآمِنُ بِهِ البِلَادَ،
na uwaongoze waja (wako),	wahdi bihil I'baada	وَاهْدِ بِهِ العِبَادَ،
Ewe Allah, kwa kupitia yeye, eneza kote ndani ya ardhi uadilifu na usawa kama vile ilivyojanzwa dhulma na jeuri.	Allahumma imla bihil ardha a'dlan wa qistwan kama muliat dhulman wa jawran	اللَّهُمَّ اَمْلَأْ بِهِ الأَرْضَ عَدْلًا وَقِسْطًا كَمَا مُلِئْتَ ظُلْمًا وَجَوْرًا
Hakika Wewe ni Mwenye kusikia Mwenyekujibu.	Innaka sami-u'n mujibun	إِنَّكَ سَمِيعٌ مُجِيبٌ
Amani iwe juu yako ewe walii wa Allah,	Alssalamu a'layka ya waliyyallahi	السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَلِيَّ اللَّهِ،

<p>Tafadhali mruhusu mtumwa wako kuingia ndani ya sehemu yako takatifu (haram),</p>	<p>i-'dhan liwaliyyi-ka fid dukhuuli ilaa haramika</p>	<p>أُذِّنْ لَوْلِيكَ فِي الدُّخُولِ إِلَى حَرَمِكَ</p>
<p>Rehema na Amani na Baraka zake Allah ziwe juu yako na baba zako waliotoharika.</p>	<p>Salawaatul-lahi a'layka wa a'laa aabaa-ikat twaahiriina wa rahmatullahi wa barakaatuhu</p>	<p>صَلِّوَاتُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَعَلَى آبَائِكَ الطَّاهِرِينَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ</p>

HITIMISHO NA MAFUNZO

1. Maimamu, Makhalifa baada ya Mtume (saww) ni kumi na mbili:

Mtume (saww) katuhusia kwamba baada yake watakuwepo makhalifa kumi na mbili. Maimamu hao kama alivyowataja ni kama ifuataavyo:

1. Imam Ali (as)
2. Imam Hasan (as)
3. Imam Husayn (as)
4. Imam Ali Zaynulabidin (as)
5. Imam Muhammad Baqir (as)

6. Imam Ja‘far Sadiq (as)
7. Imam Musa Kadhim (as)
8. Imam Ali Ridhwa (as)
9. Imam Muhammad Taqi (as)
10. Imam Ali Naqi (as)
11. Imam Hasan Askariy (as)
12. Imam Mahdi (a.t.f.)

Historia inashuhudia kwamba kweli walikuwa Maimamu katika zama zao na mmoja baada ya mwingine walirithi nuru ya Mtume (saww) hadi wa mwisho Imam Mahdi (a.t.f.). Baada ya Qur’ani na Sunnah kufukiwa ndani ya tope uzushi na kumsingizia Mtume (saww), wao ndiyo waliosimama kufukua elimu na kusomesha ul-amaa katika fani mbalimbali.

Kwa nini Maimamu hawa siyo maarufu?

Ikiwa huwajui sababu ni hizi hapa:

- Watawala katika kila zama walijitahidi kuwadhibiti na kuzima nuru yao kwa kuwaua na kufyeka wafuasi wao.⁶⁰
- Wanazuoni wachamungu wameshindwa kutetea waziwazi haki ya Ahlul Bayt (as) kwa kuhofia maisha yao. Wanazuoni wameishi

⁶⁰ Hivi ndivyo watawala waliodai ukhalifa wa Mtume (s) walivyowauwa Maimamu wa Ahlul Bayt, kizazi cha Mtume na warithi wake:

- Imam Hasan (a) alipewa sumu na mkewe Ju’dah binti Ash’ath (l.a.) kwa amri ya Muawiya bin Abi Sufyan.
- Imam Husayn (a) alikatwa kichwa na Shimr Dhil Jawshan (l.a.) kwa amri ya Yazid (l.a.) bin Muawiyah (l.a.)
- Imam Ali Zaynulabidin (a) alipewa sumu na Walid bin Abdul Malik Marwaan (l.a.), khalifa wa 6 wa kiumayyah

ndani ya taqiya (kuficha kile unachokiamini kwa kuhofia maisha yako).

- Wanazuoni waovu wanaolamba fadhila za watawala dhalimu, wametumika kuwafundisha Waislamu kwamba Mtume ni ‘Abtaru’, na kwamba hakuna watu maalumu waliochaguliwa kama kizazi cha Mtume (saww). ‘Aali Muhammad’, na ‘Ahlul Bayt’, maneno ambayo yana tafsiri maalum ndani ya Qur’ani na Sunnah yakapewa tafsiri potofu.
- Waliopofuka mioyo yao daima watakanusha nuru mithili ya mgonjwa akiletewa chakula kitamu hutapika. Ni muhimu kuelewa kwamba Maimamu hawa siyo wa Mashia bali hawa ndiyo Maimamu tulioachiwa na Mtume (saww) watuongoze. Wote ulamaa wema waliwatambua na kuwafuata.

2. Kwa nini imani ya Mahdi imetelekezwa?

Ni ajabu kwamba pamoja na ulamaa wote hawa wakubwa waliopambika na elimu mbalimbali na Huffadhi⁶¹ wa hadithi kusema kwamba hadithi za Mahdi ni sahihi, itikadi hii imekuwa inatiliwa shaka na

-
- Imam Mohammad Baqir (a) alipewa sumu na Hisham bin Abdul Malik Marwaan (l.a.), khalifa wa 10 wa kiumayyah
 - Imam Ja‘far Sadiq (a) alipewa sumu na Mansur Dawaniqi (l.a.), khalifa wa pili wa kiabbasi
 - Imam Musa Kadhim (a) alipewa sumu na Harun Rashid (l.a), khalifa wa 5 wa kiabbasi
 - Imam Ali Ridhwa (a) alipewa sumu na Maa‘mun Rashid (l.a.), khalifa wa 7 wa kiabbasi
 - Imam Muhammad Taqi (a) alipewa sumu na Mu‘tasim Billah Rashid (l.a.), khalifa wa 8 wa kiabbasi
 - Imam Ali Naqi (a) alipewa sumu na Mu‘taaz Billah (l.a.), khalifa wa 13 wa kiabbasi
 - Imam Hasan Askary (a) alipewa sumu na Mu‘tamad (l.a.), khalifa wa 15 wa kiabbasi

⁶¹ Wanazuoni, waliohifadhi hadithi za Mtume (s)

kuonekana ngeni. Kweli watu hufuata dini ya watawala wao na sio dini ya ulamaa wao.

Bila shaka wapo wanazuoni madajjali waliojiingiza na kupandikizwa kwa lengo la kuharibu Uislamu. Watatilia mkazo namna ya kutawadha lakini mambo yanayohusu uongozi, siasa uchumi na maendeleo ya ummah ni wa kwanza kuyapuuza na kuyafunika. Hawa wana faida gani kwa ummah huu. Hao ndiyo wanakula fadhila za watawala dhalimu wanaotetea '*hizbu Shaytan*', na hivyo wao kuwa ni maaskari watetezi wa nidhamu ya utaghuti. Hawa ndiyo wanazuoni waovu wanaopiga magoti mbele ya hekalu za wafalme. Hawa ndiyo waliotekeleza agenda ya siri ya kuwagawa Waislamu katika madhehebu mbalimbali na kisha kuwasha moto wa fitna na kuendelea kupakia kuni ili moto usizimike.

3. Itikadi ya Imam Mahdi (as) ni Sahihi:

Itikadi ya Imam Mahdi (as) ni sahihi kwa mujibu wa Qur'ani na Hadithi sahihi. Pia historia inathibitisha kuwepo Imam Mahdi (as) ambaye ndiye Imam (as) wa zama hadi mwisho wa zama. Ulamaa na Huffadh wa Hadithi wamethibitisha kwamba hadithi za Mahdi ni Sahihi na Mutawaatir. Kukadhibisha itikadi hii ni matokeo ya mapambano marefu baina ya Uislamu na viongozi dhalimu waliowatawala Waislamu.

4. Ushia wa Ahlul Bayt (as) ndiyo Uislamu halisi:

Ushia ni kufuata Qur'ani na Sunnah sahihi ya Mtume (saww) na kushikamana na Ahlul Bayt (as) kwamba wao ndiyo viongozi (makhalifa, maimamu, maamiri) wa waumini baada ya Mtume (saww). Hii ndiyo amri ya Qur'ani na Sunnah. Miongoni mwa Masahaba, watoto wao, Matabiina wako waliofuata amri hiyo na kui-

simika hadi leo. Mashia ni wafuasi wa Qur'an wa Sunnah. Iwe ni zamani au hivi sasa, ni watawala dhalimu na wanazuoni wanaokula fadhila zao, ndiyo chanzo cha ugomvi wa kimadhehebu na kuwaku-furisha Mashia.⁶² Siasa na uroho wa madaraka na pia uadui dhidi ya haki ndiyo sababu kubwa za kuwatenga Mashia.

5. Uimamu, Ukhalifa wa Allah ndiyo msingi wa kusimamisha Umoja wa Ummah:

Ni jambo lililo wazi kwamba Ukhalifa ni muhimili muhimu kati-ka kusimamisha umoja wa ummah huu. Lakini suala la msingi ni: Ukhalifa upi?

Historia inaonyesha kwamba Waislamu, ukiondosha kipindi cha miaka 30 baada ya Mtume (saww), wametawaliwa na watu madhalimu waliovunja waziwazi sheria za Kiislamu na Sunnah ya Mtume (saww), wakazusha maovu ya kila aina na wakawadhulumu Waislamu na baya zaidi wakachochea migogoro ya kimadhehebu na kuwafarakisha Waislamu. Mfano:

⁶² Baada ya kusimama serikali ya Kiislamu Iran, watawala wa bara Arabu walishirikiana kuipiga vita Iran kwa kumsaidia kwa hali na mali Saddam Hussein, tabaan, kwa amri ya adui wa Uislam Marekani na Israeli. Wote hawa ni kuogopea kuanguka utawala wao ikiwa Uislamu utasimama imara. Hawakutosheka na vita, bali waliandaa wanazuoni wa kuja kuzusha fitna katika ummah wa Kiislamu kwa kusisitiza kwamba Ushia ni ukafiri!? Bali ulamaa wanaharakati wenye kutaka serikali ya Kiislamu wote hao wamepotea!!! *Hizbullah*, imesimama leo kwa miaka zaidi ya 25 kupambana na uvamizi wa Israeli huko Lebanoni. Kuliko kupata msaada wamekuwa wakifanyiwa kila njama na vitimbi ili waangamizwe. Hawa ndiyo watawala wa Ghuba na huo ndiyo Uislamu wao ambao ni kulinda utawala wao wa kitaghuti na maslahi ya mabwana zao, Marekani na Israeli, hata kama Uislamu na Waislamu wataangamia!!! Watasaga meno sana, watapanga na kupangua, Uislamu halisi na sio mseto utashinda. Msafara wa Mtume (s) lazima usonge mbele hata kama mbwa watabweka (wafaransa wanasema: 'le chien aboie, la caravane passe', maana yake 'mbwa abweka, msafara waendelea na safari yake). Leo baada ya miaka 30 ya mapinduzi ya kiislamu huko Iran, Iran imepiga hatua na kuendelea katika kila uwanja wa sayansi na teknolojia. Huo ndio Uislamu na huo ndiyo uongozi.

- Muawiya bin Abu Sufyan, pamoja na kuwa ni sahaba, alifanya maovu makubwa yasiyo na mithili dhidi ya Mtume (saww) na ummah huu.
- ▶ Alisimamisha vita dhidi ya Khalifa wa zama zake, Imam Ali (as) na kusababisha maangamio makubwa ya Waislamu katika vita vya Swiffin.
- ▶ Alilazimisha Waislamu wamlaani Imam Ali (as) na kuwaua na kuwatesa wapenzi na wafuasi wa kizazi cha Mtume (saww), yaani *Shia Aali Muhammad (saww)*. Siasa hii mbaya ilijenga mfarakano katika Ummah kwa kuwatenga Mashia kwamba wamepotea. Na wasio wao ndiyo wameongoka. Kuwepo ukuta baina ya Usunni na Ushia ni matokea ya siasa na fitna ya watawala hawa madhalimu ambao hawakujali Qur’ani wala Mtume (saww) wala Waislamu bali maslahi yao. Walielewa kwamba ili kuwatawala Waislamu ni lazima kuwagawa na wale wote wanaowapinga, si Waislamu, waitwe makafiri. Siasa hii ilienezwa na wanazuoni muflisi ambao wanaabudu ikulu za wafalme.
- ▶ Ni yeye Muawiya ndiye aliyepanga njama na kumuua Imam Hasan (as), mjukuu na kipenzi cha Mtume (saww), mmoja katika *Ahlul Kisaa* watu waliotoharishwa na Allah.
- ▶ Ni yeye ndiye aliyemtawalisha mwanae khabithi Yazidi, Shetani jabbari asiyemjali Allah wala Mtume. Alimuua Imam Husayn (as) na kizazi cha Mtume (saww), akaishambulia Madina na kufanya uovu mkubwa, na baadaye akaishambulia Makka, na kuipiga kwa manjaniki.⁶³

⁶³ Ndugu Mwislamu, haya ni machache tu, soma zaidi historia, kwani kujua kwako ndio kuukomboza Uislamu. Hawa watawala dhalimu na wanazuoni wao ndiyo waliobuni hadithi zinazopingana na Qur’ani na Hadithi sahihi, kama hii: **‘masahaba wangu ni kama vile nyota, yeyote mtakayemfuata mtaongoka’?!!!!** Ee ajabu! Muawiya tumfuate kwa

- Baada ya Yazid walifuatia makhalifa wa ukoo wa Bani Umayyah na baadaye Bani Abbas ambao sera zao zilikuwa ni hizo hizo. Je hao ndiyo makhalifa tunaowataka? Hao wana tofauti gani na Bani Saud wa Saudi Arabia⁶⁴, Jamal Abdi Nasir⁶⁵, Sadat⁶⁶, Mubarak wa Misri, Saddam Husein⁶⁷ wa Iraq, Shah⁶⁸ wa Iran ... Au hawa ndio *Ulul-Amr* wa kweli tuliofaradhishwa na Mwenyezi Mungu kuwafuata? Watawala vibaraka wa Ukafiri ambao wamedhalilisha ummah huu kwa kutumikia maslahi ya mabwana zao, makafiri na mazayuni.

Ukhalifa wa Mwenyezi Mungu ndani ya ardhi ni dharura. Lazima iwepo Hoja ya Allah yenye sifa kamili za ukhalifa wa Allah. Watu wakimfuata na kumnusuru, hapo ndipo Tawhid itakaposimama na umoja kupatikana. Mfano mzuri hivi sasa ni **Utawala wa Faqih huko Iran**. Waislamu walipoelimishwa umuhimu wa kuwafuata ul-amaa kama mawakili wa Imam, walishikamana chini ya uongozi wa Ayatullah Khomein (qs) na kufanya mapinduzi na kung'oa utawala wa kifalme wa Shah.

6. Matunda ya Mti wa Utume uliobarikiwa:

Mwenyezi Mungu alimchagua na kumbariki Nabi Ibrahim (as) na Aali zake (Surah al-Baqara, 2:130, Surah Aal-Imran, 3:33). Maelezo

lipi? Kwa kuua kizazi cha Mtume (s), wachamungu wanaopinga dhulma na Mashia wao? Bila shaka tunaona nani leo anatekeleza sera hizo.

⁶⁴ Bani Saud: ukoo unaotawala Hijaz (Saudi Arabia)

⁶⁵ Jamal Abdi Nasser: rais wa Misri (1956-1970) pamoja na kuwa kiongozi mashuhuri, alipambana na wanaharakati wa Kiislamu, *Ikhwanul Muslimiin*, ambao ajenda yao ilikuwa kusimamisha dola ya kiislamu. Alimua 'Alim mkubwa na fahari ya Uislamu Sayyid Qutb mwaka 1966. Aliandika tafsiri ya Qur'an, '*Fii Dhillil Qur'an*', akiwa jela.

⁶⁶ Anwar al Sadat: rais wa Misri (1970-1981). Ni yeye ndiye aliyewadhalilisha waarabu na Waislamu kwa ujumla kwa kuitambua Israeli, dola saratani katika ulimwengu wa Kiislamu, katika mkutano wa Camp David, huko Marekani, mwaka 1978-1979

⁶⁷ Saddam Husein, aliyekuwa rais wa Iraq (1979-2003)

⁶⁸ Muhammad Reza Shah Pahlavi (1919-1980), shah wa Iran (1941-1979)

haya yanapatikana katika Biblia, (Mwanzo/Genesis, 22:17-18, 12:2-3). Kwa kupitia Nabii Ismail (as) na Nabii Is-haq (as), watoto wa Ibrahim (as), Mwenyezi Mungu amebariki Dunia na walimwengu. Mitume wengi katika kizazi cha Is-haq (as) wamekuja na kuwaongoza wana wa Israeli na walimwengu kwa ujumla. Miongoni mwao ni: Nabii Ya'qub, Yusuf, Musa, Harun, Dawud, Sulayman, Isa (Yesu) (wote juu yao amani). Katika kizazi cha Nabii Ismail (a.s.) amekuja Mtume wa mwisho, Mtume Muhammad (saww) na Aali Muhammad (as), ili kuwaongoza walimwengu hadi kitakaposimama Kiyama. Kwa ajili ya kusimamisha Haki dhidi ya Batili, hapo Zama za mwisho, Mwenyezi Mungu amewahifadhi Nabii Isa (as) na Imam Mahdi (as)...

7. Tuache kutetea mifumo batili:

Mwenyezi Mungu alikwisha hukumu kwamba atashinda Yeye na Mitume wake (58:21). Ni ujinga mtu kupoteza umri wako na uhai wako wote kwa ajili ya kutetea mifumo batili ambayo inasimika uovu na ufidadi na mwisho wake ni kuangamia. Hebu jaribu kuruka ndani ya zama na kuingia zama za Imam Mahdi (a.t.f.). Zama hizo mifumo yote batili itatoweka. Mfumo utakaobaki ni ule wa Mwenyezi Mungu na wa Mitume wote, Uislamu halisi au *Allahkrasia*. Mifumo batili ni kama ifuatayo:

- Mfumo wa ufalme, usultani (*monarchy system*). Huu ndiyo unaoongoza nchi za Kiislamu kama Saudi Arabia, Jordan, Uman, Kuwait...
- Demokrasia na Ubepari (*Democracy and Capitalism*).
- Ukomunisti na Udikteta (*Communism and Totalitarianism*).
- Dini mseto. Hii ni dini kubadilishwa na kupokea itikadi potofu na hatimaye dini kutumika kwa maslahi ya mataghuti na wote madajjali.

Mfano katika Uislamu: Ni wazi kwamba aya nyingi zinakataza waumini kutambua uongozi wa kikafiri, bali unawataka waumini wapambane na fitna ya ukafiri mpaka waiondoshe kwani fitna ya ukafiri ni mbaya kuliko kuua (2 :191,217). Mwaka wa 61 H., Waislamu walitawaliwa na Yazid bin Muawiya bin Abi Sufyan, kiongozi dhalimu mwenye sifa zote za ukafiri kiasi cha kuamrisha majeshi yake yafanye uchafu ndani ya Madina⁶⁹ na kuibomoa Kaaba. Mashetani wakawa makhalifa wa Mtume (saww)!!! Hii ilikuwa ni matokeo ya kubadilisha mafunzo ya Qur’ani na kuzusha hadithi za uongo. Mafunzo potofu ni kusema: **‘Mwenyezi Mungu ndiye Mfalme na Yeye ndiye mwenye kumpa ufalme amtakaye...’**(3 :26) kwa hiyo kama Yazid amekuwa khalifa, basi Mwenyezi Mungu ndiye ametaka kumpa ufalme, kama asingependa kamwe asingekuwa khalifa. Kwa hiyo hatuna budi ila kumkubali na kumtii Yazid. Kumkataa ni kukataa alivyotaka Mwenyezi Mungu na hivyo kusababisha fitna na mauaji!!! Hii ndiyo imani potofu kuhusu **Qadha na Qadari**⁷⁰ ambayo ndiyo mkwaju uliong’ang’aniwa na mataghuti na wanazuoni wao kudhalilisha ummah huu.

⁶⁹ Vita vya Harra:

⁷⁰ **Qadha na Qadari:** Mwenyezi Mungu alipoumba ni kwamba alitaka na kuamua maumbile, nidhamu na viwango kuhusu kila kiumbe. Maumbile, kanuni, viwango alivyoweka Mwenyezi Mungu havitabadilika. Hii ndiyo maana ya kusema: ‘Sunnah ya Mwenyezi Mungu haitabadilika’. Kwa hiyo kanuni zote za kimaumbile, kazitaka na kuziweka Mwenyezi Mungu na hawezi kuzibadilisha mtu yeyote.

- Kuhusu riziki, Mwenyezi Mungu katuwekea riziki ndani ya ardhi na mbingu na akatupa akili na uwezo wa kuitafuta na njia za kuimiliki. Sasa ikiwa mtu atatumia wizi, ghilba, ujanja, ubabe, akapata mali nyingi, je ni Mwenyezi Mungu ndiye kamariki?! Bila shaka huwezi kusema ndiyo.
- Kuhusu ufalme ni hivyo hivyo.

8. Kila anayemsubiri Mahdi, lazima kujiepusha na udhalimu na kupambana:

Kukomesha udhalimu kunategemea taratibu zifuatazo:

1. Watu kuelewa udhalimu unaofanywa, na ni nani kitovu cha udhalimu huo.
2. Watu kuukataa udhalimu huo na kuwa tayari kupambana nao.
3. Watu kujua uongozi sahihi na kumtambua kiongozi wa *Al-lahkrasia*.
4. Watu kuwa tayari kumfuata na kumnusuru.
5. Kumuomba Mwenyezi Mungu msaada na kuwa na subira katika mapambano.

9. Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ni mfano wa kuigwa na kuji-vunia kwa Waislamu wote:

Kama ilivyotangulia, kusimama dola madhubuti ya Kiislamu kabla ya kudhihiri Imam Mahdi ni lazima. Mapinduzi ya Kiislamu ya Iran ya mwaka 1979, ni katika maajabu ya karne ya 20. Hakuna aliye-fikiria kwamba utawala wa mfalme Muhammad Reza Shah Pahlavi ungeangushwa na kiongozi wa kidini bila bunduki wala jeshi. Pamoja na kupigwa vita na mataifa ya Magharibi, Israeli na vibaraka wao katika Ghuba, kwa baraka za uongozi adilifu wa Kiislamu, Iran ime-piga hatua kubwa kisiasa, kijami, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Ndani ya Iran, Uislamu umethibitisha uwezo wake wa kuongoza ulimwengu na kuleta maendeleo ya kiroho na kimada na hivyo kufikia amani ya kweli kwa wote. Waislamu, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii na siyo kuyapinga kwa sababu za ushabiki wa kihizbu au madhehebu. Mafanikio yaliyopatikana Iran katika

miaka 30 ya mapinduzi ya Kiislamu ni muujiza wa Qur'ani na Uongozi sahihi kama alivyotusua Mtume (saww). Bila shaka watawala wa Ghuba kwa kuhofia madaraka yao hawawezi kuyastahamia. Hawa ndiyo wanaotumia dini (kwa kuwasha moto wa umadhehebu na mfarakano) kwa maslahi yao ya kisiasa (kuendelea kuwatawala Waislamu kwa mifumo ya kitaghuti).

10. Nidhamu ya Mahdi (a.t.f.) siyo nidhamu ya kubweteka na kumsubiria aje kufyeka uovu na kuung'oa:

Hii ni nidhamu iliyo hai inayofanya kazi na kuandaa mazingira ya kudhihiri Imam (a.t.f.). Imam hatodhihiri ila baada ya watu kuwa tayari kujitolea muhanga kunusuru nidhamu ya Allah. Hii ina maana kwamba kila anayemsubiri Imam (as) ni wajibu wake kupinga dhulma, kuandaa na kujenga nidhamu ya haki, kama vile nidhamu ya Dajjal inavyofanya kazi kuandaa mazingira ya kumkubali mungu binadamu (Dajjal).

11. Imam Mahdi (a.t.f.) na Umadhehebu:

Zama za Imam, umadhehebu utatoweka na dini itarejea katika uhalisi wake kama ilivyokuwa zama za Mtume (saww), Uislamu bila madhehebu. Tukizingatia haya, kila anayemfuata Imam na kumtarajia ni lazima aelewe kwamba adui mkubwa wa ummah ni umadhehebu (kutetea madhehebu kwa ushabiki). Lazima tujenge mtazamo mpya kwa waumini ambao lengo si kutetea madhehebu bali ni kufuata lililo sahihi kwa mujibu wa Qur'ani na Sunnah. Hili linahitaji watu kuwa huru kiakili na kuchunguza maandiko bila kuweka pazia na mipaka ya kimadhehebu.

Ni muhimu kuelewa kwamba chanzo cha madhehebu ni hila na mbinu za watawala na maadui wa ummah huu. Kila anayetilia mkazo fitna za kimadhehebu huyo ndiye adui wa Ummah huu na

wala hana chembe cha Uislamu, bali ni adui ambaye mungu wake ni utawala na dunia.

12. Mahdi wa Kisunni na Mahdi wa Kishia:

Maadui wa Uislamu, watawala wanafiki, makafiri, mayahudi wanajua fika kwamba umoja wa Waislamu ni kifo cha nidhamu yao ya udhalimu na ukandamizaji. Mbinu kuu ambayo wamekuwa wakiitumia ni kuwafarikisha Waislamu kwa kusimika itikadi kinzani na kujenga umadhehebu. Wamewatumia wanazuoni waovu ambao wamevaa joho la dini na uchamungu kusambaza sumu hii hatari.

Kwa kuelewa hilo, siyo ajabu kuona kwamba Mawahhabi leo wanapiga tarumbeta na kutangaza kwamba Imam Mahdi wa Kisunni ni tofauti na Imam Mahdi wa Kishia, tofauti kama vile ya mbingu na ardhi⁷¹. Imam Mahdi wa Kisunni atazaliwa hapo katika zama za mwisho, ama huyu wa Kishia ni wa kubuni kwa madai ya kipotofu ya Mashia ambao wanazua kuwa ni Imam wa kumi na mbili na alitoweka ndani ya sardabu hapo Samarraa. Ee Mola! Huu ni uongo unalenga kuwapotosha Waislamu wasimjue Imam wao na wabaki ni kondoo waliopotea hawana mchungaji, kila mmoja analiwa kama tunavyoshuhudia. Mawahhabi ni bora waelewe yafuatayo:

- Wao siyo wasemaji wa Usunni. Kudai eti itikadi ya Masunni ni kwamba Imam Mahdi atazaliwa siyo kauli thabiti kwa dalili ya Qur’ani na Sunnah. Hebu watuletee hadithi sahihi inayosema Imam Mahdi atazaliwa! Hivi kwa hadithi zote nyingi hizi alizozungumza Mtume kuhusu maisha ya Imam Mahdi (as) - ambazo na wao Sunni wenyewe pia wanakubali kwamba ni *Mutawaatir* - ni vipi Mtume akaacha kuweka wazi kuhusu kuzaliwa kwake na nasaba yake?! Kwa kuzingatia shakhsia ya

⁷¹ Mahmud, Swalaahud-Diin, *Ashraatus Saa’ah*, uk. 111.

Imam Mahdi na kazi yake, huyu ni mtu muhimu, mwenye nafasi ya pekee katika historia ya mwanadamu. Ni mtu atakayesimamisha ushindi wa haki dhidi ya batili, mtu atakayesimamisha utawala wa Mitume kote duniani. Ni vipi mtu kama huyu mtukufu, Mtume (saww) asielezee kwa mapana habari zake? Bali kama vile habari za Mtume (saww) zilivyoelzwa na Mitume wa kabla, mpaka Mayahudi wakamjua Mtume (saww) kama vile wanavyojua watoto wao, ndivyo Mtume wetu alivyotuwekea wazi habari za Imam Mahdi (as) ili asije akapotea ila yule mpotofu na asiyetumia akili yake wala kuzingatia.

- Ama ulamaa wa Kisunni na Hufadhi wa hadithi, wako wengi waliokubaliana na Mashia kwamba Imam Mahdi ni Imam wa Kumi na Mbili. Rejea dalili za kihistoria, B, katika kitabu hiki.
- Mtume (saww) siyo abtaru, kama wanavyodai, bali Allah alimpa mbora wa viumbe wake kizazi kilicho bora kuliko kizazi chochote kile; wao ni Aali Muhammad, (Aali Yaasin), ambao ni bora kuliko Aali Ibrahim, Aali Ya'qub, Aali Imraan,... Hawa ni Maimamu kumi na mbili ambao ni warithi wa Qur'ani na Sunnah. Wote hawa wamesimulia kutoka kwa babu yao Mtume (saw) hadithi za Imam Mahdi (as) kwamba ni Imam wa kumi na mbili na mtoto wa Imam Hasan 'Askari (as). Sasa tufuate ya nani? Ya Mtume na Aali zake au ya Ibnu Taymiyyah, Ibnu Qayyim Al Jawzi, Muhammad Abdulwahhab na akina Al Baany na Ibn Baaz maimamu wa Mawahhabi?
- Huu ni mfano mzuri unaofichua na kuweka wazi nguvu zinazotumika kuhakikisha kwamba Mashia na Masunni hawakubaliani hata kama zipo sababu za kukubaliana. Ni muhimu kwa kila muumini kuwa macho na kufichua fitna na mbinu za maadui wa ummah waliovaa joho la dini ili kutekeleza agenda za mabwana wao za kutawala na kuwakandamiza Waislamu.

AMBATANISHO

Ambatanisho 1: Mkabala na Allamah Harun Yahya kuhusu Imam Mahdi (as)

An interview with Harun Yahya



1. To what extent is belief in the Mahdi prevalent in the Sunni faith today? Can you give a percentage?

Belief in the Mahdi has always been of great importance in the Islamic world. That applies to both Sunni and Shia faiths. Although there are some differences in the beliefs of these two major sects, the essence of the belief in the Mahdi is the same. Both Shias and Sunnis are awaiting a saviour who will liberate the world from all its troubles.

According to Sunni beliefs, the fundamental source is the hadiths of our Prophet (saws), in which belief in the Mahdi is described in

very clear terms. There is agreement among Islamic scholars that these hadiths are based on reliable sources. The subject of the Mahdi is clearly set out in Abu Dawud, Tirmidhi and Ibn Majah's collections of hadiths. In Bukhari and Muslim there is reference to a saviour, described as an *imam*, who will come in the end times. Belief in the Mahdi is therefore very powerful in the Sunni faith.

⇒ Imani kuhusu Imam Mahdi (a.t.f.) ni muhimu katika ulimwengu wa Kiislamu bila kujali madhehebu. Waislamu wote wanamsubiri kuja kuokoa ulimwengu na kusimamisha haki na uadilifu. Katika Sunni, imani hii ni thabiti kwa kutegemea hadithi sahihi kutoka Sihah Sittah.

2. Does belief in the Mahdi have a widespread influence on all classes, on all sections of society, in Sunni Islam, or have some certain sections adopted it more than others?

Belief in the Mahdi has always enjoyed a very important place in the entire Islamic world. Among Muslims there are and have always been, of course, individuals or groups who have not adopted this belief, who reject certain aspects of it, or who put forward different views. However, these are generally movements or individuals who have adopted views that are incompatible with Islamic beliefs, who reject trustworthy hadiths and have conflicting views. These represent a very small minority in the Islamic world. The fact is that despite there being some differences in belief on the subject of the Mahdi in the Islamic community there is still enormous consensus. I can see this from the very positive reactions from different countries and sections of society to my books dealing with the end times and the Mahdi. I also see how powerful this belief is in the hearts of Muslims from the messages reaching our web sites. Muslims across

the globe, from Indonesia to South Africa, from Britain to China, and from Canada to Australia possess a very deep faith and broad information on the subjects of the end times and the Mahdi.

⇒ Katika ulumwengu wa Kiislamu wako baadhi ambao walipinga usahihi wa itikadi hii. Lakini wengi ni wenye kuamini kwamba lazima Mahdi atadhihiri. Nimeshuhudia hili kwa athari ya kitabu changu *'The End Times And The Mahdi'*. Kote duniani kimepokelewa vyema.

3. What are your personal and religious views on those people who have previously declared themselves to be the Mahdi (Ibn Tumart, Muhammed Ahmed, and Manisali Mehmet in 1930s Turkey)?

I do not wish to concentrate on individuals, but according to what is related in the hadiths it appears that before the return to earth of the Prophet Jesus (peace be upon him) and the appearance of the Mahdi there will be a large number of false saviours claiming to be the Mahdi and Jesus. The appearance of such people may cause people to treat everyone who says that they are Jesus or the Mahdi with suspicion. The great Islamic scholar Bediuzzaman Said Nursi describes such people in these terms:

I have also seen many people who thought themselves to be a sort of Mahdi, and they said that they were going to be the Mahdi. These people are not liars and deceivers, they are deceived. They suppose what they see to be reality. As the Divine Names have manifestations from the sphere of the Sublime Throne down to an atom, and the places of manifestation differ in that relation, so the degrees of sainthood, which consist of manifesting the Names, differ in the same way. (Bediuzzaman Said Nursi, *Risale-i Nur Collection, The Letters, The Twenty-ninth Letter, Fourt Allusion*)

As stated by Bediuzzaman, these people will be quite certain that they are the awaited saviour. The existence of these false individuals may also have an important role to play in the recognition of the Mahdi and Jesus. Since people will have been exposed to false saviours for many years they may not recognise the Mahdi for a long time. Similarly, it is very likely that they will not recognise the Prophet Jesus when he returns because they have been exposed to people describing themselves as the Prophet Jesus for so long. However, it must not be forgotten that the appearance of false messiahs is also a sign of the coming of the two personages of the end times - Mahdi and the Prophet Jesus. Our Prophet (pbuh) related these glad tidings in these terms in his hadiths:

The Last Hour will not come before there come forth thirty Dajjals (imposters), each presenting himself as an apostle of God. (Sunan Abu Dawud)

Some false messiahs and mahdis have emerged, and others will do so in the years that follow. (God knows best.) Without any doubt, the days when the false messiahs with all their falsehoods appear are very close. That is because our Prophet (pbuh) has imparted the glad tidings of the return of the Prophet Jesus and the coming of the Mahdi in the wake of these liars.

4. How can a false Mahdi be distinguished from the true Mahdi?

In his hadiths our Prophet (pbuh) has described all the features of the Mahdi in great detail. Islamic scholars have also provided very important information about the Mahdi. Therefore, it is of great importance whether or not an individual supposed to be the Mahdi actually possesses those features. These are: being descended from the

Prophet (pbuh), bringing Islamic moral values to prevail over the whole world, cleansing Islam from all the additions and beliefs that evolved after our Prophet, bringing peace and security to the world, establishing Islamic union, eliminating sects, for the entire Islamic world to submit to him, and forming an alliance with the people of the book. When these things take place, then we may consider that this person is the Mahdi or an extraordinary human being.

Throughout history there may have been worthy Islamic scholars who have met some aspects of the criteria I have set out above. However, the actual Mahdi of the end times will combine all these features, on his own and within himself. The great Islamic scholar Bediuzzaman Said Nursi describes the differences between these people and the true Mahdi thus:

The Great Mahdi will have numerous functions. He will carry out duties in the world of politics, the world of religion, the world of government, and in the many spheres of the world of Islam. Similarly, since every century at a time of despair people are in need of a sort of Mahdi to strengthen their morale or for the possibility of a Mahdi appearing at that time to assist them, through Divine mercy, every age or perhaps every century a sort of Mahdi has appeared from among the Prophet's (PBUH) descendants, and preserved his forefather's Shari'a and revived his Sunna. (Bediuzzaman Said Nursi, *Risale-i Nur Collection*, The Rays, The Second Station of the Fifth Ray, Ninteenth Matter)

Said Nursi has made it clear that the Mahdi will be active in the political arena and be present at the highest level of state administration. Indeed, for him to be active in politics, in religion and in communicating the message requires the very broadest means. We can see from this that the Mahdi will have such very broad means, and that these duties can only be fully carried out with the use of

state powers. This is the major difference between the Mahdi and those individuals believing themselves to be the Mahdi in the end times. The Mahdi will be active worldwide, will not be held back by limited individuals, will wage a major intellectual struggle in all spheres, and will, by God's leave, cause Islam to prevail over the whole world.

5. What kind of relationship will there be between the Prophet Jesus and the Mahdi when both are on the earth?

According to the hadiths, when the Prophet Jesus returns to earth he will act together with the Mahdi, and the two will combine all their powers to bring religious moral values to prevail in the world. The Prophet Jesus will eliminate the Anti-Christ (Dajjal), the leader of the atheistic system in the world, and the Mahdi will assist him in that struggle. The Prophet Jesus and the Mahdi are two brothers with great love for one another in this world and in the hereafter. They will share the same thoughts and beliefs. The Mahdi will be the spiritual leader of the Islamic world, and the Prophet Jesus that of the Christian world. Under their twin leadership the world will enjoy great peace, security and happiness.

6. Could you describe your analysis of the hidden imam in Shiite belief?

As you know, according to Shiite belief, the statements made by Fatima, Zahra and the 12 imams are regarded as equal to those made by the Prophet Muhammad (pbuh). In Sunni belief, on the other hand, only the hadiths of our Prophet (pbuh) are reliable. For that reason, in terms of numbers, the Sunnis possess fewer accounts about the Mahdi than there are in Shiite sources. In Shiite sources some 700

accounts giving the glad tidings of the appearance of the Mahdi are reported. There are some 400 reports that the Mahdi will be from the Ahl al-Bayt (The Prophet's family). In addition, there are hundreds of other reports describing the Mahdi's appearance, actions, struggle against the unbelievers, and the kind of environment there will be when he prevails. The subject of the Mahdi is the most important creed in Shia belief, and they believe that the Mahdi, whom they refer to as the "Lord of Time," will one day appear. Throughout history many people from the Ahl al-Bayt have been regarded as the Mahdi, yet since they have been unable to fulfill what was expected of them, hope has always given way to the expectation of a new Mahdi.

The Shiite belief in the Mahdi is based on "the disappearance of the Mahdi and his coming to earth as the last of the 12 imams." In some hadiths, it is reported that after his appearance the Mahdi will twice remain apart from people, once for a short time and once for a long time. This is stated as follows in one hadith: *"The Mahdi will twice disappear from human sight. On one occasion he will remain unseen for so long that some people will think he has died and others that he has departed, and apart from his closest followers, nobody will know where he is."* (Al-Muttaqi al-Hindi, *Al-Burhan fi Alamat al-Mahdi Akhir al-Zaman*)

In this hadith it is stated that the second disappearance of the Mahdi will be under harsher conditions and will be of a longer duration, that it will be difficult to encounter him during that time and that only his closest followers will be able to do so. As we know, the Mahdi will wage a great intellectual struggle against the deniers, atheists and materialists. He will expend great efforts, using all his power and all the means at his disposal, to bring Islamic moral values to prevail on earth. Since one cannot imagine that the Mahdi would knowingly vanish at such an important time, his separation

from people will take place “outside his own will.” Indeed, one hadith reads: *“One day it was stated in the presence of Huzaiifa that the Mahdi had emerged. He said: ‘You have found happiness if he comes from among you as a companion of the Prophet Muhammed. Certain it is that because of the evils people encounter the Mahdi will not appear until he is the most beloved of people’.”* (*Al-Muttaqi al-Hindi, Al-Burhan fi Alamat al-Mahdi Akhir al-Zaman, p. 27*)

In other words, the disappearance of the Mahdi is not a mythical one that will last for hundreds of years, but may take place in the form of an enforced separation from people at specific intervals. The last part of this hadith indicates that at the time of this disappearance people’s love and longing for the Mahdi will increase due to their being subjected to various evils.

The disappearance of the Mahdi may also indicate his concealing himself. That is because he is under constant assault and pressure from atheists and materialists. He is unable to live a comfortable day-to-day life like other people. He must constantly conceal himself and remain apart from people. He can prevent the attacks and slanders made by the deniers only in this way.

7. What would your thoughts be regarding someone who declared himself to be the Mahdi today?

(For example, I have found Sunni sources wondering whether Osama bin Laden might be the Mahdi). Someone’s declaring himself to be the Mahdi is the clearest proof that he is not the Mahdi. That is because if someone says, “I am the Mahdi,” he is in fact claiming that “I am innocent, I have no need to be tested, I am not torn between hope of paradise and fear of hell, I am under the guarantee of paradise, and revelations come to me.” Such a claim is a violation

of the verses of the Qur'an and Islamic moral values. Unless such a claim stems from heedlessness, it must be based on atheism. The Mahdi will not bother saying, "Accept me as the Mahdi," and will feel no need to make such a claim. That is because being the Mahdi means success. As related in the hadiths of our Prophet (pbuh), being a means whereby Islam comes to prevail on the earth is an undeniable feature of the Mahdi. In his works, Bediuzzaman Said Nursi has set out the attributes of the Mahdi's blessed person in great detail. In describing the duties of the Mahdi, Bediuzzaman states that the establishment of an Islamic Union will be one of the three greatest of these. The passage in question reads:

THE THIRD DUTY OF THAT INDIVIDUAL (the Mahdi) is to build an Islamic Caliphate on an ISLAMIC UNITY AND TO SERVE ISLAM by allying himself with Christians. This duty can be fulfilled by A GREAT CALIPHATE and force and the sacrifices of millions. The first duty is three to four times more valuable than the other two. However, since the second and third duties will be in a very bright and broad sphere and in a glittering manner they will appear more important in the eyes of the people and the community." (Sikke-i Tasdik-i Gaybi, p. 9)

As Bediuzzaman makes clear, the Mahdi will first construct an Islamic Union. He will then draw strength and support from the Islamic Union and cause religious moral values to prevail across the world. In fulfilling this sacred duty, by the leave of God, he will possess great power, strength and dominion. When the blessed person of the Mahdi appears, by God's leave, the Mahdi's great deeds will be the greatest proof and evidence that this holy individual has actually emerged. It is reported in one hadith that "people will pledge allegiance to the Mahdi, albeit against his wishes:

